**13 APRILI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Saba – Tarehe 13 Aprili, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda, aulize swali lake.

Na. 61

**Ujenzi wa Shule ya Amali, Manchimweru**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Shule ya Amali Manchimweru?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuboresha elimu ya mafunzo ya amali kwa ngazi ya sekondari, Serikali katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilitoa shilingi bilioni 88.84, kwa ajili ya ujenzi wa shule 103 za amali za kihandisi ambapo shule 29 zilipokea fedha za ujenzi wa miundombinu yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule 74, ikiwemo shule ya Manchimweru, Wilayani Bunda, zilipokea fedha za ujenzi wa miundombinu kwa awamu ya kwanza. Shule hii ilipokea shilingi milioni 584.28 ambapo ujenzi wake umefikia 92% na tathmini inaonesha kiasi cha shilingi milioni 950 kinahitajika ili kukamilisha ujenzi kwa awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa shule hizi unafanyika kwa awamu, na hivyo, shule ya sekondari ya Manchimweru itapelekewa fedha za ukamilishaji mara utekelezaji wa awamu ya pili utakapoanza, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaomba tu masahihisho madogo, humu Bungeni hakuna Jimbo linaitwa Bunda Vijijini, kuna Jimbo linaitwa Bunda. Kwa hiyo, mnapo-*address* muwe mnajua kuna Jimbo linaitwa Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi shule za amali maana yake ni kwamba, wananchi walipokea malengo yake vizuri sana kwa sababu, ni shule za kiufundi. Nimeomba *VETA* humu zaidi ya miaka kumi, nikaambiwa tutakupa shule ya amali, ambayo ni shule ya ufundi. Shule imekamilika, sasa ni miaka mitatu. Sasa hizi fedha tukisema zipo

kwenye bajeti maana yake, malengo ya kutekeleza hizo shule itakuwa ngumu. Ni lini sasa hizo fedha zitaenda ili wananchi waone kwamba, sasa wanaenda kujengewa shule ya ufundi, kama ilivyokuwa imependekezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Shule ya Sekondari Sanzati na Shule ya Sekondari Tingirima nimeenda pale wameshapima, wamejenga, majengo hayajakamilika yote, Serikali ilitoa fedha pale. Ni lini mtaenda kukamilisha majengo ya shule hizo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Jimbo la Bunda kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya ya kuwasemea wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ujenzi wa shule za amali za sekondari ni matokeo ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2014, Toleo la 2023, ambalo mambo makubwa matatu yaliyopitishwa na sera ile, kwanza ni ujenzi wa shule za amali za sekondari ya chini kwa maana ya *O-Level.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhakikisha kwamba, somo la maadili na uzalendo wa Taifa linafundishwa. Tatu, ni kuhakikisha kwamba, tunaendelea kuboresha sana elimu ya msingi kwa kuweka darasa la kwanza hadi la sita na kidato cha kwanza hadi cha nne, kwa maana ya madarasa 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, ujenzi wa shule hizi za amali, kwanza unahitaji shilingi bilioni 2.6, ili ukamilike. Shule zote 103 zilipewa fedha awamu ya kwanza, kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya elimu kwa shule za *day* na sasa Shule hii ya Manchimweru inatoa huduma, ina wanafunzi takribani 299 na awamu ya pili ipo kwenye mpango. Wakati wowote tutapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha shule hizi zote za amali, ili ziweze kutoa mafunzo yale yanayohitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Getere kwamba, mpango huu ni endelevu. Tunakamilisha awamu ya kwanza, tutakwenda awamu ya pili, ili kukamilisha miundombinu ya shule za sekondari za amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, tunayo mipango mbalimbali ya kuhakikisha shule zetu zote za sekondari za kata zinakamilishwa miundombinu yake kwa awamu. Tumeshajenga shule ambayo Mheshimiwa Mbunge ameitaja na tayari inatoa huduma na tunafahamu kwamba, kuna upungufu wa baadhi ya miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali ipo kwenye taratibu za kupata fedha ili kupeleka Bunda kwa ajili ya kukamilisha shule hiyo ili wanafunzi waweze kupata fursa nzuri ya kujifunza. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tinnar Chenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko, na baadaye Mheshimiwa Edwin Swalle. Ninaomba maswali mafupi ya Kibunge, kwa mujibu wa kanuni na Waziri, majibu yawe mafupi.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Chenge Sekondari iliyopo Kata ya Somanda pale Bariadi ilijengwa kwa nguvu za wananchi tangu mwaka 2016, na kuna maabara ambayo ni *two in one,* lakini tangu kipindi hicho shule hiyo na maabara hiyo bado haijakamilika. Je, ni lini Serikali itakwenda kukamilisha maabara hiyo ili kuunga mkono juhudi za wananchi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwanza Serikali inatambua mchango mzuri wa wananchi wa Jimbo la Bariadi na Bariadi Mjini kwa kuchangia nguvu zao kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Secondari ya Chenge. Nakuhakikishia kwamba,

Serikali ilishafanya tathmini, na tunayo orodha ya shule zote ambazo zimejengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zote ambazo zimejengwa kwa fedha ya Serikali, kwa maana ya Halmashauri, yaani Serikali Kuu, tayari tunafahamu upungufu wa majengo na miundombinu inayohitajika. Tunaendelea na taratibu za fedha, ili tuweze kupeleka kukamilisha shule hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Shule ya Sekondari ya Chenge itapewa kipaumbele. Itapelekewa fedha ili tuhakikishe miundombinu hiyo inakamilishwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Shule ya Amali ya Nyandoto iliyopo Halmashauri ya Mji wa Tarime imeshakamilika miundombinu ya madarasa, ofisi, vyoo na nyumba ya Mwalimu, lakini shule hii ilijengwa nje ya mji, hivyo tunahitaji tupate fedha kwa ujenzi wa bweni na karakana, ili shule ianze. Sasa ni lini Serikali itapeleka fedha hizi kwa haraka?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kwamba, shule hii imejengwa awamu ya kwanza na tunafahamu kwamba katika mpango wa ujenzi wa shule zote 103 za amali mabweni, karakana na mitambo yote ya kihandisi ni sehemu ya ujenzi wa shule zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejenga awamu ya kwanza, zimeanza kutoa huduma kama shule za kutwa; awamu ya pili inakwenda kujenga mabweni, karakana pamoja na miundombinu yote ya uhandisi ili kuhakikisha shule hizo zinatoa huduma inayotakiwa. Kwa hiyo, tupo kwenye hatua za mwisho za kupata fedha kwa ajili ya kwenda kujenga miundombinu hiyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edwin Swalle. Ajiandae Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kata ya Kidegembye, hasa pale kwenye Kijiji cha Image, ambako Mheshimiwa Naibu Waziri anapafahamu, wananchi wamejengewa shule nzuri sana ya amali, lakini ipo mbali na makazi ya wananchi, kwa hivyo, hakuna nyumba za waalimu wala karakana kwa ajili ya wale wanafunzi, na hakuna bweni. Ni lini Serikali itapeleka fedha, kwa ajili ya bweni, karakana na nyumba za waalimu pale Image?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa shule hizi tulianza na awamu ya kwanza ya shilingi milioni 584 na tulijenga miundombinu ya madarasa na shule zile zimeanza kutoa huduma, kwa maana ya shule za kutwa. Awamu ya pili, tunakwenda kutenga shilingi bilioni 1,600, kwa ajili ya kujenga miundombinu inayosalia, yakiwemo mabweni, karakana na kununua vifaa vya kihandisi, ili wanafunzi wanaojifunza masuala ya kiuhandisi waweze kuwa na mazingira bora ya kujifunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Swalle, Mbunge wa Jimbo la Lupembe, unayefanya kazi kubwa sana kwa ajili ya wananchi wa Jimbo la Lupembe, kwamba, Serikali hii sikivu ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan inatambua hilo, na tupo kwenye taratibu za kupata fedha kwa ajili ya kukamilisha shule hizo zote 103, ili ziweze kutimiza lengo lililokusudiwa, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, ajiandae. Mheshimiwa Yahya Mhata.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Serikali ilitoa mwongozo kwamba, inapeleka shule za amali katika majimbo ambayo hayakupatiwa Vyuo vya *VETA*. Je, ni

lini Serikali itapeleka shule ya amali katika jimbo la Bumbuli, Wilaya ya Lushoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, Serikali iliweka kipaumbele kupeleka shule za mafunzo ya amali za sekondari katika majimbo au wilaya ambazo hazina vyuo vya *VETA*. Zoezi hilo limeendelea kufanyika na ndiyo maana tayari shule 103 zimejengwa, zipo hatua mbalimbali za ukamilishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, bado Serikali inaendelea kufanya tathmini kwenye maeneo yale yote ambayo yana uhitaji wa shule hizo na hayana vyuo vya *VETA,* tutahakikisha tunaweka mipango kwa awamu ili kufanikisha dhamira ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo, Mheshimiwa Mbunge, tutakwenda kufanya tathmini na kuona uwezekano wa kufanya jambo hilo ambalo Mheshimiwa Mbunge amesema.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yahya Mhata. Tutamalizia na Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles kwa swali hili.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya jimbo langu ipo shule ya wasichana wenye vipaji maalum. Shule ile pamoja na jitihada kubwa za Serikali za kuleta shilingi bilioni nne kwa ajili ya shule, lakini haina uzio, hivyo kusababisha wasichana wale na wenye changamoto, yaani wenye ulemavu, kuwa katika hatari ya usalama wao. Ni lini Serikali italeta fedha ili kujenga uzio katika ile shule, ili wasichana wetu, watoto wetu waishi katika mazingira salama zaidi? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli, Serikali hii ya Awamu ya Sita, na kwa dhamira njema sana ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka mpango mkakati wa kujenga shule maalum za wasichana kidato cha kwanza hadi cha sita katika mikoa yote 26, kote nchini. Tayari shule hizo zimesajiliwa na zimeanza kutoa huduma. Ujenzi wa shule zile uligharimu takribani shilingi bilioni nne nukta sita na tunafahamu kwamba, bado kuna miundombinu inayohitajika ukamilishaji wake zikiwemo *fence* za shule zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mhata, Mbunge wa Nanyumbu kwamba, Serikali inatambua uhitaji wa *fence* hizo. Ninatumia nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kuwasisitiza na kuwakumbusha Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini kwamba, pia, katika mapato ya ndani wanayo fursa ya kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya kuanza ujenzi wa *fence* hizo wakati Serikali Kuu ikiendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kukamilisha *fence* hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Bwilegi ni miongoni mwa kata ambazo vijiji vyake vipo mbalimbali sana katika Wilaya ya Butiama, lakini Kijiji cha Lyamsanga sasa hivi kwa muda wa miaka miwili, wananchi wameshakusanya mawe na mchanga *trip* 50 na kokoto *trip* 16. Je, lini Serikali itapeleka fedha ili wananchi wa Kijiji cha Lyamsanga waweze kupata shule ya sekondari? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Butiama na ninawapongeza sana wananchi kwa kutoa nguvu zao kukusanya mawe na mchanga, kwa ajili ya ujenzi wa shule

hiyo ya sekondari. Ninaomba kutumia fursa hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, kumwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Butiama, walete taarifa rasmi ya maandalizi kwanza, kama eneo linakidhi vigezo vya kuwa na shule hiyo ya sekondari. Pili, walete taarifa ya maandalizi kupitia mapato ya ndani na Serikali Kuu iweze kuona namna bora zaidi ya kuunga mkono nguvu za wananchi katika ujenzi wa shule hiyo ya sekondari.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Ninakushukuru kwa majibu haya ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Mheshimiwa Asha Salum Motto, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Kukaribisha Wawekezaji Kuwekeza Mtwara**

**MHE. ASHA S. MOTTO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukaribisha wawekezaji wa viwanda vya mbolea na saruji, Mtwara, kutokana na uwepo wa makaa ya mawe?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Salum Motto, Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mtwara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uwepo wa makaa ya mawe na rasilimali ya gesi asilia katika Mikoa ya Kusini, ukiwemo Mkoa wa Mtwara, kampuni kadhaa za uwekezaji zimevutiwa kuwekeza katika mikoa hiyo. Miongoni mwa kampuni kubwa za uwekezaji za nje

zilizowekeza Mtwara baada ya kuvutiwa na mazingira hayo ni pamoja na Kampuni ya *Dangote Cement* kutoka Nchini Nigeria, ambayo imewekeza katika kiwanda cha saruji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kampuni ya Indorama ya Nigeria na *Soil Solution* ya India zimeonesha nia ya kuwekeza katika viwanda vya mbolea, ambapo Kampuni ya *Soil Solution* imeanza ujenzi wa kiwanda cha mbolea ndani ya eneo lililopo Mtwara Mjini. Ofisi inaendelea kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya mbolea na saruji kupitia mikutano na makongamano ya wawekezaji yanayofanyika ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Salum Motto.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali kwa majibu mazuri ya kutia moyo wananchi wa Mkoa wa Mtwara. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, tayari kuna mwekezaji huyu *Soil Solution*, ambaye kimsingi kwa taarifa za awali mwekezaji huyu tayari ameshalipa fidia wananchi wa Mgau, kwa maana ya Halmashauri ya Mtwara *DC*, ekari 151 za ardhi kwa shilingi 1,832,000,000; kwa taarifa rasmi, kiwanda hiki kikikamilika kinatarajia kuajiri wafanyakazi 3,000, lakini pia, kinatarajia kugharimu uwekezaji wa Dola za Kimarekani 627,000,000. ni nini Kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda hiki mpaka sasa hakijaanza kufanya kazi. Wananchi wa Mkoa wa Mtwara, kwa maana ya Mtwara *DC*, walikuwa na matumaini makubwa sana baada ya kuona kuwa wamelipwa fidia, wakijua kabisa utekelezaji unaenda kuanza kufanya kazi kwa muda siyo mrefu na mwekezaji huyu yupo nchini hapa Tanzania mwaka mmoja sasa…

**MWENYEKITI:** Umeeleweka Mheshimiwa Asha. Uliza swali la pili, kama unalo.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa, Mikoa ya Kusini ina rasilimali ya gesi na makaa ya mawe, na tayari tumeona kuna wawekezaji wamewekeza katika rasilimali hii ya gesi; ni nini Kauli ya Serikali juu ya uwekezaji wa makaa ya mawe? Maana tuna bandari tayari inayosafirisha makaa ya mawe, pia Mkoa wa Mtwara tuna njia kuu ya kupitisha hayo makaa ya mawe. Ninaomba kujua Serikali ina mkakati gani kukaribisha wawekezaji wanaotumia makaa ya mawe? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa maswali hayo mawili.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Asha Salum Motto, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Mtwara, kwa jinsi anavyowatetea wananchi. Mheshimiwa Asha amenisumbua sana kuhusu huyu mwekezaji ambaye anaitwa *Soil Solution,* ambaye kimsingi ni kweli ameshanunua zaidi ya ekari 150 na amelipa fidia zaidi ya shilingi bilioni 1.4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu pamoja na Wizara ya Nishati tumekuwa tukifanya majadiliano kuona ni jinsi gani tunaweza tukamsaidia mwekezaji huyu ili aanze ujenzi wa kile kiwanda chake? Majadiliano yanaenda vizuri. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi kama Serikali, tunafanyia kazi na tupo hatua nzuri ya kuhakikisha mahitaji yote ya mwekezaji yanafanyiwa kazi na tunaona tija ya uwekezaji huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwekezaji huyu anakuja kutengeneza ajira zaidi ya 3,000, na anakuja kuwekeza zaidi ya Dola za Kimarekani zaidi ya milioni 627 Mkoani Mtwara. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi kama Serikali, tupo. *On top of that* tutahakikisha tunamsaidia na tunawasaidia wawekezaji wote wanaokuja nchini, ili wawe na mazingira rafiki, kwa ajili ya uwekezaji wao kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ni kweli, sisi kama Serikali na Tanzania, tuna makaa ya mawe ya kutosha na Mtwara ni lango la

kupitisha makaa ya mawe. Tunapofanya uhamasishaji wa wawekezaji, mojawapo ya eneo ambalo tunalihamasisha ni jinsi gani wawekezaji wanaweza kuja Mkoa wa Mtwara kwa ajili ya kuwekeza wakitumia nishati ya makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mbunge kwamba, tutachukua suala la Mkoa wa Mtwara kama kipaumbele tunapozunguka huko duniani na hapa Tanzania kuwahamasisha wawekezaji waje kuwekeza Mtwara. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, ajiandae Mheshimiwa Arif Premji.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Guta, kwenye Jimbo la Bunda Mjini, kuna eneo la Tairo ambalo limetengwa kwa ajili ya uwekezaji na wananchi wameshalipwa fidia. Eneo hili limekaa wazi zaidi ya miaka 14. Naibu Waziri ameenda kulitembelea eneo lile, eneo ambalo ni *very potential,* liko karibia na Ziwa na lipo kwenye lami. Je, ni lini sasa wataletwa wawekezaji, wajenge viwanda ili akina mama wa Bunda na Vijana wa Bunda waweze kupata ajira? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Bulaya, amekuwa akinisumbua sana kuhusu ile *Bunda SEZ,* ambayo kimsingi ni mojawapo ya vipaumbele vya Serikali. Kama tunavyotambua, Rais amesisitiza kwamba tunaenda kuanzisha kongani za viwanda, lakini mojawapo ya mkakati wetu sasa hivi tunaenda ku-*promote* uwekezaji kwenye maeneo ya *SEZ*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunda ni mojawapo ya meneo ambayo kimsingi ni mkakati wa Serikali na katika bajeti yetu ya mwaka huu imo, na tunaenda kutenga eneo kwa ajili ya uwekezaji wa vijana.

Ninaomba nimhakikishe Mbunge kwamba suala la Bunda *SEZ* tumelipa kipaumbele. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Arif Premji, ajiandae Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji wa *Soil Solution* ni wa kimkakati, unaenda kusaidia Taifa hili kupunguza gharama ya Dola za Kimarekani milioni 400 kwa kuagiza mbolea. Majibu ambayo yametolewa ni mepesi mno, uhitaji wa *Soil Solution* ni gesi na gesi inatoka Mtwara, hadi sasa hivi ni mwaka mzima anazungushwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipi kauli rasmi ya Serikali kuhusiana na mradi huo wa kimkakati ambao unaenda kusaidia Taifa letu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mbunge kutoka Mtwara, Ndugu yangu, Mheshimiwa Arif, amekuwa akiniuliza sana swali hili, amekuwa akifuatilia sana kuhusu huyu mwekezaji ambaye kimsingi anatoka Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba *Soil Solution Limited* ni mojawapo ya uwekezaji wa kimkakati, kulingana na vigezo vyetu, mwekezaji yeyote wa nje anapokuja kuwekeza akiwa na zaidi ya milioni 50 *USD* ni mwekezaji wa kimkakati, huyo wa kwetu ana zaidi ya milioni 150, anazo milioni 627 za Kimarekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kujibu kwenye swali la nyongeza la Mheshimiwa Asha Motto, naomba niseme kwamba Serikali ipo *on top of that,* na tumekuwa na majadiliano na wenzetu wa Wizara ya Nishati. Ninamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Ndejembi, amekutana mara nyingi sana na huyu mwekezaji na wamemhakikishia kwamba baada ya mipango ya

upatikanaji wa gesi itakapokuwa vizuri, tunamhakikishia ujenzi wa kiwanda utaanza. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume.

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Morogoro Vijijini kwa sasa ndiyo mzalishaji mkubwa wa karafuu. Wawekezaji kutoka *Indonesia* walionesha nia ya kutaka kuwekeza katika eneo letu. Je, Wizara ina mpango gani sasa wa kuendelea kuvutia wawekezaji ili wakaweke viwanda vya kusindika karafuu kule Morogoro *DC*? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mbunge kwa swali lake zuri la kutetea watu wa Morogoro, hususan kwenye suala la kilimo cha karafuu na haja ya kupeleka viwanda na wawekezaji Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, kipaumebele chetu ni kuvutia wawekezaji. Rais ameshatuagiza, lakini ninyi wenyewe ni mashahidi Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amekuwa kipaumbele katika kuvutia wawekezaji anapozunguka huko duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue suala la Morogoro kama kipaumbele, nasi tutaliweka kwenye mpango wetu wa kuhamasisha na kuvutia wawekezaji waje kuwekeza Morogoro. Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Morris Makoi.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Ninaomba niulize kwamba hapa Dodoma kuna

kiwanda cha mbolea, na hivi karibuni na hapa ninapoongea katika Jimbo la Moshi Vijijini wananchi wanataabika sana kutafuta mbolea ya ruzuku na mbolea mpaka sasa haipatikani kwa ajili ya palizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali inatuambiaje kuhusiana na uzalishaji wa kiwanda cha mbolea hapa Dodoma na kama mbolea ile inaweza ikapelekwa katika Mikoa hususan Kilimanjaro na Jimbo la Moshi Vijijini ili kusaidia kupunguza taabu ya mbolea katika Jimbo lile wakati huu wa palizi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mbunge kutoka Moshi Vijijini kwa swali lake zuri la kuwatetea Wananchi wa Moshi ambao ni wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana kwamba tunacho kiwanda kikubwa cha *ITRACOM* cha hapa Dodoma ambacho kipo maeneo ya Nala. Ni mwekezaji mkubwa wa kimkakati ambaye kimsingi amesaidia sana kupunguza tatizo la mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba bado tuna changamoto katika suala la mbolea na ndiyo maana Serikali tumeweka mkazo kuvutia wawekezaji wa viwanda vya mbolea. Kwa hiyo, ninaomba Mbunge akubaliane nasi kwamba, wakati Serikali inajipanga kuvutia wawekezaji, tutaendelea kutumia viwanda vilivyopo kuhakikisha wakulima wanapata mbolea kwa ajili ya kilimo. Ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge, kutoka Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji.

Tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, aulize swali lake.

Na. 63

**Wafugaji Kupata Soko na Bei ya Uhakika ya Maziwa – Korogwe Vijijini**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwasaidia wafugaji wa Korogwe Vijijini na Mkoa wa Tanga kwa ujumla kupata soko na bei ya uhakika ya maziwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi. Ninaomba sasa nijibu swali la Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini, kama Ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mifugo na Uvuvi kupitia Taasisi ya Bodi ya Maziwa, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga na Chama cha Ushirika cha Wazalishaji Maziwa Mkoa wa Tanga *(TDCU)*, wanaendelea na utatuzi wa changamoto za kiwanda cha kusindika maziwa cha Tanga almaarufu kama *Tanga Fresh* ambacho kina uwezo wa kusindika maziwa lita 120,000 kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kiwanda hicho ndicho soko kubwa la maziwa yote ya Mkoa wa Tanga na Mikoa ya jirani. Changamoto za kiwanda hicho ni pamoja na upungufu wa mtaji na gharama kubwa za uendeshaji na hivyo kushindwa kununua maziwa ya wafugaji kwa bei ya uhakika. Kutatuliwa kwa changamoto hizo kutasaidia wafugaji wa Korogwe vijijini na Mkoa wa Tanga kwa ujumla kupata soko na bei ya uhakika ya maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara ya Mifugo na Uvuvi inatekeleza mradi wa miaka kumi wa mageuzi ya tasnia ya maziwa na

mabadiliko ya tabianchi katika Mikoa 13 nchini, Mikoa nane Tanzania Bara na Mikoa mitano Zanzibar ikiwemo Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo utaboresha mnyororo wa thamani wa maziwa ikiwemo vituo vya kukusanyia maziwa kutoka kwa wafugaji kabla ya kupeleka kiwandani. Hatua hizi, zitasaidia wafugaji wa Korogwe Vijijini na Mkoa wa Tanga kwa ujumla kupata soko na bei ya uhakika ya maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza; kwa sasa hivi hali ya wafugaji ya Mkoa wa Tanga ni mbaya. Kiwanda mnachosema kinao uwezo wa kusindika lita 120,000 kwa siku. Kwa uhalisia kwa sasa, kinasindika lita zisizozidi 20,000. Kiwanda hiki kinakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwemo madeni makubwa, pia changamoto za kiuendeshaji. Kwa hali ilivyo, hatuoni matumaini ya hivi karibuni kutatua changamoto ya kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari kutafuta mpango mwingine wa kuvutia wawekezaji wengine tujenge kiwanda kingine cha maziwa kwa ajili ya kusaidia wafugaji wa Mkoa wa Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; tunaipongeza Serikali kwa mradi huu mzuri wa mageuzi ya tasnia ya maziwa, lakini kiuhalisia, mradi huu sisi Korogwe Vijijini haufiki ambako uhitaji ni mkubwa sana ikiwemo uhitaji wa maeneo ya kuhifadhia maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari wakati wa mapitio ya mradi huu, tuongeze na Wilaya ya Korogwe Vijijini iwe mnufaika wa mradi huu ili wafugaji wa Korogwe Vijijini waendelee kupata uhakika wa kuhifadhi maziwa yao na kupata bei ya kueleweka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Timotheo Mnzava kwa sababu amekuwa akifuatilia mgogoro huu kwa karibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tulikaa kikao pamoja na Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga. Nitumie fursa hii kuwashukuru sana na kuwapongeza kwa kufuatilia maslahi mapana ya wafugaji wa Mkoa wa Tanga. Mwenyekiti wa kikao hiki alikuwa ni Mheshimiwa Timotheo Mnzava, ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mbunge kwamba, moja ya vipaumbele vikubwa sana katika Wizara yetu kwa sasa ni pamoja na utatuzi wa changamoto zilizopo katika kiwanda hiki. Tunatambua ni kwa kiasi gani uimara wa kiwanda hiki ulikuwa unachangia katika kuongeza soko la maziwa na bei nzuri kwa wafugaji wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tumeshaanza kuchukua hatua. Tayari Waziri wa Mifugo na Uvuvi amekaa kikao na uongozi wa *TADB* ambao ni mdeni namba moja wa kiwanda hiki. Pia, tumeshakaa vikao na wadeni wengine, tumekaa kikao katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi alikwenda Tanga mahsusi kabisa katika kikao na wadau wote wanaohusika na changamoto katika kiwanda hiki ili kuona namna gani tunakwenda kuzitatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Wabunge wote wa Mkoa wa Tanga, wananchi wote wa Mkoa wa Tanga na wale wote wa Mikoa jirani ambao walikuwa wananufaika na kiwanda hiki, kwamba moja ya vipaumbele vyetu kwa sasa ni utatuzi wa changamoto katika kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wakati huu, wakati tunaendelea na utatuzi wa changamoto za kiwanda hiki, tunaendelea na kuvutia pia wawekezaji binafsi ili waweze kutambua fursa zilizopo katika Mkoa

wetu wa Tanga, ikiwemo wingi wa malighafi hii ya maziwa ili tuweze kuanzisha viwanda vingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, mradi huo ambao tunakwenda kuanzisha wa Mikoa Nane ambayo iko Kanda ya Ziwa na mitano Zanzibar, ni kweli, katika Mkoa wetu wa Tanga tunazo Wilaya tatu, Wilaya ya Lushoto, Muheza na Wilaya ya Mkinga na Wilaya ya Korogwe Vijijini ambazo kwa sasa katika mradi huu hazipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mbunge kwamba Serikali tunaendelea na juhudi mbalimbali za kupata fedha kwa ajili ya kuanzisha hizi *milk collection centres* katika sehemu mbalimbali ambazo hatuna, ili kupunguza upotevu wa maziwa. Pia tunaendelea kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ili tuweze kupata fedha za miradi mbalimbali na kule ambako hatuna hizi *milk collection centres* tuziweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi nimpe tu uhakika kwamba Wilaya yetu ya Korogwe Vijijini itakuwa kipaumbele. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, ajiandae Mheshimiwa Ramadhani.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nina swali kwa Waziri. Wananchi wa Jimbo la Ludewa wanapenda sana kufuga samaki Ziwa Nyasa ila kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa vifaranga vya samaki ambavyo vinaendana na ekolojia ya Ziwa Nyasa. Je, Serikali iko tayari kuwezesha Kituo cha *TAFIRI*, Mbeya na Ruhila, Songea ili waongeze uzalishaji wa vifaranga vya samaki na kuhakikisha upatikanaji wa chakula cha samaki kirahisi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kati ya maziwa yetu makuu ambayo tunayo hapa nchini, na sisi kama Wizara tunayaangalia kama maziwa ya mkakati, ni pamoja na Ziwa Nyasa. Tunaendelea kufanya mikakati mbalimbali ya kuhakikisha

kwamba vituo vyetu ambavyo vinazalisha vifaranga ambavyo ndiyo vina-*supply* kwa wote wanaofuga kwenye Ziwa Nyasa vinaongezewa uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe tu hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kati ya fedha ambazo tumepokea sasa hivi Wizarani kwa ajili ya kuwezesha vijana kwenye uvuvi na mifugo, baadhi ya fedha hizo pia zitakwenda kuwawezesha vijana katika Ziwa Nyasa. Kwa hiyo, tunao mpango na mkakati wa kuhakikisha wale wote wanaowekeza katika Ziwa Nyasa wanapata chakula na vifaranga kwa wakati na kwa uhakika. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ramandani, ajiandae Mheshimiwa Joshua Nassari.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika mipango mizuri ni kuweka mipango ya muda mfupi ya kati na ya muda mrefu. Sasa kwa kuwa wananchi wa Tanga wameshahamasika sana na zao hili la maziwa, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi wa kuhakikisha kwamba wananusuru mapato haya yanayopotea katika zao la maziwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana. Nami ninampongeza sana Mbunge mwingine wa Mkoa wa Tanga ambao kwa kweli kwa kiasi kikubwa wanafuatilia mgogoro huu kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyozungumza katika swali la msingi, mgogoro huu ni kipaumbele chetu kwa sasa. Tunaendelea kutafuta *solution* za muda mrefu, lakini hata za muda mfupi ikiwa ni pamoja na kuona namna gani tunaweza kutenga fedha kadri zinavyopatikana kuongeza juhudi ya kuhakikisha tunazuia upotevu wa malighafi hii ya maziwa kwa wafugaji wetu wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tunaendelea kulifanyia kazi kwa karibu sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joshua Nassari, ajiandae Mheshimiwa Yannick Ndoinyo.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona. Swali la msingi limeulizia habari ya soko na bei ya maziwa kwa wafugaji. Sasa Katika kukabiliana na tatizo hilo la soko na bei, wakulima na wafugaji wa Meru wameanzisha umoja wao unaitwa UWAWAME (Umoja wa Wakulima na Wafugaji Meru). Wanachohitaji kwa Serikali ili waweze kusaidika ni kuongeza thamani kwenye mazao ya maziwa na vitu vingine. Kuna baadhi ya vitu ambavyo wanahitaji msaada kutoka kwa Serikali kwa maana ya Wizara inayohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali iko tayari basi kukutana na hawa *UWAWAME* ili waweze kuwasaidia waweze kukabiliana na hii changamoto ya bei na soko kwenye maziwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Ninamshukuru pia Mbunge kwa sababu mara kwa mara amekuwa akiniuliza juu ya namna gani tunaweza tukawafanya *UWAWAME* waweze kuendelea kuzalisha kwa tija zaidi hasa wafugaji katika umoja juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge katika muda na saa ambao tutapanga kwa pamoja na Wizara tupo tayari kukutana na *UWAWAME* ili twende tukaone namna gani ya kuwaongezea tija katika uzalishaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Yannick Ndoinyo, ajiandae Mheshimiwa Charles Sungura.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Langu ni ombi na ushauri kwa Wizara kufanya utafiti wa uzalishaji wa zao la maziwa katika Wilaya yangu ya Ngorongoro ili kuwashauri

na kuwasaidia wazalishaji wa maziwa wapate soko la uhakika na kuongeza kipato chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ushauri na ombi kwa Wizara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru sana, ninamshukuru sana Mbunge wa Ngorongoro, ushauri wake ni mzuri na tumeupokea kwa ajili ya kuufanyia kazi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Charles Sungura.

**MHE. DKT. CHARLES J. SUNGURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nipate majibu kwa Naibu Waziri kwamba, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa kituo cha kukusanyia maziwa kilichopo katika Kijiji cha Msomela, Kata ya Misima?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru sana. Kadri ya upatikanaji wa fedha ndivyo ambavyo Serikali itaendelea na ujenzi wa kituo hiki cha ukusanyaji wa maziwa kilichopo Msomela. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Mvomero, aulize swali lake.

Na. 64

**Ujenzi wa Barabara ya Kutoka Kipera – Kisaki kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. SARA M. ALLY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga barabara ya kutoka Kipera – Mlali – Nyandila – Luale – Kikeo hadi Kisaki kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Sara Msafiri Ally, Mbunge wa Mvomero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kipera – Mlali – Nyandila – Luale – Kikeo – Kisaki inajumuisha barabara ya Mkoa ambayo inaanzia Sangasanga – Langali – Luale – Kikeo yenye urefu wa kilometa 59.16 inahudumiwa na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha barabara hiyo inapitika majira yote ya mwaka na kutoa huduma ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi, Serikali imeendelea kufanya matengenezo mbalimbali hususan sehemu korofi kwa kuijenga kwa kiwango cha lami na zege ambapo jumla ya kilometa 13.19 zimejengwa na kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali pamoja na hatua hizo, inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hiyo ili kuijenga kwa kiwango cha lami. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sara Msafiri Ally.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi, na ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri na kwa mipango mizuri ya kuboresha barabara zetu hasa zilizopo chini ya *TANROADS*. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, barabara hii ni barabara ya kimkakati ya kiuchumi ambapo kuna shughuli za kiuchumi za uchimbaji wa madini, madini ambayo yanategemewa sana kwenye viwanda vya *tiles*, Jiji la Dar es Salaam na Mkoa wa Pwani na Kituo cha Afya kikubwa kinachotegemewa na Tarafa mbili ya Mlali na Mgeta, lakini kuna soko kubwa la kisasa pale, barabara hii imekuwa ikikwamisha shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali haioni ipo haja sasa ya kutenga fedha kwa ajili ya kufanya *feasibility study* ili barabara hii ya kilometa 59 ijengwe kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa barabara hii imeenda mpaka ikaunganika na Kituo cha Kisaki cha Treni ya *TAZARA* na wananchi wa Tarafa ya Mgeta na Mlali ni wazalishaji wakubwa kama nilivyoongea kwenye swali la kwanza: Je, Serikali haioni kuchelewesha kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami ni kuwachelewesha wananchi kuboresha shughuli za kiuchumi na kujiongezea kipato? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakubali kwamba barabara hii ni ya muhimu sana. Kama alivyosema, kwamba kuna shughuli nyingi za kiuchumi ikiwemo madini, kituo cha afya, lakini pia kuna soko. Ndiyo maana tumesema kwamba tunahakikisha inapitika muda wote, na yale maeneo ambayo yamekuwa yanakwamisha, tunayaboresha kwa kuyajengea lami ama zege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika jibu langu la msingi, tumekiri kwamba tunatafuta fedha ili tuweze kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ikiwa ni maandalizi ya kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, kuhusu kuunganisha na Kisaki, ninakiri kwamba hii barabara ndiyo inayounganisha hawa wananchi mpaka kituo cha *TAZARA* cha Kisaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna vipande viwili. Sisi Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* tunaishia pale Kikeo na kutoka Kikeo kwenda Kisaki inahudumiwa na wenzetu wa *TARURA*. Kwa hiyo, tutawasiliana na wenzetu ili tuweze kuhakikisha kwamba, wakati hatujaijenga kwa kiwango cha lami, lakini barabara yote iweze kupitika kuanzia hapa ambapo inaanzia, Sangasasanga – Kikeo hadi Kisaki, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Edifonsi Kanoni, wajiandae Mheshimiwa Esther Midimu na Mheshimiwa Olelekaita.

**MHE. EDIFONSI J. KANONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pia ninashukuru kwa kupata mradi wa barabara kutoka Matai – Kashesha ambayo ni ya kilometa 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ikikamilika, itachochea uchumi sana katika Wilaya ya Kalambo, na Serikali itakusanya mapato katika Kituo cha Forodha Kashesha. Wananchi wa Kalambo wanataka kupata majibu ya Serikali, je, ni lini barabara hii ambayo inaendelea kusuasua, itakamilika ili waweze kufaidika? Watapata ajira, tutachochea Uchumi, na pia tutapata wawekezaji kwa sababu ipo mpakani mwa Zambia na Tanzania.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri kwamba hii barabara ni muhimu sana na hasa kwa kipindi hiki kwa sababu ni moja ya barabara kuu, na pia tuna kituo chetu cha forodha kule. Tunavyoongea barabara hiyo kutoka Matai – Kasese ina kilometa 50. Mheshimiwa Mbunge atakubalina, kwamba, ili kufanya haraka tumeigawa katika vipande viwili, kwa maana ya *lots*; Matai – Tatanda, Tatanda – Kasesya na tuna Wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tumechelewa kwa sababu mkandarasi alikuwa anadai. Tumeshamlipa na mkandarasi wa kipande cha pili tunafanya maandalizi ya kumlipa ili barabara hii iweze kukamilika, kwa sababu sasa magari mengi yanayotokea

Zambia yanapita huko kwenda mikoa ya Kaskazini na hata kwenda nchi jirani. Kwa hiyo, tunalitambua hilo na tunalipa umuhimu mkubwa sana kuhakikisha kwamba hiyo barabara yote inajengwa kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Midimu.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Bariadi – Itilima – Meatu – Sibiti hadi Singida iko kwenye Ilani, je, ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami barabara hii muhimu kwa vile ndiyo itakuwa *shortcut*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli barabara hii iko kwenye kiwango cha lami, ilikuwa haijakamilishwa usanifu. Tunachokamilisha sasa hivi ni usanifu wa kina wa barabara hii ambayo ni muhimu sana kwa wenzetu wa Mkoa wa Simiyu. Baada ya hapo, tutatafuta fedha kwa ajili ya kuanza kuijenga kwa kiwango cha lami, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Olelekaita, Mheshimiwa Devota Minja ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kibaya – Kisima kilometa 50 walisema wataijenga kwa kiwango cha lami. Kipindi hiki cha mvua wananchi wa Kiteto wamesumbuka sana. Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami? Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, barabara hii ambayo ni ya kipande cha kutoka Handeni – Kibirashi – Kibaya kwenda kwa Mtoro kilometa 50 Kibaya – Kisima, tunachosubiri tu sasa hivi ni kumpa mkandarasi malipo ya awali ili aweze kukijenga kipande hicho cha kilometa 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi yupo tayari, tumeshapeleka maombi yetu Hazina ili aweze kulipwa malipo ya awali aanze kazi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Devota Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kuniona. Manispaa ya Morogoro ni Manispaa ambayo barabara zake nyingi ni za vumbi, hazijaunganishwa kwa lami. Kwa mfano, Kata ya Mkundi, Bigwa, Kihonda, Tungi hazina lami. Serikali kupitia *TARURA* ina mpango gani wa kuunganisha barabara hizi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nilipokee swali la Mheshimiwa Mbunge wa Morogoro, lakini niseme tutawasiliana na wenzetu wa *TARURA* kwa sababu barabara nyingi za mijini zinasimamiwa na wenzetu wa TAMISEMI kupitia *TARURA*. Hata hivyo, kama Serikali, tumelichukua na tutampa majibu sahihi.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Kilolo.

Na. 65

**Ukamilishwaji wa Barabara ya Kilolo – Udekwa – Ilula**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza: -

Je, lini Barabara ya Kilolo – Udekwa – Ilula itakamilika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, Mbunge wa Kilolo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya Kilolo – Udekwa – Ilula ni barabara ya mkoa inayojulikana kwa jina la Kilolo – Ipalamwa – Watalisoli – Ilula yenye urefu wa kilometa 91. Kwa sasa, Serikali ipo katika hatua za mwisho za manunuzi ya kumpata mhandisi mshauri wa kufanya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Baada ya usanifu kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha kwa ajili ya ujenzi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Enespher Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali madogo mawili. Ninaomba niipongeze Serikali kwa majibu mazuri, lakini pia nipongeze kwa ujenzi wa kiwango cha barabara ya kutoka Ipogolo – Idete. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Kilolo na barabara hii inaunganisha kata nyingi ikiwepo Makao Makuu ya Kilolo, Kata za Mtitu, Kising'a, Upwega, Udekwa, na Ilula. Barabara hii inaunganisha kata zilizopo eneo la chini na eneo la juu katika Jimbo letu la Kilolo na ina Daraja la Lukosi. Daraja hili limeanza kujengwa tangu tarehe 15 Februari, 2023. Tulitegemea suluhisho la daraja hili lingeweza kusaidia, kwa sababu sasa hivi kuna vidaraja vidogo ambavyo havipitiki, ule mto ukiwa umejaa maji: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini daraja hili litakamilika ili wananchi wa Kilolo wasiendelee kupata mateso makubwa ambayo wanayapata wakati wa mvua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa barabara inayotoka Kibaoni inapita Ukumbi – Kitoo hadi Ihemi, Iringa *DC,* ni barabara ya kiuchumi mkubwa na inapitisha magari makubwa sana ya mbao; sasa kutokana na ubovu wa barabara hii magari yamekuwa yakikwepa njia ya kupita katika barabara hii na kwenda kupita kwenye halmashauri nyingine na kusababisha upotevu wa mapato makubwa katika Wilaya yetu ya Kilolo, je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kuboresha hii barabara ili Kilolo iweze kupata mapato yao yote bila kwenda kupitisha kwenye halmashauri nyingine?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Dkt. Ritta, Mbunge wa Kilolo kwa kuipongeza Serikali kwa kukamilisha kujenga barabara kutoka Ipogolo – Kilolo yenye urefu wa kilometa 33 kwa kiwango cha lami, tunamshukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, na hasa kuhusu daraja ambalo lipo katika barabara aliyoiuliza, ni kweli daraja hili ni muhimu sana kulijenga. Tayari tuna mkandarasi yupo *site,* lakini amechukua muda mrefu. Mkataba wake unamtaka kabla ya mwisho wa huu mwaka awe amekamilisha kulijenga daraja hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tutahakikisha kwamba tunamlipa fedha hiyo, kwa sasa yupo *site* anafanya kazi, daraja lenye gharama ya kama shilingi bilioni 2.8 ili aweze kukamilisha na kuondoa adha ambayo inawakabili wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Barabara ya Kibaoni – Itoho – Ihemi, tumepokea. Ninapenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kupitia Bunge lako nimwagize Meneja wa Mkoa wa Iringa ahakikishe kwamba barabara hii inapitika muda wote ili wananchi wasiweze kupata adha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli barabara hizi ambazo ni changarawe kipindi cha mvua, na hasa eneo lake lina mvua nyingi sana, zinakuwa na changamoto. Hivyo, meneja ahakikishe kwamba hii barabara inapitika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar, Mheshimiwa Zacharia Paulo, ajiandae.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaomba kuuliza swali. Je, ni lini barabara inayounganisha barabara tatu, kwa maana ya Tabora Mjini – Ulyankulu na Jimbo la Uyui, itajengwa kwa kiwango cha lami ambapo wananchi wengi wanahitaji lami ili waweze kunufaika na huduma hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sijamsikia, amesema Tabora Mjini hadi...

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara inayoounganisha wilaya tatu za Tabora Mjini, Ulyankulu na Uyui ambapo kuna kata zangu za Idiri na Usagai.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii tumeshaifanyia usanifu, na kwa kweli Serikali inatafuta fedha ili iweze kuijenga kwa sababu ni kweli ni barabara muhimu na inapita kwenye maeneo mengi na hasa ikiwa inaunganisha hizo wilaya alizozitaja Mheshimiwa Mbunge. Tumeshakamilisha usanifu, kwa hiyo, Serikali inatafuta fedha ili kuijenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Paulo, Mheshimiwa Mashimba Ndaki, ajiandae.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Kwa kuwa ni takribani miaka mitatu sasa, Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara – Mbulu, usanifu wake ulishakamilika na ahadi nyingi za viongozi wetu wakuu zimetolewa kwa wananchi wa Jimbo la Mbulu Mjini. Je, ni lini barabara hii itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda sijamwelewa vizuri, ni Barabara ya Mbulu – Galbad!

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mbuyu wa Mjerumani – Magara – Mbulu, usanifu wake umekamilika kwa miaka miwili zaidi ya miaka miwili sasa. Ahadi nyingi za viongozi wa Kitaifa zimetolewa kwenye hii Barabara. Je, ni lini ujenzi wa barabara hii utaanza kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, umeipata?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hii Barabara ya Mbulu – Mbuyu wa Mjerumani ni barabara ambayo inapita kwenye miinuko mikali sana. Ni kweli maelekezo ya viongozi wetu wa Kitaifa wameshatuelekeza tuijenge kwa kiwango cha lami. Tumeshakamilisha usanifu, lakini kitu cha kwanza ilikuwa ni kujenga kwanza daraja ambalo lilikuwa ni korofi, daraja la Magara ambalo tulishalikamilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, maeneo mengi korofi tulikuwa tunayajenga na bado tunaendelea kuyajenga kwa kiwango cha zege ili ziweze kupitika, na wakati hiyo tunatafuta fedha ili barabara hiyo tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, ajiandae.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa barabara ya Mwigumbi – Maswa inakarabatiwa angalau kila mwaka, mwaka 2024 imekarabatiwa, mwaka 2025 imekarabatiwa, na hata sasa vipande vingi vinakarabatiwa. Je, ni kwa nini Serikali isiifumue barabara hii yote kwa ujumla na kuijenga upya, kwa sababu inaonekana haikujengwa kwa ubora unaotakiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge. Kilichofanyika Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi alishatoa maelekezo kwa Meneja wa *TANROADS* wa Mkoa, lakini pia na Meneja wa Makao Makuu waweze kwenda wakafanye tathmini na watoe taarifa ya kina ili Serikali ione inafanya nini kuhusu hiyo barabara ambayo imekuwa mara kwa mara inafanyiwa matengenezo wakati ni barabara ambayo haijajengwa muda mrefu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali. Barabara ya kutoka Bulige - Kahama kupita Mwakitolyo – Solwa mpaka Salawi ni barabara muhimu sana. Je, ni lini itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara inajengwa kwa kiwango cha lami kwa awamu. Ni kweli tumejenga kidogo kidogo, lakini tumeshakamilisha usanifu. Kwa sasa tunajenga kwa vipande wakati tunatafuta fedha ya kuikamilisha barabara yote.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu hayo kutoka Wizara ya Ujenzi.

Tunaendelea Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa John Stephano Luhende Mbunge wa Bukene aulize swali lake.

Na. 66

**Ujenzi wa Skimu za Umwagiliaji Bukene**

**MHE. JOHN S. LUHENDE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga skimu za umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha kisasa katika eneo la Kisasiga Jimbo la Bukene?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea na utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji katika maeneo mbalimbali katika Mkoa wa Tabora ikiwemo Jimbo la Bukene. Kwa mwaka 2025/2026, jumla ya miradi nane ya upembuzi

yakinifu na usanifu wa kina katika Jimbo la Bukene inaendelea, ambapo utekelezaji wa miradi hiyo umefikia wastani wa asilimia 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ni Kahamanhalanga, Mambali, Ikindwa, Malolo, Igombe, Lakuyi, Nindo na Sigili. Kukamilika kwa upembuzi yakinifu na usanifu, kutaiwezesha Serikali kujua gharama halisi kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji pamoja na kuimarisha miundombinu ya mashambani ili kuwezesha kufanyika kwa kilimo chenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka 2026/2027 imepanga kufanya tathmini katika eneo la Kisasiga kwa lengo la kubaini mahitaji halisi ya miundombinu ya umwagiliaji. Baada ya kukamilika kwa tathmini hiyo, mradi huu utaingizwa katika mipango ya Serikali kwa ajili ya utekelezaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Stephano Luhende.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi nyingine ya maswali ya nyongeza. Swali langu la kwanza la nyongeza, ninataka kuuliza mradi wa umwagiliaji wa Kata ya Sigili, Vijiji vya Iyalemwalagwa na Bulambuka umefikia 39%; na mradi huu umeanza kujengwa tangu 2023, wastani sasa wa chini ya 10% kila mwaka.

(a) Je, ni lini mtaweza kuukamilisha mradi huu ili uweze kuwasaidia wananchi katika shughuli za kilimo?

(b) Je, ni lini mtaanza ukarabati wa bwawa lililopo Kata ya Kahama ya Haranga, ili liendelee kusaidia wananchi walioko huko katika shughuli za kilimo, ufugaji pamoja na uvuvi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Luhende, Mbunge wa Jimbo la Bukene kwa maswali yake ya msingi. Nimthibitishie tu jambo moja, kwamba miradi yote ambayo inatekelezwa katika eneo la jimbo lake na maeneo mengine

yote nchini, Serikali tulishaiweka katika mipango. Jukumu letu ni kuhakikisha kwamba inakamilika kwa wakati. Kwa hiyo, hata hili Bwawa la Bulambuka ambalo amesema ni lini litakamilika, niseme litakamilika kulingana na mkataba ambao tulikuwa tumeandikishana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba muda ulizidi kwa sababu kulikuwa na changamoto ya kifedha. Sasa hivi Wizara ya Fedha imeji-*commit* kutoa fedha kila mwezi ambazo zitasaidia sisi kuwalipa wale wakandarasi ili waweze kukamilisha ile miradi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jibu hilo la kwanza ndilo linaloambatana na vilevile katika mradi wa Bwawa la Kahama Mlanga, kwamba kwa sababu sasa tuna uhakika kwamba tutakuwa na *flow* nzuri ya kupata fedha, maana yake miradi hii sasa tutakuwa tuna uwezo wa kuipelekea fedha na kukamilika kama vile ambavyo imepangwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fadhili Ngajilo, ajiandae Mheshimiwa Rashid Mtima.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi linahusu skimu za umwagiliaji. Pale Iringa Mjini kuna skimu ya umwagiliaji ya wenyeji inayojulikana kwa jina la Mkoga Chelahani inapatikana Kata ya Isakalilo. Hii skimu imeajiri watu wengi sana zaidi ya 10,000 ambao wanaitegemea. Sasa swali, je, Serikali iko tayari kuijenga upya, kuiboresha ili iweze kutoa ajira zaidi kwa wananchi wa Iringa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Vilevile ninamshukuru Mbunge wa Iringa Mjini, Bwana Fadhili Ngajilo na nimwondoe shaka tu, aende akawathibitishie tu wananchi wa Jimbo la Iringa Mjini kwamba, Serikali tuko tayari kufanya ukarabati

na kuboresha skimu hiyo ili kuhakikisha kwamba inaleta tija kwa wananchi wale.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Mtima, ajiandae Mheshimiwa Japhael Lufungija

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuuliza swali la nyongeza katika sekta hii ya kilimo kwamba, ni lini Serikali itakamilisha *designing* ya mradi wa umwagiliaji eneo la Chikwedu, Chipalang'anda na Lipeleng'inyi ambalo utawezesha wananchi wa Vijiji vya Chihanga, Mpilipili, Chiunjila na Tarafa ya Mkunya jumla, ili kutumia maji ya Mto Ruvuma kuweza kumwagilia na kuongeza kipato kupitia sekta hii ya uzalishaji ya Kilimo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimejibu katika maswali niliyotangulia, ni kwamba miradi yote ya umwagiliaji ikiwemo hii ambayo ameitaja Chipalang'anda, (majina yake ni magumu kidogo), lakini miradi yote hii sisi kama Serikali tulishapewa maagizo na Mheshimiwa Rais kuingiza katika mipango, kuifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili tupate gharama halisi, na baada ya hapo tuweze kuitangaza ili iweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *at least* kwenye suala la miradi ya umwagiliaji, kwa sababu ni ajenda kubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita, niseme tu kwamba haya ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais, na sisi jukumu letu ni kutekeleza. Kwa hiyo nimwondoe tu shaka Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalifahamu, na kazi inaendelea.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhael Lufungija, ajiandae Mheshimiwa Azza Hamad.

**MHE. JAPHAEL M. LUFUNGIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Napenda kumwuliza Naibu Waziri kwamba, Jimbo la Ulyankulu kuna mradi wa bwawa la umwagiliaji pale Kata Konanne, ambapo Serikali imeahidi kwa muda mrefu kulijenga, lakini pamoja na

Bwawa la Mwamnange, je, ni lini utekelezaji wa miradi hii utaanza kufanyika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika miradi ambayo Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, tumepanga kuitekeleza kuanzia mwaka wa fedha unaokuja ni pamoja na ambayo baadhi ameitaja Mheshimiwa Mbunge. Kwa hiyo, matarajio ni kwamba sasa tunakwenda katika utekelezaji baada ya kukamilisha upembuzi na usanifu wa kina.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Azza Hamad.

**MHE. AZZA H. HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itaanza ujenzi wa mifereji ya umwagiliaji katika skimu ya umwagiliaji ya Masengwa iliyopo katika Jimbo la Itwangi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena kwamba miradi mingi ya umwagiliaji ambayo Wizara ya Kilimo tunaitekeleza ipo katika hatua mbalimbali. Ipo ambayo tunaifanyia upembuzi yakinifu na usanifu wa kina ili tuweze kupata gharama halisi na kujua *design* za michoro ili tuweze kuitekeleza. Vilevile, ipo ambayo tumeshatangaza kwa ajili ya kupata wakandarasi na ipo ambayo inaendelea kwa maana wakandarasi wako kazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiwemo huu wa mradi wa Masengwa katika Jimbo la Itwangi ni sehemu ya miradi ambayo tunamalizia upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha ili sasa uanze kufanya kazi na wananchi waweze kupata huduma hiyo ya umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Lucy Simirya Kombani, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 67

**Kuboresha Miundombinu kwa Wakulima wa Milimani – Morogoro**

**MHE. LUCY D. S. KOMBANI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuboresha miundombinu kwa wakulima wanaolima milimani Mkoa wa Morogoro ili kudhibiti upotevu wa maji?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kufanya uwekezaji mkubwa wa miradi ya umwagiliaji katika Mkoa wa Morogoro ambapo katika mwaka wa fedha 2025/2026, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inatekeleza jumla ya miradi ya umwagiliaji 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi inayotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa Skimu ya Rudewa - Kilosa yenye ukubwa wa hekta 2,500 ambapo utekelezaji wake umefikia 41% na ujenzi unaendelea. Kukamilika kwa skimu hiyo, kutanufaisha wakulima 3,384 katika maeneo ya Kijiji cha Gongoni, Rudewa - Mbuyuni, Rudewa - Batini na Peapea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali inaendelea na ukarabati wa Skimu saba za Mgongola, Tulokongwa, Itete, Mbalangwe, Kiroka, Msolwa - Ujamaa na Mvumi, ambapo utekelezaji umefikia wastani wa 45% na skimu za umwagiliaji 32 na mabwawa ya umwagiliaji 10 yapo katika hatua ya usanifu kwa zaidi ya 50%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea na jitihada za kuboresha miundombinu ya

umwagiliaji hususan katika maeneo ya milimani ili kudhibiti upotevu wa maji na kuongeza ufanisi wa matumizi yake pamoja na uzalishaji katika kilimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lucy Kombani.

**MHE. LUCY D. S. KOMBANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Swali langu la kwanza la nyongeza, je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya skimu za Lupiro, Euga na Minepa ambapo Skimu hii ya Lupiro tu ikikamilika ina uwezo wa kuhudumia ekari 40,000, na hii ya Euga ikikamilika ina uwezo wa kuhudumia ekari 32,000 ambayo ni sawasawa na wakulima 82,000 watanufaika kwenye skimu hizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Wilaya ya Mvomero hususan kwenye Tarafa ya Mgeta ni wakulima na wasambazaji wazuri sana wa mbogamboga pamoja na matunda, lakini wakulima hawa wamekuwa wakitumia njia za kienyeji kama kutumia mianzi ili kupitisha maji kwenye mabomba yao. Je, Serikali haioni haja ya kuwaboreshea miundombinu hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninampongeza Mheshimiwa Lucy Kombani, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Morogoro kwa maswali yake mawili ya nyongeza ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ni kwamba kuhusu Skimu ya Lupiro na Luhuga kwamba lini tutapeleka fedha, nimwambie tu kwamba skimu hizi ziko katika mpango wa fedha wa mwaka unaokuja kuhakikisha kwamba zinaendelea kutekelezwa. Kwa hiyo, tuko katika hatua za mwisho za kuhakikisha kwamba fedha inashuka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Tarafa ya Mgeta katika Jimbo la Mvomero, amesema wananchi wanatumia mianzi kama sehemu ya mabomba kupeleka maji na ameiomba Serikali kuhakikisha tunaboresha mradi huo. Nimthibitishie tu kwamba mradi huo tayari

tumeshatuma wataalamu wanaofanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kwenda kuboresha ule mradi ili wananchi wale sasa wapatiwe miundombinu bora na ya kisasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haidary Sumry, ajindae Mheshimiwa Josephine Kapoma.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninaomba kumwuliza swali Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, je, ni lini Skimu ya Umwagiliaji ya Kakese ambayo iko kwenye Jimbo la Mpanda Mjini itaanza kujengwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Skimu ya Kakese iliyopo katika Jimbo la Mpanda Mjini, tulikuwa tumeshamaliza upembuzi yakinifu na sasa tunakwenda katika hatua ya kuutangaza ili kupata mkandarasi na ianze kujengwa. Kwa hiyo, nimwondoe shaka tu kwamba ninaamini katika mwaka wa fedha unaokuja shughuli hiyo itaanza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Kapoma.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wa Kata ya Boma Mlimani Luhungo wa Wilaya ya Morogoro Mjini wamekuwa na mgogoro wa muda mrefu na Serikali kwa ajili ya uharibifu wa mazingira. Je, Serikali ina mpango gani wa kuja na mkakati wa kutoa elimu ya mbinu bora za kilimo zitakazozingatia uhifadhi wa mazingira?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nimthibitishie tu Mheshimiwa Josephine kwamba, moja ya mkakati wa Serikali ili kuhakikisha kwamba wananchi hawaendelei kuharibu mazingira, ni pamoja na kuhakikisha tunajenga miundombinu bora na ya kisasa, kwa maana ya mabwawa na *schemes* ili wananchi wale tukishawapanga na kuonesha maeneo

ambayo wanafaa kufanya kilimo chao, maana yake hawatakuwa na nafasi ya kwenda kuharibu mazingira katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, tutaendelea kupeleka timu kwa ajili ya kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kutunza mazingira, kwa sababu sisi mazingira ndiyo ambayo yanatusaidia kupata vyanzo bora vya maji ambavyo sasa miradi yetu ndiyo maeneo ambayo tumekuwa tukitekeleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Kilimo.

Tunaendelea na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum. Mheshimiwa Mariam Madalu Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Maryam Azan.

Na. 68

**Kuimarisha Vikundi vya Wanawake Kiuchumi – Ruvuma**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI K.n.y. MHE. MARIAM M. NYOKA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha vikundi vya wanawake kiuchumi katika Mkoa wa Ruvuma ili wapate fursa za masoko, mafunzo na mitaji?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mariam Nyoka, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inashirikiana na wadau kutekeleza mikakati ya kuendeleza vikundi vya wanawake kiuchumi kwenye mikoa yote, ambapo kwa Mkoa wa Ruvuma jumla ya vikundi vya kiuchumi 9,430 vya wanawake vimeshasajiliwa na usajili unaendelea. Baada ya usajili wa vikundi hivyo, mikakati ifuatayo inaendelea ili kuiimarisha viweze kukidhi kupata mitaji:-

(i) Kutoa elimu na mafunzo ya ujasiriamali ili vikundi viwe na uwezo wa kujiendesha na kutekeleza miradi yenye uendelevu inayokuza ajira na kuongeza kipato;

(ii) Kutoa elimu ya mikopo ikiwemo ile isiyo na riba kuanzia iliyopo kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa na kwenye Taasisi za umma na binafsi;

(iii) Kuendelea kurasimisha biashara za wanawake ambapo kupitia mkakati huu, vikundi vinaendelea kuelimishwa na kusajili biashara zao ili zitambulike kisheria, kupata sifa ya kukopesheka na ukubalifu katika masoko ya ndani na nje;

(iv) Ushirikishwaji wa vikundi kwenye fursa ya kujitangaza, kuongeza wigo wa wateja, kubadilishana uzoefu na kupata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya ukuaji wa vikundi vya wanawake kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Azan.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza, kwa niaba ya Mheshimiwa Mariam Nyoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hatua gani zinachukuliwa kuhakikisha wanawake wanapata taarifa sahihi, fursa na mitaji na masoko mkoani Ruvuma?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Je, Serikali inashirikiana vipi na sekta binafsi au taasisi za kifedha kuongeza fursa za masoko hapa nchini? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Maryam Azan kwa maswali mafupi ya Kibunge. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Maryam Mwinyi kwa kumwakilisha vyema Mheshimiwa Mariam Nyoka. Hakika ameitendea haki hiyo nafasi. Ninapende kujibu maswali yako mawili; kwanza, namna ambavyo wanawake wanapata taarifa kuhusiana na hii mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sisi kama Wizara tuna Kitengo cha Habari ambacho kinafanya kazi kwa weledi mkubwa, kinatoa taarifa katika mitandao ya kijamii. Pia, sisi kama Viongozi wa Wizara tunaendelea kuongea mara kwa mara kwenye vyombo vya habari ili wananchi wote waweze kupata taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika mikutano mbalimbali ya vijiji katika maeneo ya kata, kule tunao Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii na wenyewe wanashiriki katika mikutano ile ya shughuli zao za maendeleo ya maeneo yao, pia na ajenda ya namna ya kupata hii mikopo wanapewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, tuna majukwaa ya uwezeshaji kiuchumi nchi nzima na sasa hivi mikoa yote Mheshimiwa Dkt. Dorothy Gwajima, amehakikisha yamesimama vizuri, lakini wilayani na sasa hivi tunasisitiza hadi kwenye kata, majukwaa ya uwezeshaji kiuchumi yaweze kuimarishwa na wanawake wengi waendelee kujitokeza kujiunga kwa sababu ni wanawake wote wanastahili kuingia katika majukwaa haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye majukwaa yale katika ajenda mbalimbali watakazoongea, wataambizana namna ya kupata mitaji, lakini wataoneshana fursa mbalimbali, lakini vilevile haya masoko pia wanapata kufundishana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kama Wizara, tunashirikiana na Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Halmashauri kwa maana ya Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi. Wote hawa ni kuhakikisha kwamba tunaweza kuwafikia wananchi, na wote wanapata hii fursa ambayo Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan anatamani kuona makundi haya yote yanaweza kufikiwa kwa ukubwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili anasema, namna gani Serikali inashirikiana na sekta binafsi ama taasisi za kifedha kuongeza fursa za masoko kwa vikundi vya wanawake wa Mkoa wa Ruvuma? Ninampongeza sana Mheshimiwa Mariam Nyoka, amekuwa akifuatilia sana suala la kuhakikisha wanawake wameshapata mikopo. Wanapataje sasa masoko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa niseme, sisi kama Serikali tunashirikiana na taasisi binafsi hasa mabenki waweze kutoa fedha kwa kutoa kwanza elimu ya fedha na vilevile namna ya kupata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza *Tanzania Women Chamber of Commerce,* wamekuwa wakifanya kazi nzuri sana. Wamesimamia wanawake ambao ni wajasiriamali wadogo wadogo, wa kati na wakubwa, wote wanaungana. Kwa hiyo, wanabadilishana uzoefu, wanasafiri ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wakina mama wanaendelea kuyapata masoko ndani na nje ya nchi. Hivi karibuni *Tanzania Women Chamber of Commerce* inaratibu wanawake wajasiriamali wadogo wadogo kwenda kwenye maonesho ya 66 ya biashara ya Kimataifa huko Bulawayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, biashara mbalimbali ndogo ndogo, wakina mama wanapata mwanga, wanafika kule nchi jirani, wanapata kuongeza masoko mapya. Pia, hata hapa hapa Tanzania wamekuwa wakifanya haya yote pale Arusha, Mbeya, Dar es Salaam, Mwanza, lakini tunaona namna makundi ya wanawake yanaendelea kuimraika. Vilevile, taasisi kama *BRAC* pia inaendelea kufanya vizuri

kuona kwamba masoko yanapatikana kwa wanawake, lakini kama Wizara tunafanya kazi na Wizara karibia zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwa wachimbaji wadogo wadogo, kwa maana ya Wizara ya Madini, unakuta pale kuna *TAWOMA*. Pia wanafundishana na kupeana taarifa mbalimbali kuhusu namna ya kupata masoko ya bidhaa zao na shughuli ndogo ndogo wanazozifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Chama cha Wahandisi Wanawake na wenyewe hawako nyuma, wanafanya vizuri sana na wanaoneshana kazi mbalimbali na wanashiriki kazi mbalimbali na wanapata masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Baada ya majibu hayo ya kina, kuna maswali jamani kweli! Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kuna baadhi ya vikundi vya wanawake katika Mkoa wa Mtwara, hawajapata mikopo kwa takribani miaka miwili, wamekuwa wakifuatilia kutoka vijijini kwenda kwenye halmashauri zao za wilaya, je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wakurugenzi ambao hawawezeshi upatikanaji wa mikopo kwa wanawake hao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Hili kauli ya Serikali kwenye mikopo Mtwara.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mtwara. Ninampongeza sana kwa kazi nzuri dada yangu amekuwa akifuatilia hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoweza kusema kwa Wakurugenzi wote nchini, tafadhali sana msiangushe jitihada za Mheshimiwa Rais. Makusanyo ya ndani ya 10% ni haki ya msingi, zile asilimia nne

wanawake kuzipata. Hivyo ninapenda kutoa wito kwa wanawake kufika halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale ambao bado hawajapata hii mikopo maafisa maendeleo yetu ya jamii tunaendelea kuwasisitiza kuwasaidia hawa wanawake kufikia vile vigezo vyote ili waweze kupatiwa mikopo. Wengine wanachelewa kupata, huenda anakosea kitu kidogo katika kukidhi vigezo vya kupata mkopo, hivyo Maafisa Maendeleo ya Jamii niwasihi sana wafanye kazi yao ili wanawake wote kwenye halmashauri zote ikiwemo ya Mtwara waweze kupata mikopo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, na Mheshimiwa Shadya Omar ajiandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kipekee kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kazi nzuri anayoifanya, anapambana hata kupitia mitandao kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo mbalimbali yanayotekelezwa na Serikali hii, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa baada ya maeneo hayo ya utangulizi niulize swali langu la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kufupi CCM ina lengo zuri la kutoa mikopo kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kule nyuma mikopo hii ilikuwa inatolewa na halmashauri, lakini kwa sasa mikopo imehamishiwa kwenye benki. Zipo changamoto ambazo zinajitokeza ikiwa ni pamoja na ucheleweshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri mimi nimewahi kufanya kikao na vijana wa bodaboda, tunafahamu kwamba bodaboda ni sehemu ya ajira. Wanacholalamika ni kwamba hata kama kajaza fomu na kuweka viambatanisho vyote, mwisho wa siku hapati mkopo, na hapati majibu yoyote kwamba umechelewa kupata mkopo kwa sababu fulani…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sikudhani, swali…

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nini sasa kauli ya Serikali katika kuhakikisha inapitia upya hizo changamoto ili kurahisisha mikopo kwa makundi hayo maalumu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninashukuru kwa pongezi, vile vile naomba kujibu swali hili kuhusu, changamoto zinazopatikana kwenye benki. Kwa sasa hivi sisi kama Wizara, benki tunayoitumia ni *NMB*. Kulingana na makubaliano tuliyoyafikia changamoto hizi kwa sasa hivi zimepungua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakati mikopo hii inatolewa pale halmashauri, ilikuwa, Mheshimiwa Diwani naamini unakumbuka namna ambavyo watu wanakopa hawarejeshi, kwa hiyo, wale wengine sasa wanashindwa kupata kwa sababu waliokopa awali hawajaresha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutibu hilo, Serikali iliona ni vyema sasa tuweze kushirikiana na sekta binafsi kwa maana ya benki, wenzetu wana uzoefu na namna nzuri ya kufuatilia ili mikopo hii iweze kurejea ili kuwe na mzunguko kwa watu wengine, baada ya wengine kurejesha. Hiyo ndiyo ilikuwa sababu kubwa ya kutoka halmashauri kwenda benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingi tumeweza kuzishughulikia, mambo mengi yaliyokuwa ni vikwazo, tumeweza kuongea na wenzetu wa sekta binafsi kwa maana ya benki, wameyaondoa kama matumizi ya hati, matumizi ya vyeti vya ndoa, tumeweza kuyaondoa ili kupunguza kero katika upatikanaji wa mikopo hii iliyotolewa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa bodaboda ninapenda tu kutoa taarifa kwamba kwanza wamepatiwa mkopo maalumu kabisa wa

wafanyabiashara wadogo wadogo na wakapunguziwa mpaka riba, wakapewa kwa asilimia saba tu *single digit* kwenye mkopo. Yote hii ni kuona kwamba tunaendelea kuwawezesha wakuwe. Kama Wizara, tutaendelea kusimamia kuhakikisha kwamba changamoto zote zinazoendelea kujitokeza tunaziondoa ili lengo la Mheshimiwa Rais liweze kutimia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shadya Omar.

**MHE. SHADYA HAJI OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niendelee kuipongeza Wizara hii kwa mazuri ambayo wanayafanya na mengi tukiwa tunayashuhudia. Niende moja kwa moja kwenye swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vikundi vingi vya akina mama vinakufa kwa sababu ya mitaji pamoja na masoko ya uhakika. Je, Serikali ina mpango gani wa kuunganisha wanawake hawa na masoko ya *EAC* na *SADC* badala ya kutegemea masoko ya ndani?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE WA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Shadya kwa pongezi, lakini kuona kwamba Serikali inaunganisha haya makundi ya wanawake na masoko ya nje kama nilivyotoka kujibu swali langu lile la kwanza kwa mwuliza swali la msingi. Tayari tunafanya, ila niseme kwamba tunapokea huu ushauri ili kuongeza kasi ya kuona tunawapeleka makundi ya wanawake kwenye masoko ya nje zaidi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum.

Tunaendelea sasa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, aulize swali lake.

Na. 69

**Minara ya Simu Kata za Kikolo na Kagugu**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga minara ya simu katika Kata za Kikolo na Kagugu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika kukabiliana na changamoto za upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu nchini, ilifanya tathimini katika Kata ya Kikolo inayojumuisha Vijiji vya Kikolo, Njomlole, Uzena na Luhehe na kukijumuisha Kijiji cha Kikolo katika Mradi wa Mawasiliano vijijini awamu ya tisa unaosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari ambapo mtoa huduma ambaye ni Shirika la Mawasiliano Tanzania - *TTCL* anajenga mnara katika kijiji hicho na utekelezaji wa ujenzi wa mnara huo unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata ya Kagugu inayoundwa na Vijiji vya Kagugu, Makunguru, Mtetema, Makatani na Maganagana, Serikali kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote - *UCSAF* itafanya tathmini katika kata hii ili kupata mahitaji halisi ya huduma za mawasiliano na kuyaweka maeneo yatakayobainika kuwa na uhitaji katika mpango mkakati wa ujenzi wa minara kwa mwaka 2025/2030.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu mazuri. Pili ninaishukuru Serikali kwa kuanza kujenga mnara wa simu katika Kata ya Kikolo, na pia kufikiria kuanza kufanya tathmini ya kujenga mnara wa simu katika Kata ya Kagugu. Nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, mradi unaoanza kutekelezwa kujengwa mnara katika Kata ya Kikolo unakwenda kwa kusuasua. Nataka nijue, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa mnara huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kijiji cha Ruangai eneo la Kipungu Kata ya Mpepai kuna changamoto kubwa ya mawasiliano ya simu. Ni lini Serikali itaweka mkakati wa kuhakikisha kwamba inajenga mnara wa simu katika eneo hili ili wananchi waweze kupata mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa mnara tulioutaja katika Kijiji cha Kikolo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hii itakamilika tarehe 30 Juni, 2026, kwa sababu tayari mkandarasi ameshapatikana na anaendelea na *mobilization*. Atakapokamilisha *mobilization*, ujenzi utaanza mara moja. Ifikapo tarehe 30 mwezi wa Sita, ujenzi huu utakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto ya mawasiliano katika Kijiji cha Luhangali, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mkakati wetu wa Serikali wa miaka mitano kuanzia mwaka 2025 kwenda mwaka 2030, tutafanya tathmini katika maeneo yote yenye changamoto na tutayafikia. Tutaanza na maeneo ya changamoto kubwa, changamoto za kati na changamoto zenye unafuu. Kwa hiyo, tutapitia zote na kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2030 kila Mwananchi wa Tanzania atakuwa na uso wenye furaha katika sekta hii ya mawasiliano.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Happiness Ngwando, halafu ajiandae Mheshimiwa Lucy Mwakyembe.

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kuuliza swali la nyongeza. Serikali ina mpango gani wa kuweka *network* kwenye hospitali zetu ambazo zinatumia *system,* ili kupunguza mgonjwa kukaa muda mrefu kumsubiria daktari apate *network*. Kwa mfano, Hospitali ya Wilaya ya Nyasa na Nangombo, Tunduru, ili daktari apate *network* inabidi atoke nje kutafuta mnara. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka *network* haraka ili wananchi wetu wasipate usumbufu wa kusubiri majibu muda mrefu hususan wanawake wa Mkoa wa Ruvuma? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwamba tuna mkakati wa miaka mitano wa kupeleka mawasiliano ya simu na *data* katika maeneo yote nchini. Katika haya maeneo ya hospitali na maeneo mengine muhimu, tutayatekeleza katika awamu ya 11 ambapo Serikali ina mpango wa kupeleka mawasiliano ya *internet* na *data* katika maeneo ya mkakati yakiwemo haya ya miundombinu ya Serikali ikiwemo Reli ya *TAZARA, SGR, MGR* ikiwemo mbuga ya hifadhi za wanyama na maeneo mengine ya kimkakati kama hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba eneo hilo pia kama Serikali tunalifanyia kazi na lipo kwenye mkakati mahususi wa Wizara. Kwa hiyo, tutalifanyia kazi na maeneo yote hayo yatapata mawasiliano ya *internet.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na tumshukuru sana Mheshimiwa Happiness kwa maswali yake na kuweka msisitizo kuhakikisha kwamba Wilaya ya Nyasa na Tunduru zinapata mawasiliano ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Happiness, katika mradi wetu wa utekelezaji wa ujenzi wa minara 201, Wilaya ya Nyasa tutaweka minara miwili katika Kata ya Liuli pamoja na Mpepo. Vilevile kwa Wilaya ya Tunduru tutajenga mnara katika Kata ya Mchesi pamoja na Mlingoti Magharibi. Hivyo basi, niendelee kumhakikishia kwamba sasa hivi tunakamisha ujenzi wa minara 908 katika kata 730, na tutahakikisha kama Mheshimiwa Naibu Waziri alivyoeleza katika makakati wetu, tuwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, ifikapo 2030 hakuna eneo ambalo litakuwa halina mawasiliano. Nashukuru kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waziri wetu, Mheshimiwa Angellah Kairuki na Waheshimiwa Wabunge, nasisitiza tu na kukumbusha kwamba maswali ya nyongeza yaendane na maswali ya msingi. Vinginevyo Mheshimiwa Waziri anaweza kujibu kama binadamu, hawezi kujua nchi nzima ipoje kwa wakati ule, lakini ukiuliza kwa mujibu wa swali la msingi, anaweza kujibu swali kwa ukweli na nyie mkapata faida.

Tunaendelea na Mheshimiwa Lucy Mwakyembe.

**MHE. LUCY E. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali katika Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Ni utaratibu gani unaotumika kwa kutumia mkongo wa Taifa katika kupeleka mawasiliano kule Zanzibar ili kufikisha huduma kwa wateja kwa haraka sana na kwa maeneo ambayo hayafikiki?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu unaotumika katika kupeleka mawasiliano Zanzibar kupitia mkongo wa Taifa, huwa kwanza inafanyika tathmini, kuangalia uhitaji wa maeneo husika, ikishafanyika, Shirika la Mawasiliano Nchini hupeleka mawasiliano hayo kulingana na uhitaji wa eneo husika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda Mbunge wa Buhigwe.

Na. 70

**Ujenzi wa Chuo cha Tehama Buhigwe**

**MHE. PROF. PIUS Z. YANDA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga Chuo cha TEHAMA Wilayani Buhigwe ili kutekeleza ahadi ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Pius Zebhe Yanda, Mbunge wa Buhigwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imewezesha upatikanaji wa eneo la ujenzi wa chuo lenye ukubwa wa ekari 155 katika Kijiji cha Songambele, Halmashauri ya Wilaya ya Buhigwe. Pamoja na hiyo Serikali tayari imekamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini ya gharama ya ujenzi wa chuo ambapo inakadiriwa kuwa kiasi cha shilingi bilioni 113 kitahitajika kukamilisha ujenzi husika. Kwa sasa Serikali inaendelea na utaratibu wa kutafuta vyanzo mbalimbali vya fedha ili kuanza ujenzi wa chuo husika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Pius Zebhe Yanda.

**MHE. PROF. PIUS Z. YANDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, kwa kuwa taaluma ya teknolojia ya TEHAMA sasa hivi ni taaluma ya msingi sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali kwamba ujenzi wa chuo hicho uweze kupata kipaumbele. Hii itawezesha kwanza kunufaisha vijana ambao wakipata elimu hiyo wataweza kujiajiri kwa sababu ya ile elimu waliyoipata. Pia, hiyo itasaidia kusukuma gurudumu la maendeleo kwa kutumia teknolojia ya maendeleo vijana wetu watakuwa wamepata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa misingi hiyo basi, ombi letu ni kwamba, Serikali ione jinsi gani iweze kupata uwezeshaji wa ujenzi wa hicho chuo, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri umepokea hayo maombi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Profesa, amekuwa akilifuatilia suala hili kwa karibu kwa Mheshimiwa Waziri na pia kwangu. Hii inaonyesha kwamba ana hamasa kubwa ya masuala ya teknolojia ya Habari, na Wananchi wa Buhigwe pia wana hamasa hiyo. Nimhakikishie kwamba ombi lake tumelipokea, na tutatoa kipaumbele kikubwa katika ukamilishaji wa chuo hicho.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana, ninakushukuru kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala, Mbunge wa Ndanda, aulize swali lake.

Na. 71

**Fidia kwa Wananchi Waliopitiwa na Mradi wa *Grid* ya Taifa**

**MHE. FARAJI B. NANDALA** aliuliza: -

Je, lini Wananchi wa Kata za Chikukwe, Chigugu, Chikundi, Mwena, Ndanda na Nanganga ambao wamepitiwa na Mradi wa *Grid* ya Taifa watalipwa fidia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala Mbunge wa Ndanda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa fedha wa 2025/2026 Serikali imetenga bajeti kwa ajili ya malipo ya fidia yenye thamani ya shilingi bilioni 5.1 kwa wananchi 1,730 wanaopisha njia ya kusafirisha umeme ya msongo wa kilovoti 220 kutoka Masasi hadi Mahumbika. Hivyo, naomba kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kuwa fidia hii italipwa mwaka huu wa fedha kadri itakavyopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Faraji Buriani Nandala.

**MHE. FARAJI B. NANDALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati. Nina maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya eananchi wa Jimbo la Ndanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2025/2026 ndiyo hii ambayo tunaitekeleza na tunaelekea kuikamilisha hivi karibuni. Hizi fedha shilingi bilioni tano zilishatengwa, ina maana zipo. Kwa hiyo, nataka majibu ya Serikali, ni lini hasa watawalipa hawa wananchi wakati tuko kwenye *process* za kupitisha bajeti mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; ninataka kufapata ushauri wa Serikali, je, wale wananchi waendelee kuandaa mashamba yao au wasiendelee, kwa sababu hii gridi ya Taifa inapita kwenye mashamba ya wananchi? Kama wasiandae yale mashamba, je, Serikali itakuwa tayari kulipa penati itayotokana na kuchelewesha kulipwa kwa hii fidia yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninampongeza sana kaka yangu Mheshimiwa Faraji kwa kufuatilia maslahi ya wananchi wake wa Ndanda, amekuwa anatufuatilia mara kwa mara na kuja ofisini kwa ajili ya kujua hatima ya *line* hii ambayo itaingiza mikoa ya Lindi na Mtwara katika gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa, sisi Wizara ya Nishati pamoja na Wizara ya Fedha, tunajitahidi sana kuhakikisha kwamba fidia italipwa kwa wakati ili wananchi hawa wasiingie kwenye mgogoro mwingine kati yao na Serikali. Kwa hiyo, hilo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunajitahidi kutafuta fedha, na bado muda tunao, na hilo litatendeka ndani ya mwaka huu wa fedha, Mwenyezi Mungu akitujalia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni takribani miaka miwili inaenda mitatu sasa tangu Wananchi wa Kipagalo – Bulongwa - Iniho wapishe mradi wa Bwawa la Umeme la Lumakyala lakini Serikali haijatoa kauli ni ipi jibu la Serikali kwa wananchi hawa ili waweze kupata fedha zao kutokana na tathimini iliyofanyika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utaungana nami kukubaliana kwamba Mheshimiwa Sanga amekuwa ni Mheshimiwa Mbunge kinara katika kufuatilia maslahi ya wananchi wake wa Jimbo la Makete. Nimhakikishie, hili bwawa la umeme litazalisha Megawati 222, na ni la muhimu sana katika kuchangia megawati 8000 ambazo ndiyo lengo la Serikali kwa mwaka huu mpaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatafuta fedha kupitia *TENESCO* na *TANESCO* ipo katika mazungumzo na wabia mbalimbali ili tuweze kujenga mradi huu kwa *PPP*. Wananchi wake watalipwa fidia na

tutajenga bwawa hili na tutafikia adhima yetu ya kuzalisha umeme ya Megawati 222.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Emanuel Nuwas ajiandae Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. DKT. EMANUEL Q. NUWAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mji Mdogo wa Haydom ambao unategemea umeme kutoka Mji wa Katesh ambapo umeme huo hupita umbali mrefu sana na hivyo Mji huu kupata changamoto ya umeme kukatikatika mara nyingi, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga kituo cha kupoozea umeme ili kuwahakikishia wananchi hao kupata umeme wa uhakika?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la Serikali siyo tu kuhakikisha taa zinawaka, lakini pia ni kuhakikisha nishati ya umeme inatumika kwa ajili ya uchumi. Kwa sababu hiyo, ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanapata umeme wa kutosha ambao utawasidia katika kuendesha maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Mbunge nimelipokea, tutajenga *substation* katika eneo hili ili kuimarisha upatikanaji wa umeme ambao unaweza kusaidia katika uchumi wa eneo lake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Innocent Bashungwa, ajiandae Mheshimiwa Marirta Kivunge.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza ninaishukuru Serikali kwa mpango wa kuweka Mkoa wetu wa Kagera kwenye gridi ya Taifa, na katika mipango hii wananchi wa Kata za Nyakahanga, Kata ya Bugene na Kata ya Kayanga wamepisha ujenzi wa gridi ya Taifa, lakini hawajapata fidia. Je, ni lini watalipwa fidia?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Innocent Bashungwa kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuzungumza na wananchi wake ili waweze kuridhia kupisha mradi wa *line* ya umeme katika eneo hilo ambalo kimsingi kama alivyosema, litatusaidia kuunganisha Mkoa wa Kagera katika katika gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, mpaka sasa tumeshalipa shilingi milioni 385 ili kuweza kujenga *substation,* lakini tutakwenda kulipa shilingi bilioni 5.8 kwa wananchi zaidi ya 1,001 ambao wao wameridhia kupisha ujenzi wa *line* ambayo itasafirisha umeme kwenda katika Mkoa wa Kagera. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Marirta Kivunge, ajiandae Mheshimiwa Tinnar Chenge, halafu atamalizia Mheshimiwa Florent Kyombo. Maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. MARIRTA G. KIVUNGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Je, ni Serikali itakamilisha zoezi la kufikisha umeme kwenye vitongoji vilivyosalia katika Wilaya ya Longido na hasa kwenye vyanzo vya maji?

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa swali fupi la Kibunge. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha ifikapo mwaka 2030 vitongoji vyote ndani ya nchi yetu vinapata umeme. Nimhakikishe Mheshimiwa Mbunge, sisi kama Serikali tutafika kwenu na tutakapopata fedha, tutahakikisha kwamba vitongoji hivyo alivyovitaja vianapata umeme na Mheshimiwa Mbunge atakuwa ni sehemu ya watu ambao tutakwenda kuzindua kuwasha umeme kwenye vitongoji hivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tinnar Chenge.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Kumekuwa na changamoto ya kukatikakatika umeme katika Mkoa wa Simiyu, na Serikali iliahidi kutoa fedha kwa ajili ya kujenga kituo cha kupozea umeme. Je, ujenzi huu umefikia hatua gani? Lini utakamilika ili kuondoa changamoto hii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia namna ambavyo Wizara ya Nishati inaendelea kutekeleza majukumu ya ujenzi wa *substation* katika eneo la Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi inaendelea na mpaka sasa ujenzi wa *substation* umefika zaidi ya 30%. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira. Ninamhakikishia mara baada ya *substation* hiyo kukamilika, Mkoa wa Simiyu utakuwa umeondokana na changamoto ya kukatikakatika kwa umeme. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Florent Kyombo.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi. Wananchi wa Jimbo la Missenyi walipisha ujenzi wa Mradi wa Kakono ambao unaleta umeme katika *substation* ya Kyaka. Sasa hivi ni takribani miaka mitatu, na mwaka 2025 tathmini ilifanyika, wanadai shilingi bilioni 1.5, lakini mpaka leo hawajalipwa. Je, ni lini sasa wananchi hao watalipwa ili waweze kuendelea na maisha yao mengine na kupisha mradi uendelee?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Mbunge kwa ajili ya kuzungumza na wananchi wake hata waliridhia kupisha mradi huu wa kujenga *Substation* ya Kakono. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, tutakwenda kulipa fidia kwa wananchi hawa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kwa kadiri fedha ambavyo itapatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu hayo mafupi na yenye kueleweka. Tunashukuru sana Wizara ya Nishati.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Moses Ludovico Kaegele, Mbunge wa Nkasi Kusini, aulize swali lake.

Na. 72

**Kuongeza Ardhi kwa Wananchi wa Nkasi Kusini**

**MHE. MOSES L. KAEGELE** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaongeza ardhi kwa wananchi wa Vijiji vya Kasapa, King'ombe, Mlambo, Kala na Ng'undwe kutoka Hifadhi ya Lwafi kwa ajili ya kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hifadhi ya Msitu Loasi ilianzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 346 la 25/10/ 1957 ikiwa na ukubwa wa hekta 33,468. Msitu huu unazungukwa na vijiji vinne ambavyo ni King'ombe, Mlambo, Kilambo Mkorochi na Mpasa. Vijiji hivyo vilibainika kuvamia sehemu ya hifadhi kwa matumizi mbalimbali ya kijamii ambapo Baraza la Mawaziri kupitia Kamati ya Mawaziri nane wa kisekta lilielelekeza Serikali kumega hifadhi ili kupata suluhu ya migogoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mwaka 2023 Serikali ilitekeleza Maelekezo hayo kwa kumega eneo lenye ukubwa wa hekta 10,834 (sawa na ekari 27,050) kutoka kwenye hifadhi na kugawiwa kwenye vijiji kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali haioni haja ya kuendelea kumega eneo la hifadhi kutokana na umuhimu wake wa kiikolojia na kijamii. Hii inatokana na ukweli kwamba hifadhi hii ni chanzo kikuu cha maji ya Mto Loasi na Msalamba. Hali kadhalika,

inahifadhi mimea na Wanyama, inasaidia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuepusha migogoro ya wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine maji yanayotiririka kutoka hifadhi hii huchangia katika maporomoko maarufu ya Kalambo *(Kalambo Water Falls)* ambayo huchochea utalii na uchumi wa nchi katika ukanda huo. Aidha, Serikali inaendelea kuhimiza wananchi kushiriki katika shughuli za uhifadhi na kutumia hifadhi kwa shughuli rafiki za kimazingira kama ufugaji nyuki ili kujipatia kipato endelevu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Moses Ludovico Kaegele.

**MHE. MOSES L. KAEGELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Serikali kwa majibu ambayo yana matumaini, lakini nina swali moja la nyongeza. Katika vijiji hivyo yapo maeneo ambayo yapo nje ya Hifadhi ya Loasi ya mipaka ya Hifadhi ya Loasi halali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado maeneo hayo yanaendelea kulindwa na watu wa hifadhi; na kwa kuwa wananchi wanaongezeka, lakini ardhi haiongezeki, je, Serikali haioni ni muda mwafaka basi wa kwenda kuangalia hiyo mipaka ili yale maeneo ambayo yapo nje ya hifadhi yaweze kurejeshwa kwa wananchi waweze kujiandaa na msimu wa kilimo ujao kwa ajili ya kuwaepusha na migogoro mingine ambayo inaweza kutokea? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali la Ndugu yangu Mheshimiwa Kaegele, kwanza ninampongeza sana kwa namna anavyowapambania wananchi wake hasa katika suala hili. Ni mara kadhaa anakuja ofisini, tunakaa kuzungumzia jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, Serikali imepokea ushauri wake na ipo tayari kupeleka wataalamu wake kushirikiana na Halmashauri

pamoja na Ofisi ya Mbunge ili kwenda kuhakiki mipaka hii na kutoa ufafanuzi unaofaa kwa maendeleo na maslahi ya wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu hayo kwa Mheshimiwa Mbunge.

Tunaendelea na kumalizia na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 73

**Kuongeza Gati Bandari ya Dar es Salaam**

**MHE. AMINA ALI MZEE** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza gati katika Bandari ya Dar es Salaam ili kuhudumia meli nyingi zaidi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Vitu Maalum Vijana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia utekelezaji wa Mradi wa *DMGP (Dar es Salaam Maritime Gate Project)* katika Bandari ya Dar es Salaam unaoendelea ambao umehusisha uboreshaji wa gati nane kuanzia gati namba sifuri hadi gati namba saba, ikiwa ni pamoja na uongezaji wa kina cha lango la kuingilia meli *(Entrance Channel)* hadi kufikia meta 14.5 na lango la kugeuzia meli *(Turning Basin)*, mradi huu umechangia kuongeza ufanisi na uwezo wa kuhudumia meli kubwa zaidi kuliko hapo awali na hivyo kuongeza idadi ya meli na kiasi cha shehena inayohudumiwa na Bandari hiyo kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA)* inaratibu mpango wa ujenzi wa

gati mpya zipatazo 10 ili kuhudumia meli nyingi zaidi kwa wakati mmoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Ali Mzee.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, pia ninaipongeza Serikali yetu inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uendelezaji bora wa Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ni yapi manufaa ambayo yamepatikana katika uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam hasa kutokana na uwekezaji ambao umefanyika mwaka 2023?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, ni ipi mikakati ya Serikali katika kuboresha Bandari ya Dar es Salaam katika kukuza biashara na kuweka ushindani katika *East Africa* na *SADC*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mbunge wa Viti Maalum ambaye anawakilisha kundi la vijana, kwa sababu kupitia maelezo yake na ufuatiliaji wake anathibitisha umuhimu na namna ambavyo vijana wa CCM walivyo makini kufuatilia maendeleo ya vijana wenzao katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kazi kubwa imefanyika na ninashukuru kwa pongezi zake ambazo amezielekeza moja kwa moja kwa Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa maono makubwa na mapana ya namna ya kutumia bandari zetu kugeuza kuwa uchumi kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikishwaji wa sekta binafsi katika uendeshaji wa bandari kwenye Taifa letu, upo kwa mujibu wa sheria. Hivyo basi, baada kuona umuhimu mkubwa, ndiyo maana Serikali

ikaamua kufanya hivyo. Ninapenda sasa kumjibu kwenye hoja yake aliyozungumza kuhusu manufaa ambayo tumeyapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ifahamike kwa Watanzania na Wabunge wote kwamba tuliposhirikisha sekta binafsi, *especially DP World* kwa ajili ya kuendesha kitengo namba moja, mwaka 2024 haikuwa mara ya kwanza. Mara ya kwanza, kazi hii iliwahi kufanyika mwaka 2000 ambapo wenzetu wa *TICTS* walipewa mkataba wa zaidi ya miaka 20 kuendesha sehemu ya makasha pale Dar es Salaam. Mwaka 2024 tulishirikisha wenzetu wa *TICTS* pamoja na wenzetu wa *DP World* kitengo cha kwanza, pamoja na *East Africa Gateway Terminal Limited* kitengo cha pili ili watusaidie katika kuendesha. Manufaa ambayo tumeyapata ni mengi na makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni kwenye utoaji wa huduma ya meli. Hapo zamani, kuna kitu kilikuwa kinaitwa *ship turnaround time*, yaani muda ambao meli inatumia kuanzia inapofika, inakwenda kuhudumiwa na inaondoka. Zamani zilikuwa zinatumika takribani siku 30. Zimeshuka mpaka kuwa siku nne kutokana na kazi kubwa ambayo wanafanya wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuna kitu kinaitwa *Ship turn at berth*, yaani muda ambao meli inahudumiwa ikiwa kwenye eneo la gati. Zamani tulikuwa tukitumia kuhudumia mpaka siku 10, lakini imeshuka mpaka siku tatu. Hii yote inaongeza ushindani wa bandari yetu. Ndiyo maana ukienda kwenye *ranking* leo za bandari unakuta bandari yetu imekuwa ya 373 wakati ya wenzetu majirani zetu pale Mombasa imekuwa ya 393. Kwa hiyo, tuko mbele yao kiufanisi. Tembeeni kifua mbele Watanzania, kwa sababu kazi hii ni nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, manufaa makubwa ambayo tunaweza kuyazungumza, mengine ni kwenye upande wa makasha. Makasha yaliyokuwa yanahudumiwa wakati huo kwa Bandari ya Dar es Salaam peke yake ilikuwa 728,000, leo imefika 1,080,000. Hivyo, kuifanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa miongoni mwa Bandari kubwa katika Bara la Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni shehena kwa maana ya mzigo. Wakati huo tulikuwa tunahudumia tani 16,000,000 kwa maana ya Bandari ya Dar es Salaam. Leo imefika tani 27,000,000 ndani ya muda mfupi ya muda miaka michache. Hii yote ni kwa sababu ya uwekezaji ya ambao tumeufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kwenye idadi ya meli. Meli zilizokuwa zinahudumiwa kwenye Bandari ya Dar Salaam peke yake ilikuwa ni meli 880 zimeongezeka mpaka kufika meli 1,245, wakati meli zote Kitaifa zimeongezeka kutoka meli 4,241 mpaka meli 4,888. Hii yote ni kwa sababu ya maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuamua kushirikisha wawekezaji katika bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, magari yaliyokuwa yanahudumiwa mwaka 2021/2022 mpaka 2023, yalikuwa ni machache, takribani magari 100,047. Mara baada ya kufanya maamuzi hayo, magari yanayohudumiwa yamefika 216,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, hata mapato ya *TPA* yalikuwa shilingi bilioni 896 kwa mwaka. Mara baada ya kufanya maamuzi haya, mapato yakaongezeka mpaka yakafika takribani shilingi trilioni mbili, ya *TPA* 1.3, na yanayobaki ya wawekezaji. Pesa hiyo ndiyo imekwenda sasa kwenda kujenga na bandari nyingine kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, hata wenzetu wa *TRA* wameongeza fedha zao maradufu zaidi. Fedha kwenye Mfuko wa Serikali zimeongezeka, ndiyo maana hata wanafunzi wa elimu ya juu sasa wamekuwa wengi zaidi takribani 235,000 kutoka 170,000. Kwa sababu gani? Mheshimiwa Dkt. Samia ameongeza fedha kwenye mfuko wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, shehena ya nchi yetu inayokwenda kwenye nchi jirani ilikuwa ni tani 5,600,000. Kutokana na ufanisi na mzigo kuongezeka, shehena imeongezeka na kufikia milioni 12.6. Hata Wabunge wenyewe wanakubali na kusema kwamba kweli Mheshimiwa Dkt. Samia ameamua kuibadilisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge ameuliza je, ni ipi mikakati ambayo Serikali hii ya Awamu ya Sita imejiwekea kuifanya Bandari yetu ya Dar es Salaam kuwa shindani? Ninataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na Mheshimiwa Amina Ali Mzee ambaye anatoa sauti kwa niaba ya vijana wa nchi hii wanaopenda kuona nchi yetu ikinufaika na uchumi wetu. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anayo mikakati mingi, ninaomba nitaje michache:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, kama nilivyosema kwenye swali la msingi, ni kuhakikisha kwamba tunaongeza gati kwenye Bandari Dar es Salaam na tayari Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi ameshaanza vikao, na ameielekeza Mamlaka ya Bandari Tanzania iharakishe mchakato huo ili tupate gati nyingi zaidi.

Muheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, tunaboresha reli yetu kama ulivyoona ule mradi ambao tunaufanya na mzigo tunaobeba unafanyika wakati Reli ya *TAZARA* ambayo Mheshimiwa Dkt. Samia anaihubiri haijaanza kufanya kazi vizuri. Reli ya *SGR* haijaanza kutekeleza kazi yake vizuri. Je, tukikamilisha *SGR*, na kukamilisha *TAZARA,* hali itakuwaje? Maana yake ufanisi wetu utaongezeka zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi wote ni mashahidi, kila akisimama hapa Waziri wetu Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa anaelezea kwa kina na uchungu mkubwa umuhimu wa ushirikishwaji wa sekta binafsi. Moja ya mkakati wetu ni kuendelea kuwaalika Watanzania na wasio Watanzania, maadamu ni wawekezaji, waje kuwekeza kwenye sekta yetu. Walete meli, wajenge *SGR*, walete matreni na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo ni nini? Kuiongezea uwezo mamlaka yetu. Hapa asubuhi mmesikia ninyi wenyewe kwamba tunakwenda kushirikisha sekta binafsi kwenye kujenga barabara kuondoa msongamano kutoka maeneo ya Kibaha mpaka Chalinze, kutoka Chalinze mpaka Morogoro na maeneo mengine. Yote hii sasa ili mzigo unaotoka Bandari ya Dar es Salaam uweze kufika maeneo husika katika muda ambao umepangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa maelezo hayo au majibu hayo ya ziada kuonesha mafanikio katika Wizara yetu ya Uchukuzi. Ninakushukuru sana kwa majibu hayo kwa Mheshimiwa Mbunge.

Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umefikia mwisho kwa siku ya leo. Ninawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote ambao wanajitahidi kuuliza maswali mafupi ya Kibunge na Mawaziri ambao wanajibu *straight forward* kwa maana ya moja kwa moja kwenye *point*. Pia, niendelee kuwaomba tuulize maswali ambayo yanaendana na swali la msingi, na kama kawaida yawe mafupi kwa mujibu wa Kanuni.

Pia, kwa nidhamu tu nzuri ukishauliza swali moja la nyongeza, basi usiombe tena mara ya pili kwa sababu kuna wengi wanahitaji kuuliza. Kwa hiyo, mnaporudia mara mbili tatu, sisi kama binadamu tunaweza tukakosea tukampa mtu mara mbili, halafu mwingine akakosa. Kwa hiyo, ukishauliza mara moja, basi ni bora uwaachie wengine waweze kuendelea kuuliza.

Baada ya maelezo hayo, kuna matangazo ya wageni ambao wapo Bungeni asubuhi hii. Nitaanza na wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Wapo wageni 24 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge ambao ni Watumishi wa *Geita Media Group* wakiongozwa na Ndugu Salma Mrisho. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Pia, tunao wageni ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Yupo Ndugu Nicholas Pungameza, Mtumishi wa Kanisa la *EAGT* kutoka Jijini Arusha. Karibu sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 15 na walimu watatu wa Shule ya Msingi *Bay Bridge* kutoka Jijini Dar es Salaam. Karibuni sana. (Makofi)

Pia, tunao viongozi 35 kutoka Jukwaa la *Samialism Malkia wa Amani* na *Malkia Online TV*. Karibuni sana. (Makofi)

Pia, tuna wanafunzi 20 wa Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Idara ya Usimamizi wa Masoko kutoka Jijini Dodoma. Karibuni sana wageni wetu wote katika Bunge letu. (Makofi)

Katibu.

**NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala wetu. Tutaanza na Mheshimiwa Edward Kisau Olelekaita, Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, ajiandae.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa nafasi na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema. Ninawashukuru wananchi wangu wa Kiteto kwa heshima kubwa sana waliyonipa, kurudi Bungeni hapa. Ninawahakikishia nitaendelea kuwa sauti yao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ndiyo iliyotujengea heshima kule majimboni, ndiyo maana Watanzania wale wametuchagua kwa nguvu nyingi sana. Kwa kweli, kwa miradi ya maendeleo iliyofanyika kwa kipindi cha miaka mitano kwa Kiteto tu peke yake ni kazi kubwa sana na kila Mwanakiteto popote alipo akitoka kwenye kata yake, kijiji chake, ataona mradi ambao umejengwa kwa kipindi cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara zake anazozifanya na anasikiliza wananchi sana. Tunamwomba aendelee na nguvu hiyo hiyo ya kuwasikiliza Watanzania hawa. Amekuja Kiteto, leo timu ya matumizi bora ya ardhi iko Kiteto kwa ajili ya vijiji karibu 20 kwa sababu ya ziara yake, lakini vilevile kero za wananchi zimeanza kusikilizwa, karibu kero 300 wakati wa ziara hiyo. Ziara hizi za viongozi wetu ni nzuri sana, zinawagusa Watanzania walio wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Profesa Shemdoe na timu yote ya TAMISEMI. Ninamfahamu Profesa, ni mtu mwema sana, *humble*. Aendelee hivyo hivyo na timu yake yote, na Mawaziri walioko Wizara hii, kwa kweli, wanafanya kazi nzuri. Tunawaombea Mwenyezi Mungu awape nguvu ili waendelee kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wana-Kiteto safari hii wamenituma nizungumzie barabara peke yake. Barabara tu. Jimbo la Kiteto ni kubwa kidogo, ni *square* kilometa karibu 17,000. Ukitoka mwanzo wa Kiteto mpaka mwisho ni karibu kilometa 500, jimbo moja, na wako wakulima na wafugaji wanachapa kazi sana; wanalima vizuri, wanafuga vizuri, lakini miundombinu ya barabara imekuwa tabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mtandao wa barabara. Barabara za *TARURA* ni kilometa 1,291 halafu zenye lami ni kilometa nne tu peke yake. Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja Kiteto alipita kwenye Barabara ya Kongwa – Kiteto – Simanjiro, ambayo ni muhimu sana kwa sababu, kwanza magari karibu 533,995 yanapita kwa mwaka. Ni barabara inayounganisha Mikoa ya Dodoma – Manyara – Arusha na Kilimanjaro. Kwa kuwa, sera yetu ni kuweka kipaumbele kwa barabara hizi ambazo zinaunganisha mikoa na kufungua uchumi, barabara hii haikwepeki, yaani haikwepeki sasa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tu, nitawakera sana kipindi hiki kuhusu barabara. Wananchi wa Kiteto wamenituma, *in fact* wameniambia kila nikipata nafasi hapa nianze kuzungumza kuhusu barabara. Hata nikipata nafasi ya kuuliza swali kwenye Wizara ya Maendeleo ya Jamii, nizungumze barabara hapa. Namna ya ku-

*frame* i-*fit,* hiyo mniachie mimi, lakini kwa kweli, Wanakiteto sasa wanataka barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ilikuwa kwenye mradi ule wa *EPC+F*, tumesaini mikataba hapa, Wanakiteto walikuja. Tuliambiwa kuna shida imetokea kwenye *EPC+F,* tunafahamu, lakini kupitia Wizara ya Ujenzi mlisema kwamba, mmehuisha tena mikataba. Kwa hiyo, kwa kweli, kama mnataka kujenga heshima ya wananchi hawa wa Kiteto, Barabara hii ya Kongwa – Kiteto – Simanjiro – Arusha ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ziara, Mwenyezi Mungu alitusaidia, mvua ikanyesha sana na Waziri Mkuu akapita barabara yote hiyo mpaka Arusha. Mwenyezi Mungu alisaidia naye aone. Kwa hiyo, kwa kweli, umuhimu wa barabara hii ni mkubwa sana. Kwa hiyo, tungependa sana majawabu na Serikali ijipange kuleta fedha, kwa ajili ya barabara hii. Barabara hii ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya kutoka Handeni – Kibirashi – Kiteto inakwenda Chemba mpaka Singida, ni barabara nyingine muhimu inayounganisha Mikoa minne ya Tanga – Manyara – Dodoma mpaka Singida. Ni barabara ya wakulima na wafugaji, ni barabara ya kilimo, barabara ya mifugo, Itafungua sana uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu umuhimu wa bomba la mafuta na Bandari ya Tanga. Barabara hii itakuwa ni muhimu sana na magari karibu mia tano na themanini na ngapi yanapita kwa mwaka. Kwa hiyo, ni barabara muhimu sana. Ni vizuri Serikali ikajipanga kwa kweli, tupate barabara za lami zitakazofungua uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ajira kwa vijana. Tumejenga shule nyingi sana, na ni kitu kizuri sana. Tumetoka kwenye shule za kata, sasa tunakwenda vijijini na vijana wasomi wamekuwa wengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku nilikuwa naangalia kipindi fulani hivi kinaitwa sijui, Watu-*Back Jobs;* kijana mmoja anazungumza anasema, siku hizi *GPA* ambayo tulikuwa tunafahamu kwamba, ni "*Grade Point Average*", siku hizi inaitwa ni "*Gambling People*

*Association*", ile *GPA* kwa sababu ya *frustration,* ambayo vijana wanaipata kwa sababu ya kukosekana kwa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona fedha nyingi hapa, zile shilingi bilioni 200 za Mheshimiwa Rais. Nia ya Mheshimiwa Rais ni kwamba, ifike kwenye majimbo yote, na vijana wengi sana wa Kiteto wameomba hizi fedha. Tunachoomba ni hizi fedha tuone kila kijana ameguswa kutoka kila mahali, siyo kutuletea namba tu kwamba, wameajiriwa vijana kadhaa, hapana. Nchi yetu ni ya ujamaa, ni lazima kazi hizi na fursa zinapojitokeza kila mahali tusikie mkono huu wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kweli, mratibu wote walioomba kwenye sekta hizi. Tunachotamani ni kuona kwamba, kuna Vijana wa Kiteto, Vijana wa Simanjiro, Kilindi, Chemba huko, majirani zangu wote. Tukiwagusa itaendelea kuwapa *courage* vijana kwamba, *yes,* elimu yetu siyo *Gambling People's Association,* ile *GPA. It matters* bado na kwamba, Taifa hili linajali elimu na fursa zipo; lakini lazima tuongeze uwazi katika utekelezaji wa ajira hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwambia Profesa, ni kilometa 1,291 mnatuletea shilingi bilioni mbili tu, haiwezekani. Mtuongezee bajeti kwenye *TARURA, the minimum* ni shilingi bilioni sita. Tungetaka yote, ni shilingi bilioni 11, lakini sisi tunafahamu uchumi wa nchi yetu, angalau sasa ile bajeti itoke shilingi bilioni mbili, twende shilingi bilioni sita angalau, lakini shule za sekondari kidato cha tano na cha sita tunazo mbili tu; Shereta, Maombi, Lesoit, Dongo, Sunya, Dosidosi, Ndedo na Kibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo haimshindi Profesa. Tumeleta maombi kwa ajili ya mabweni, kwa sababu ya mazingira ya shule zetu. Huko kwetu huko mazingira ya shule zetu lazima yawe bora, ili yawe motisha kwa watu wetu kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kazi kubwa sana ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Miaka 50. Hii dira wataalamu wanasema ni "*ambitious*" lakini ni "*achievable.*" Ni *achievable* peke yake tukifanya

mambo kama haya, kwa sababu, sisi kuandika *document* nzuri, tuko vizuri sana na hata baada ya dira kwisha tukiambiwa tuandike, kwa nini hatukufanikiwa? Tutaandika *document* nyingine nzuri sana. Sasa tabu yetu ni utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Mheshimiwa Rais inasema hivi, ili kutimiza Dira ya Maendeleo ya 2050 ni lazima tujenge utamaduni wa utekelezaji na uwajibikaji, kwa hiyo, hapa lazima mchakamchaka uwepo kidogo. Utekelezaji uko kwa Ofisi ya Waziri Mkuu, tukimbizane wazee, tutoke huko sasa kwamba, sisi tunaambiwa tunaandika *document* nzuri, na tusipopata matokeo, tunaandika nyingine nzuri ya kusema kwa nini hatukupata? Hebu twende kwenye utekelezaji sasa, dira ni nzuri, itahitaji nguvu kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tumesema *private sector*. *Private sector* ni 70% tunatarajia, lakini wanachotaka *private sector* ni lazima tu-*expand tax base*, siyo *tax burden.* Watu wachache lazima tufungue *tax* na *informal sector*, lazima waingie, lakini wakati mwingine tunafikiri wawekezaji ni kuomba tu waje nchini. Wawekezaji waliopo nchini, kila mmoja akija hapa anataka aweke kwanza mtaji kidogo halafu jinsi unavyo-*behave* ndiyo ataongeza zaidi na zaidi na hao ndio wanaongea na watu wengine wote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuache zile sheria ambazo ni *unpredictable*, zinabadilikabadilika tu, tuache *bureaucracy*, tuwe ni watu wa vitendo. Tukifanya hivyo, tuta-*attract* hiyo 7%0 ya *private sector*. Baada ya kusema hayo machache, nakushukuru na ninaunga mkono hoja. Ahsanteni sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle. Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, wajiandae.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nami nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetupa afya na uhai wa kuwemo ndani ya Bunge hili siku ya leo na hasa, Bunge la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninaishukuru sana Serikali. Wahenga walisema "Usione vyaelea, vimeundwa." Sisi Wabunge wengi kwenye majimbo na mikoa ambako tunatoka, zipo kazi nyingi zimefanywa na Serikali. Hata Jimbo la Lupembe, kwa mfano, ukienda leo, hali ilivyokuwa miaka mitano iliyopita, Jimbo la Lupembe, leo jimbo zima linawaka umeme vijiji vyote 45.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumepata vitongoji vingine 28, tunaendelea kukamilisha vitongoji vyote kwa ajili ya umeme Jimbo la Lupembe. Hii ni kazi kubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita. Ukienda kwenye elimu, madarasa yamejengwa, ukienda kwenye zahanati vituo vya afya hadi kule Ikondo vimejengwa, ambako havijawahi kujengwa tangu kuumbwa kwa dunia hii. Hii ni kazi nzuri ya Chama cha Mapinduzi. Ninaishukuru sana Serikali kwa kazi ambayo inaifanya, kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa najielekeza kwenye mchango wangu wa siku ya leo, kwenye eneo la Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sehemu ya kwanza ambayo imesemwa na Wabunge wengi ni kuhusu hali ya barabara nchini. Tumeambiwa kwenye hotuba, Wabunge wengi wamesema na mimi naomba kupaza sauti kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Lupembe. Hali ya barabara za nchi yetu hivi sasa siyo nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Lupembe leo hii kwa mfano, Barabara ya Njombe – Lupembe – Madeke mpaka Mlimba kule Morogoro, nimekuwa naisemea ndani ya Bunge hili kila wakati. Sasa hivi yako maeneo yanaleta shida, magari yanakwama, wananchi hawasafiri vizuri na imeahidiwa takribani miaka 20 sasa. Barabara hii ni muhimu kwa sababu, inaunganisha Mkoa wa Njombe na Mkoa wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi wa Mkoa wa Morogoro wanategemea Mkoa wa Njombe kwa ajili ya mbao. Bidhaa za majani ya chai, parachichi na mazao mengine mbalimbali. Tukijenga hii barabara itaweka msukumo wa uwekezaji Lupembe na kufanya

wananchi wengi wapate ajira na viwanda vingi sana kujengwa Lupembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali, umefika wakati sasa tujifunge mkanda tuandae mkakati maalum wa kujenga barabara za nchi hii ili kusudi wananchi wetu waweze kuwa na uhakika wa kusafiri kutoka eneo moja kwenda eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu Barabara za *TARURA*. Hapa nina ushauri maalum kidogo na ninaomba Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Profesa Shemdoe na Manaibu wako mnisikilize vizuri sana kwenye sehemu hii ya *TARURA*. Mheshimiwa Rais alimengea wakati fulani, ukisoma kwenye hotuba ya leo hapa *TARURA* imeongeza bajeti kutoka shilingi bilioni 940 mpaka shilingi trilioni 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni habari njema, lakini lipo tatizo kwenye Barabara za *TARURA,* na hapa ndipo naomba Serikali mnisikilize vizuri. Hizi barabara maeneo mengi tunajenga kila mwaka, barabara hizo hizo. Tunaweka shilingi bilioni moja mwaka huu, shilingi milioni 500 mwakani, mvua ikija inasomba barabara zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wa nchi yetu alitoa maelekezo kwamba, ni muhimu *TARURA* mkatafuta teknolojia ya kujenga hizi barabara zikae kwa muda mrefu, ili kusudi tukijenga mwaka huu barabara mwakani tusirudie tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa, Profesa ninakuomba sana ukae na wataalamu wako mjifunze teknolojia mpya ya kujenga hizi barabara, ili fedha ya walipakodi isipotee kila mwaka kwa sababu, bila kufanya hivyo ni kama kila mwaka fedha ya wananchi inapotea kwa kusombwa na maji kwenye barabara za *TARURA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda Jimbo la Lupembe, Barabara pale Mtwango – Welela kwenda Kichiwa, Barabara pale Itunduma – Ibumila – Ikando kwenda Nyombo haipitiki vizuri kwa sababu, barabara hii mwaka 2025 imejengwa, lakini mwaka huu tena imeharibika. Ukienda kule Njinga kwenda Ikondo, mwaka 2025 imejengwa, mwaka huu tena haipitiki, kwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa sababu, tunajenga barabara za tope bila kuwa na teknolojia nzuri, ili hizo barabara ziweze kukaa kwa muda mrefu. Hili Mheshimiwa Waziri ni muhimu sana mlifanyie kazi, ili kusudi hii fedha iwe na thamani, ili kila mwaka tujenge eneo lingine, kwa ajili ya ufanisi wa barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo wananchi wa Lupembe wamenituma kusema kwa niaba yao, ni kuhusu mikopo ya 10%. Ukisoma kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Serikali imetoa mikopo mingi sana, zaidi ya shilingi bilioni 130 zimetolewa, kwa ajili ya mikopo ya vijana, wanawake na wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliongea wakati fulani hapa ndani ya Bunge, moja ya changamoto kubwa kwenye mikopo hii ya 10% ni hairejeshwi. Ninamshukuru Mungu kwa wananchi wa Mkoa wa Njombe, nimefuatilia Taarifa ya TAMISEMI, Mkoa wa Njombe na Halmashauri ya Njombe *DC* ni kati ya mikoa ambayo wananchi wake wanaongoza kwa kurejesha mikopo ya 10%. Hongereni sana Mkoa wa Njombe. Watu wa Njombe ni waaminifu sana, lakini maeneo mengi mikopo ya 10% hairejeshwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu kubwa ya mikopo kutokurejeshwa, na hapa ndipo naomba kushauri, ni huu utaratibu wa kupeana mikopo kwenye vikundi peke yake, hauwezi kuwa na tija. Inawezekanaje unamchukua mtu mmoja mwenye ujuzi wa biashara unasema aunde kikundi na watu watano au kumi, ambao hawajui mambo ya biashara?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mikopo hiyo wanagawana fedha, wanaenda kutumia, lakini ukimpa mkopo mfanyabiashara mmoja mwenye biashara, anayejua biashara, anaweza kuajiri wenzake 50 mpaka 100 ikawa na tija kubwa. Kwa hiyo, ninaiomba Serikali, sheria hii ya mikopo ya 10% ya mwaka 2024 iletwe Bungeni tuifanyie marekebisho, ili mwananchi mmoja mmoja mwenye wazo zuri la biashara, mtu mwenye biashara yake, apate mkopo urejeshwe kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, tutaendana na Dira yetu ya 2050 ya kusaidia wananchi wetu kuweza kuwa na tija na ajira kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, naomba nichangie kuhusu dawa za kulevya. Tumesoma hapo kwenye Taarifa yetu ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu kwamba, watu wa kudhibiti dawa za kulevya wamefanya kazi nzuri sana nchini. Leo hii nchini dawa za kulevya zimedhibitiwa kwa zaidi ya 80%. Ninatumia nafasi hii kuwapongeza sana *DCEA* na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa udhibiti wa jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwao ni pamoja na mafanikio kwenye dawa za kulevya. Limetokea tatizo lingine, kuna ongezeko kubwa la bidhaa *fake* mitaani. Zipo pombe nyingi *fake* mitaani ambazo watu wetu wanaendelea kunywa na zinaweza kuwa na madhara zaidi kuliko hata *cocaine* na dawa za kulevya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Waziri wa Viwanda, ameanza vizuri, washirikiane na Taasisi ya Kudhibiti Dawa za Kulevya wadhibiti uholela wa pombe haramu, pombe *fake* na bidhaa *fake* ambazo zinaweza kuathiri afya za wananchi wetu kuliko hata dawa za kulevya. Hili ni jambo muhimu sana kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kwa siku ya leo, Wenyeviti wa Vijiji, Vitongoji na Madiwani, wanaiomba Serikali inapoendelea na mipango yake iangalie uwezekano wa kuona namna ya kuwapa posho watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Madiwani, Wabunge pia waliongea wakati fulani hapa, wanakaa vikao siku mbili, siku moja, Waziri Profesa Shemdoe, atoe maelekezo kwa Wakurugenzi kwamba Madiwani wetu wapate muda wa kutosha kukaa vikao kwenye Halmashauri, angalau kwa siku tano hadi siku saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hatuwezi kuwaongezea mishahara, basi wakae vikao muda wa kutosha wajadili vizuri miradi ya maendeleo kwenye halmashauri ili kuwe na tija, lakini pia waweze

kujikimu kama viongozi wetu wa halmashauri. Hali kadhalika kwa vijiji na vitongoji vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo Rais wa Awamu ya Pili, Alhaj Ali Hassan Mwinyi aliwahi kutuasa kwamba maisha haya ni hadithi tu. Akasema: "Ewe ndugu yangu, andika hadithi yako vizuri." Ninataka niwaombe viongozi walioko Serikalini, Mawaziri, tuandike hadithi yetu vizuri kwa kupeleka maendeleo kwa wananchi wetu. Asanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle. Nilimtaja Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ajiandae.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa?

**MWENYEKITI:** Taarifa kwa nani? Hakuna mtu ambaye anazungumza Mheshimiwa.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninataka kumwongezea Mheshimiwa Swalle.

**MWENYEKITI:** Ameshamaliza muda wake. Mheshimiwa Timotheo Mnzava atafuatia na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King na Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Rahim ambaye ametujalia uhai, ametupa uzima na ametuwezesha kuendelea kuwepo kwenye jengo hili kwa ajili ya kuendelea kuifanya kazi ya watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nitumie nafasi hii kwa kuwa ni bajeti ya kwanza tangu Bunge hili la Kumi na Tatu limeanza, niendelee kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na kazi nzuri anayoifanya kwenye nchi yetu. Pia nimpongeze na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania na nimpongeze Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na kazi nzuri anayoifanya kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kwa dhati kabisa kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa kuhudumu chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, ambapo hotuba hii ni hotuba yao Ofisi ya Waziri Mkuu. Mawaziri tunawapongeza sana kwa imani kubwa waliyopata kwa Rais na tunawatakia kila la kheri katika kutimiza majukumu yenu ya kuwatumikia Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unajikita kwenye maeneo mawili tu siku ya leo. Eneo la kwanza nitazungumzia kidogo kuhusu Serikali za mitaa; eneo la pili nitazungumzia usimamizi wa shughuli za Serikali. Nchi yetu miaka ya 90 tuliamua kuanzisha na kutekeleza sera ya ugatuzi wa madaraka. Ili sera hii ifanye kazi vizuri, tukaziboresha na kuziweka vizuri Mamlaka za Serikali kuzishusha kule chini kwa wananchi ili ziwe karibu na wananchi na ziweze kuwahudumia wananchi pia zifanye kazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto kadhaa, lakini sera hii imekuwa na mafanikio makubwa kwa sababu imewashirikisha wananchi katika maamuzi ya shughuli mbalimbali zinazohusu maisha yao na shughuli zao kwa ujumla. Pia, tumeendelea kuisimamia sera hii na kuitekeleza. Tunashukuru hata kwenye dira tuliyoizindua hivi karibuni, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050, tumeonyesha ni namna gani ambavyo Serikali yetu inakusudia kuendelea kupeleka madaraka kule chini kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiiangalia pia bajeti hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo ndiyo bajeti ya kwanza ya utekelezaji wa dira hii tuliyoizindua, kwa mujibu wa taarifa za ukomo tunatarajia bajeti ya mwaka huu itakuwa kwenye shilingi trilioni 62.9. Katika hizi shilingi trilioni 62.9, shilingi trilioni 12.5 zinakwenda Ofisi ya Waziri Mkuu. Katika shilingi trilioni 12.5, shilingi trilioni 12.2 zinakwenda Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba fedha nyingi tunazipeleka TAMISEMI ili zikafanye kazi za kugusa maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu ni mdogo tu kwenye eneo hili, tunapeleka fedha nyingi sana TAMISEMI, tunapeleka fedha nyingi sana halmashauri, lakini lazima tujiulize maswali fedha hizi tunazopeleka tunampelekea nani? Nani mwenye jukumu la usimamizi wa fedha hizi? Wenye jukumu la usimamizi kwa kuwakilisha wananchi kule chini ni viongozi wetu wa vijiji, viongozi wetu wa kwenye kata na Mabaraza yetu ya Madiwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya Mabaraza yetu ya Madiwani ikoje? Hali ya Halmashauri zetu ikoje? Ni ushauri wangu katika kipindi hiki cha miaka hii mitano, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI watengeneze programu nyingine ya maboresho ya Serikali za Mitaa tuziongezee uwezo Halmashauri zetu na Serikali za Mitaa kwa ujumla ziwe na nguvu na uwezo wa kusimamia fedha hizi na ziweze kutoa matokeo kule kwa wananchi wetu ambao tunawaongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo ninataka kulizungumza leo kwenye hotuba hii ya Waziri Mkuu ni eneo mahsusi la usimamizi wa shughuli za Serikali. Kazi ya usimamizi wa shughuli za Serikali ni kazi ya Waziri Mkuu na ni jukumu lake la Kikatiba. Ibara ya 52(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Waziri Mkuu, tumemwona anavyofanya kazi, tumeona ziara anazozifanya na tumeona namna ambavyo wananchi wanamkimbilia. Pamoja na nia nzuri aliyonayo na aliyoanza kuionesha mapema, lazima tukubaliane bado Serikalini kuna ugonjwa. Bado kuna ugonjwa wa kuleana, bado kuna ugonjwa wa kufanya kazi kwa mazoweya na bado kuna ugonjwa wa kuvumilia mambo ambayo hayako sawasawa, pia, kuna ugonjwa wa kutokufanya maamuzi au kuchelewa kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeiona dhamira ya Waziri Mkuu, ni ushauri wangu kwa Waziri Mkuu, aongeze nguvu, aongeze ukali. Tunahitaji tuone wananchi wa nchi hii wanatumikiwa na viongozi wao na wanatumikiwa na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo mawili nitatoa mfano, Serikali ya Awamu ya Sita ilifanya kazi nzuri sana kwenye kufufua kilimo hasa kwenye maeneo ya mazao ya kimkakati. Kilimo cha mazao ya kimkakati. Tumeona Serikali ikifanya kazi kubwa kwenye korosho, tumeona ikifanya kwenye michikichi, imefanya kwenye mkonge na kwenye maeneo mengine. Kwa kweli tunaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita, imeweka alama kubwa sana kwenye eneo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme kazi hii kubwa ya Serikali ya Awamu ya Sita ambayo ilifanyika chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na mtangulizi wa Waziri Mkuu wa sasa, Mheshimiwa Kassim Majaliwa aliifanya vizuri sana, ilirudisha matumaini kwa Watanzania wa nchi hii, hasa wakulima wale wa mazao yale ya kimkakati. Kwa mfano kwenye zao la mkonge, kutokana na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Serikali chini ya ofisi ya Waziri Mkuu, tumeongeza uzalishaji wa mkonge kutoka tani 36,000 mwaka 2020 mpaka tani 73,000 mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi hii nzuri inayofanywa na Serikali kuna mahali tumeanza kupata ulegevu na kuna mahali pameanza kuwa na shida. Tumeanza kuwaruhusu, kuwavumilia na kuwaonea haya wahuni wanaokwenda kucheza na bei za mazao ya wakulima wetu. Leo tunavyozungumza zao la mkonge liko kwenye changamoto kubwa, bei za mkonge zimeporomoka na mkonge umekaa kwenye maghala kwa zaidi ya miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nani anaruhusu watu kucheza na bei za mazao ya wananchi wa nchi hii? Tunaiomba Ofisi ya Waziri Mkuu, jambo hili tusiachie Wizara ya Kilimo peke yake, Ofisi ya Waziri Mkuu iingie ilishughulikie na ilisimamie ili tuendelee kuboresha maisha ya watu wetu na waweze kupata maisha mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nitoe ushauri kwenye maeneo mawili, ushauri wa aina mbili kwenye eneo hili la mkonge. Jambo la kwanza, tunaiomba Serikali ituletee mfumo mzuri na mfumo mpya utakaosimamia kazi ya uuzaji na ununuaji wa zao la mkonge ili kuondoa uwezekano wa watu kucheza na bei kwenye zao la mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais alipokuja katika Mkoa wa Tanga aliahidi kwamba mashine zote za kuchakata mkonge ambazo zilikuwa kwenye Kampuni ya Sisalana ambayo ni kampuni ya Serikali, zitarudishwa kwenye *AMCOS* zetu ili wakulima chini ya Bodi ya Mkonge wakasimamie. Jambo hili limechukua muda mrefu, kampuni inayosimamia mashine hizo mpaka sasa hivi hazifanyi kazi, zimefungwa na wakulima wamekuwa na changamoto ya uchakataji wa zao lao la mkonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ambalo linaonesha ulegevu ni kwenye upande wa zao la chai. Kwa zaidi ya mwaka mmoja wakulima wa Tarafa ya Bungu, Kata Tisa, viwanda viwili vya chai mwekezaji amevifunga ameondoka na wakulima hakuna kazi wanayoifanya. Alipokuja Rais, tumemweleza alitoa maelekezo, alikuja Waziri Mkuu tulimweleza alitoa maelekezo, lakini mpaka leo zaidi ya mwaka mmoja, hakuna kinachoendelea na wananchi hawajui hatima yao ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linahitaji usimamizi madhubuti wa Serikali, tukawakwamue wakulima ili waendelee kufanya shughuli zao wapate kipato, watengeneze uchumi wao, na uchumi wa nchi na maisha yao yaendelee kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava. Nilimtaja Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa na Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso wajiandae.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante. Awali ya yote kwanza ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kutujalia kuwa hai na pia kuwa na afya kutufikisha siku ya leo, kuja kutathmini, lakini pia kupanga matumizi na mipango ambayo tumeipanga kwa ajili ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Waziri Mkuu, ninampongeza kwa maana yangu kwa sababu ninampa hongera lakini ninampa na pole. Hongera kwa sababu ni wa kwanza kusoma hotuba ya bajeti kwa ajili ya kutekeleza Dira ya 2050, kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Muda Mrefu wa Miaka 25, kwa ajili ya kutekeleza Mpango wa Kati wa Miaka Mitano. Hongera na pole, yeye ndiye wa kwanza kutekeleza Mpango wa Muda wa Kati na Mpango wa Muda Mfupi wa Mwaka huu 2026-2027. Ninampongeza pia kwa sababu yeye ndiye wa kwanza kutekeleza bajeti ya mwanzo ambayo ndiyo tunaanza kutekeleza Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kwanza ninanukuu maneno yake ambayo ameyasema katika *paragraph* ya 120 *page* ya 48. Waziri Mkuu amesema kwamba, "Ninaelekeza Wizara ya Fedha iimarishe vyanzo vya upatikanaji wa fedha kwa Mfuko wa Barabara, aidha ihakikishe fedha hizo zinapelekwa moja kwa moja kwenye Mfuko kama ilivyotengwa kwenye bajeti."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila Mbunge anayesimama hapa na Wabunge watatu waliotangulia kusimama kabla yangu, walikuwa wanaelezea barabara, barabara, barabara, barabara! Wabunge wengi waliozungumza wanazungumzia maji, Wabunge wengine walikuwa wanazungumzia umeme vijijini. Umeme vijijini kupitia *ring-fenced fund,* fedha zilizozingirwa imefanya vizuri kwenye umeme, lakini kwenye barabara tunajiuliza kuna kitu gani? Ndiyo maana na mimi nikasema nije na jambo hili nilizungumzie kwa kuwa Wabunge wengi wamezungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya kuweka *ring-fenced fund* ni kwa ajili ya kupata fedha za uhakika kwa ajili ya kutekeleza ahadi za Serikali, ahadi za Chama Cha Mapinduzi na ahadi za Rais. *Ring-fenced fund* hizi leo tumemwona Waziri Mkuu anasimama anatoa *administrative measure* kwamba, anataka kuli-*solve* hili tatizo kiutawala wakati sisi kama Wabunge kupitia Katiba ya Jamhuri ya Muungano Kifungu Na. 63(3)(d) kwamba tunaweza kutunga sheria pale ambapo utekelezaji wa jambo linahitaji kutunga sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasi tulitunga sheria, katika Sheria ya Bajeti, Kifungu Namba 41(2)(1) kwamba, tukiidhinisha matumizi ya *ring-fenced fund* tunasema kwamba ziheshimiwe. Leo Waziri Mkuu anazungumza ametoa mwongozo kwa Serikali, Bunge nalo linatoa mwongozo kwa Serikali, kwa nini sheria tulizozitunga zipo na Wabunge tuko kwa mujibu wa sheria, kwa nini hizi sheria zisifuatwe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema kitu kimoja ambacho ni muhimu sana, ninataka tukazie sasa kwa kuwa Waziri Mkuu amesema fedha hizi moja kwa moja ziende kwenye Mifuko iliyozingirwa, basi tutumie nafasi yetu kama Bunge kisheria tuliweke hili kisheria tuache kutoa miongozo wakati sisi tunaweza kutunga sheria na tunaona athari yake isipotekelezwa mambo hayakai vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninanukuu Ibara ya 135 ya Katiba ambayo iko Sura ya Saba, Sehemu ya Pili, Kifungu cha Pili, kwamba, "Fedha ambazo hazitawekwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ni zile ambazo zimetajwa na sheria, kwamba zitumike kwa shughuli maalum au ziwekwe katika Mifuko mingine kwa ajili ya matumizi maalum."

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha tulizoziweka mwanzo zilikutwa na changamoto na changamoto iliyokuwepo, zilikuwa fedha zinazokusanywa zinakuwa ni nyingi kuliko zinazowasilishwa katika Mifuko. Pili, uwasilishaji ulikuwa unachelewa na fedha haziendi kwa uhakika kwa sababu hii sheria tuliyoweka haikufuatwa vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, matumizi ya fedha hizi yalikuwa yanahitaji lazima yapate idhini ya Mlipaji Mkuu wa Serikali, *Paymaster General* (Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha) na Wizara ya Fedha inapokuwa ina ukwasi wa fedha, hizi fedha haziendi! Ndiyo haya malalamiko tunayoyakuta yako hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi niseme kitu kimoja. Unapoweka *bond,* ukiona kwamba *bond* ile inalegeza unaweka na *washes.* Wakati mwingine kama hata hizi *washes* kwamba kila wakati unabadilisha *washes* zinakuwa nyingi kinachohitajika ubadilishe *bond* uweke nyingine ili ile *bond* iwe ina-*fit* na kile kilichopo pale. Sasa

ninapendekeza kwamba tuweke *bond* ambayo ina-*fit* kutokana na hiki kipengele ambacho tunacho hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna msanii mmoja anaitwa Juma Bhalo amesema: "Ukilegeza kukaza kifundo kinafunguka." Maana kama hujakaza vizuri kifundo kinafunguka. Sasa ninataka tukaze ili kifundo kisifunguke. Ninapendekeza tuweke sheria ambayo itampa mamlaka Kamishna wa *TRA* kupeleka fedha moja kwa moja katika Mifuko iliyozingirwa *(ring-fenced fund)* ili zisipite sehemu nyingine, zikipita sehemu nyingine leo haya malalamiko tumeyasikia hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka juzi tumeanza kujadili bajeti hii nilikuwa ninawasikiliza Wabunge wengi wanaongea jambo hili, ili tuondokane nalo tuondoe hivi vitu kwa sababu kuna jambo moja, tumewekea Mfuko wa Maendeleo ya Barabara, Mfuko wa Barabara ambao kwa Sheria Sura Na. 220 ili kukidhi matengenezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kila Mbunge anazungumza hapa barabara zetu mbovu, tukiwa na barabara mbovu maana yake uchumi wetu hautakwenda vizuri kwa sababu tuna bandari tunategemea usafirishaji, lakini tukaweka *TARURA* kwa sheria hiyo ili tuweze kukidhi kupata barabara hizo, leo Wabunge hapa wanazungumza kuhusu barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninanukuu mtu mmoja anasema: "Siasa ya sasa hivi inaweza ikaja ikahamia kwenye barabara." Kwa hiyo, kwa nini hizi *ring-fenced fund* tusiziwekee sheria ambazo zitatumika kama vile ambavyo Wabunge ambao ndiyo tumekuwa mamlaka ya kutunga sheria tunatakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali tuje na sheria ambayo itasema hizi *ring-fenced fund* moja kwa moja ziende katika Mifuko. Katiba haijakataa, Kifungu 135(2). Sheria tuliyonayo ya Bajeti, Sura 439 Kifungu cha 41(2), ninaona kama kinahitaji *washes,* kila wakati tunatoa miongozo, miongozo lakini tuweke sheria tumeshajua matatizo yetu ni yapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke Ibara ya Nane ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasema: "Serikali inapata mamlaka na madaraka kutoka kwa wananchi." Wajibu wa Serikali itakuwa kazi yake ni kupeleka ustawi kwa wananchi, kama barabara ni mbovu na kama maji hayapatikani, huo ustawi utakuwa ustawi gani? Kwa hiyo, ili twende vizuri tufanye hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatolea mfano hapa mwingine kwa mara ya pili, kwa nini tumefanya vizuri kwenye umeme vijijini? Tulikuwa tuna Mfuko MCC. MCC tulivyozuiliwa tukaja tukatenga fedha zetu hizi ambazo tukaanza kutumia 2015/2016, leo imetusaidia vijiji tumemaliza, tunakwenda kwenye vitongoji. Kwa nini tusiheshimu na huku ili tukapata maendeleo ambayo yanafanana na haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize kitu. Watu wengi sana wanataka wapewe miongozo wakati sheria ipo. *Fabi ayyi hadithim ba'dahu yu'minun,* watu wataamini nini wakati tayari sheria ipo? Wapewe maelezo gani mengine ambayo yako chini au juu ya sheria? Kwa hiyo, *fabi ayyi hadithim ba'dahu yu'minun.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ali Hassan Omar King. Nilimtaja Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa, Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso na Mheshimiwa Fadhili Sandali Chilombe, wajiandae.

**MHE. MASANJA K. KADOGOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuzungumza kwenye Bunge letu Tukufu. Nianze kwa kumshukuru na kumpongeza sana Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri ya kibajeti vilevile ya mwelekeo wa kisera kwa Serikali, niungane naye pia katika kumpongeza Rais kwa kazi nzuri ya kutuletea maendeleo vilevile kuonesha dira ya mwelekeo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninamshukuru Rais kwa kutupatia watendaji wazuri sana katika Mkoa wetu wa Simiyu, Mkuu wa Mkoa ni mweledi wa hali ya juu sana, Mheshimiwa Annamringi Macha, RAS wetu na katika *level* ya Wilaya, Mkuu wetu wa Wilaya,

Mheshimiwa Simon Simalenga na *DED* Ndugu Khalid Mbwana wanafanya kazi nzuri sana ya kumwakilisha Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ningetaka nijielekeze zaidi kwenye kutoa shukrani kwa wananchi wa Wilaya ya Bariadi Vijijini. Wamenituma hapa nitoe shukrani zao za dhati kabisa kutokana na maendeleo tuliyonayo. Kwa upande wa miundombinu ya elimu tunafanya vizuri sana kwenye shule za sekondari na za msingi. Vile vile kwa upande wa miundombinu ya afya, tuna vituo vya afya vinne kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba sera ya Serikali ni kuwa na kituo cha afya kwa kila kata. Tunaamini tumeanza na mwanzo mzuri, tuna vituo vinne sasa hivi ambavyo vimekuwa *registered* na kuna vingine viwili vinajengwa. Tuna zahanati 40, ukiangalia katika kata zetu 21 unaweza ukaona kwamba karibu kila kata ina zahanati mbili. Huu ni mwanzo mzuri. Tunaamini kwamba maendeleo ni hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumefaidika sana vilevile katika hii ahadi ya Mheshimiwa Rais ya siku 100, sisi tulipata wafanyakazi 113, si haba. Kwa upande wa afya wafanyakazi takriban 67, kwa walimu wafanyakazi 27; na tunaishukuru sana TAMISEMI kwa hilo. Vile vile, hata kwa upande wa umeme tumepata vitongoji 85 na kabla ya hapo tulipata vitongoji kama 15, kwa hiyo tuna vitongoji kama 100. Kwa mwanzo huu kwa kweli Ubunge wangu huu mpya unaanza vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili suala la shilingi bilioni 200 pia ambalo limezungumzwa; sisi tunajiandaa kama jimbo ili kuhakikisha kwamba tunafaidika, kwa maana ya kuwasaidia vijana kwenye maandiko. Hiyo kama Mbunge nilikwishajitolea kwamba kwenye maandiko nitahusika moja kwa moja kwa vijana kuhakikisha kwamba tunakuwa na andiko ambalo linaweza kuwa na mashiko ya kupata zile fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bima mpaka sasa hivi ndani ya jimbo letu tumefaidika sana; kwa maana mpaka sasa hivi

tuna kaya 7,011 tayari zimeshapata namba na kupata zile kadi na hili zoezi linaendelea. Kwa hiyo, tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa zoezi hili na ninaamini kwamba linatoa nafuu kubwa sana kwa wananchi. Vilevile, sisi tumekuwa wafaidika wakubwa sana, kwa maana ya ruzuku ya pembejeo, mbolea kwa wakulima wetu na ujenzi wa majosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ni mambo ambayo ni lazima tuyashukuru na kuonyesha kwamba Serikali inafanya kazi kubwa sana. Zipo changamoto ambazo TAMISEMI ni vizuri wakazielewa. Wakipita kule wawe wanajiongeza kidogo kwenda kwenye shule; kuna changamoto kubwa sana ya madawati. Sasa, hili katika *level,* kwa maana ya mkoa, katika *level* ya jimbo tunafanya juhudi zetu, lakini tunahitaji mkono wa Serikali katika hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri kwamba tunapokuwa tunaongeza madarasa nafikiri kuwe na *package*, tusijenge tu darasa bila kufikiria madawati, matundu ya vyoo au vyoo. Ninafikiri tukiwa tunaongeza madarasa, lakini hatufikirii upande mwingine, tunaongeza *crisis*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo ni *very common* na ninajua inawezekana kwa Waheshimiwa Wabunge na wenyewe watakuwa nalo hili. Tunajenga shule hizi ambazo ziko karibu katika mkoa na pengine zimekuja, tumekuwa wafaidika wakubwa sana; shule za wasichana. Ninafikiri takribani shilingi bilioni nne *plus,* lakini unakuta ule ujenzi inajengwa shule ya wasichana lakini haina *fence*. Hili ninafikiri halijakaa vizuri sana. Ninajua si kwetu tu, kwa *research* niliyoifanya takriban shule zote ambazo zimejengwa zinakuwa hazina *fence*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haileti mantiki kuwa na mradi wa bilioni nne halafu ukashindwa kujenga *fence* ya shilingi milioni 100; kitu ambacho kingeweza tu kuwa *negotiated* humo ndani katika ujenzi wakandarasi ambao ni wazawa, wakalifanya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kwamba *speech* hii na Mheshimiwa Mbunge mwenzangu aliyetangulia, inatoa mwelekeo

wa kisera; kwa maana ya bajeti ya kwanza katika utekelezaji wa Dira yetu ya 2050 na ndiyo mwanzo wa kuanza kuendea uchumi wa shilingi trilioni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, hili ni jambo kubwa sana katika Taifa letu, ambalo tumejiwekea shabaha. Ni lazima, hata tunavyofikiria katika utendaji wetu au katika *approach* yetu ya kufikiria namna tunavyoweza kufanya kazi ibadilike. Kwa mfano, kwa upande wa barabara, ninajua sasa hivi kwa ngazi ya mikoa tunaunganisha, tumebakiza sehemu ndogo sana; lakini wakati tunasema tuunganishe wilaya na mkoa ni vizuri vilevile kama Taifa tukajielekeza kufungua zile barabara ambazo zinaunganisha kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sisi watu wa Simiyu, tuna Barabara ambayo imetajwa na Mheshimiwa hapo ambayo inatokea Magu, kwa maana ya Salama – Nguliati – Itilima – Mwandoya – Kisesa – Meatu na kwa ndugu zetu Singida kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Iramba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii barabara siyo tu ni kwa Simiyu, unazungumzia Mara, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Singida na inaenda kuunganisha vile vile na kaskazini. Kwa hiyo, ni barabara muhimu sana. Ninajua kwa upande wa kusini na wenyewe wana barabara zao. Ni muhimu sana tukajielekeza kufungua kanda kwa ajili za kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka nilizungumzie hapa, ambalo limezungumzwa na waheshimiwa wengi, ni hili suala la mafuta. Kwanza, tumshukuru sana Mheshimiwa Spika kwa sababu alilitolea maelekezo siku ya kwanza na ninajua mpaka sasa hivi Serikali inafanya kazi nzuri sana kuona kwamba tunaendaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ninataka kuwakumbusha Watanzania ni jambo moja, suala la mafuta halikuanza leo. Mwaka 1951 – 1954 tulikuwa na *crisis* ya mafuta; kwa wale ambao wanasoma historia. Nilikuwa sielewielewi wakati huo, lakini historia inaonyesha kulikuwa na *Abadan Crisis*, kulikuwa na tatizo

kubwa sana. Mwaka 1973 tulikuwa na *crisis* ya mafuta kwa ajili ya *issue* za *OPEC,* kulikuwa na mgogoro mkubwa sana na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1979 tulikuwa na *crisis* nyingine tena ya mafuta kutokana na *Iranian Revolution*. Mwaka 1990 kwa wale ambao wanafuatilia historia tulikuwa na mambo ya Iraq kuivamia Kuwait, tulikuwa na *crisis* nyingine. Miaka kati ya 2003 – 2008 tulikuwa na *crisis.* Mwaka 2021 – 2023 kulikuwa na *COVID,* baadaye vita ya Ukraine ikaongeza tatizo hilo na sasa hivi tuna tatizo hili la Israel na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, ninachotaka kusema ni nini hapa? *Crisis* ni namna utakavyoichukua lakini inatupa mwanya wa kufikiria tofauti. Kama Taifa ni muhimu sana tukaanza kufikiria kuwa na *reserve* ya mafuta. Mheshimiwa Rais katika hili ameonesha mwanga mzuri sana. Tumejenga *farm tank* pale Dar es Salaam lakini kuna nyingine ziko Mtwara; zile ni kwa ajili ya *storage* lakini kama Taifa ni lazima tuanze kufikiria kwa mawazo tuwe na *reserve* ya mafuta. Tunaweza tukaanza na miezi mitatu, lakini baadaye tukaenda miezi sita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini ni muhimu sana? Tunapoiendea hii dira yetu 2050 *growth* yetu ambayo tume-*project* ni lazima iwe kwenye *10 plus*, maana yake ni kwamba, hatuwezi ku-*afford shocks* za mara kwa mara kwenye uchumi wetu au *100 percent*. *At least* lazima kuji-*cover may be 40%* au *50%*. Kwa hiyo, ni lazima tuwe na *reserve*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili Mheshimiwa Waziri Mkuu atusaidie ku-*coordinate;* kwa sababu tusianze na kufikiria fedha, tuanze na mawazo. Kwa namna yoyote *nature* ya mafuta *obvious* hata *financing* yake itakuwa ni *evolving*, haitakuwa kwamba unaweka fedha pale, zitakuwa zinarudi. Kwa hiyo, kwa maana ya kujumuisha *private sector,* hili litawezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna lingine ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu alilitolea maelekezo; kwamba Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Nishati wakae chini kutafuta *specifications* kwa ajili ya *equipment* zetu

au vyombo vyetu vya Serikali, vianze kuona namna ya kutumia *either gas* au umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maelekezo mazuri sana, lakini ningependa twende zaidi, lazima kama Taifa tujiwekee mpango kwamba, tunaanza pengine usafiri wetu wa *public,* mabasi haya. Pengine ndani ya miaka 10 – 15 tuone *50% 70%* tuanze kutumia *either* gesi au umeme katika mabasi hayo. Hiyo itapelekea kuwa na tatizo kubwa ndani ya nchi inapotokea *crisis*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tuangalie kuanza na Serikali, magari yetu, kwa sababu kama tukipanga hivyo kwa miaka 10 – 15 tuna uwezo mkubwa wa kujenga miundombinu kwenye barabara zetu hizi ili tuanze kutumia umeme na gesi. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba, tunapokuwa na tatizo hili; na kwa *statistics* ambazo nimezitoa, ni *obvious* kwamba *it's another thing coming*. Yaani tatizo hili tutakuwa nalo tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Taifa ni lazima tuangalie namna ya kupunguza ukali. Pengine katika *finding* yake tunaweza tukaangalia; tuna *reserve* sasa hivi ya madini; tunaweza tukaunganisha na hii namna ya ku-*create reserve* ya mafuta kwa kutumia *reserve* yetu ya madini bila hata kuuza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine la mwisho, hili ni vizuri nikalizungumza, ni kuhusu madini. Tuna *GST* na tuna Mamlaka ya Madini. *GST* kazi yao kubwa ni kufanya *research* au kuangalia *indicatives,* kwamba sehemu gani kuna madini, halafu tufanye *exploration* ya ndani zaidi ili kujua yale madini yako kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, kuna shida moja, *GST* ukiangalia iko *less funded*, hawawezi kufanya kazi hiyo, lakini kuna Mamlaka ya Madini ambao wanakusanya zaidi ya trilioni moja kwa mwaka. Sasa, ni suala la kuangalia, kuna mambo mawili ambayo wanaweza wakafanya. Kwanza, wanaweza wakasema kwamba fedha inayokusanywa kiasi Mamlaka ya Madini i-*fund GST* iweze kufanya *exploration* zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kama *GST* inaonekana ni ndogo sana iwe *part, either* iwe ni *subsidiary company* ya mamlaka ya *authority* au iwe *department* ndani ya *authority* ili iweze kuwa *funded*. Kwa sababu mategemeo yetu ya kupata madini zaidi na sasa hivi tunazungumzia 16% tu ndiyo tumefanya utafiti; kwa hiyo bado tuna *potential* kubwa sana. Sasa, tusipoi-*fund GST* maana yake hatuwezi kufika huko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo ninataka kuzungumzia, Mheshimiwa Mavunde nimemfahamu kwa muda kidogo. Bahati nzuri sana Mheshimiwa Mavunde amekuwa *advocate* mkubwa wa wachimbaji wadogo wadogo. Miaka 15 iliyopita nilikuwa Mkurugenzi Benki, walikuja kufuatilia anawatafutia wachimba madini wadogo wadogo fedha. Kwa hiyo, ni mtu ambaye ni sahihi katika sekta hii kwa sababu amei-*view* miaka mingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningeweza kuomba watu wa madini watusaidie na *especially* sisi watu wa vijijini; wanapokuta watu wa vijijini, wananchi wamegundua *either* kwa kupiga ramli au kwa namna nyingine yoyote ile, wako 1,000 au 2,000 wasiwaondoe; wawafanyie utaratibu ili wawe wachimbaji pale. Serikali kwa sababu wana *muscles,* wakatafute *exploration* sehemu zingine, kwa sababu hii inatuletea kelele kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza hayo ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana kwa kunivumilia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Masanja Kungu Kadogosa. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mheshimiwa Fadhili Sandali Chilombe na Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando wajiandae.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuwa mchangiaji wa hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kuleta maendeleo; na sisi watu wa Mkoa wa Katavi tumenufaika sana baada ya fedha nyingi zilizoletwa kwenye mkoa wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee, kwenye halmashauri yangu tu tumepata shilingi bilioni 558 ambazo zimekwenda kutekeleza miradi mbalimbali, ikiwemo ya Sekta ya Elimu, Afya, Kilimo na nyinginezo. Tunamshukruu sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa ambayo anaifanya ya kusukuma maendeleo. Ziara ambazo anazifanya zina mafanikio makubwa sana ndani ya nchi yetu, tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nijikite sana kwenye suala la miundombinu. Tumebahatika kupata mvua nyingi kwenye nchi yetu ambayo kimsingi imekuja kuharibu suala la miundombinu ya barabara za vijijini, mijini na barabara kuu. Eneo hili tunahitaji kupata fedha za kutosha ili tuweze kukarabati miundombinu iliyokufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bajeti tulizonazo za *TARURA* za barabara kuu, hazitaweza kumudu kukarabati barabara ambazo zimeharibika. Nina ushauri kwa Serikali; ninaomba sisi Wabunge tuchukue dhamana zetu kwa ajili ya kuisaidia nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumsaidia Mheshimiwa Rais ni pamoja na kubuni vyanzo vipya vya mapato ambavyo tutaishauri Serikali kuweza kwenda kuvifanyia kazi. Ninaamini kuwa Serikali ikikubali mawazo ya Waheshimiwa Wabunge tunaweza tukatoka mahali ambapo kwa sasa tupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri, kama tukikubaliana, la kwanza, Serikali iendelee kudhibiti Mfuko wa Barabara ambao tumekuwa tukichangia kupitia tozo mbalimbali. Ile Mifuko ambayo imewekewa *ring fence* lazima iheshimiwe. Tunaomba tuweze kuanzisha chanzo kipya cha mapato. Tukianzisha kwenye Mfuko wa Mawasiliano ambao utakwenda kusaidia kupata fedha za kukarabati miundombinu iliyoharibika, tuna nafasi ya kuweza kwenda kukarabati barabara zilizoharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kuwa wataalam wetu wakikubali tunaweza tukapata fedha takriban shilingi trilioni moja kwa shilingi mia moja tu, ambayo tukikubaliana tuiweke kwenye muda wa maongezi inaweza kwenda kusaidia kupunguza tatizo tulilonalo kwa sasa la uharibifu wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi trilioni moja ikipatikana igawanywe iende kwenye barabara za *TANROADS* na iende kwenye zile barabara zinazomilikiwa na *TARURA*. Itatusaidia sana kutatua kero ambayo ipo takriban kila mkoa, takriban kila wilaya na kwenye vijiji na kata zetu ambazo zimeathirika sana baada ya mvua nyingi zilizonyesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa yetu ya Kigoma, Rukwa na Katavi ni mikoa ambayo inapata mvua nyingi sana. Mvua zilipozidi sisi Mikoa ya Katavi na Kigoma ilijifunga kwa sababu madaraja yaliathirika kwa kiwango kikubwa sana. Ninaomba hili tulifanyie kazi; na sisi Wabunge tuchukue dhamana zetu kwa kuishauri Serikali tuisimamie ili waweze kupata fedha ambazo zitaenda kukarabati miundombinu ya barabara zilizoharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ninapenda kuipongeza Serikali ni kwenye suala la uvuvi haramu kwenye Ziwa Tanganyika. Ninaipongeza Serikali wameanza juhudi za kwenda kutafuta nyavu zile ambazo zina uharibifu mkubwa kwenye eneo la Ziwa Tanganyika. Maisha ya wananchi wa Mkoa wa Kigoma, maisha ya wananchi wa Mkoa wa Katavi na Rukwa wanaoishi pembezoni na Ziwa Tanganyika yanategemea shughuli za uvuvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ambalo lipo ni wananchi wanaovua kwa kutumia nyavu zile ambazo zimepigwa marufuku. Zipo nyavu maarufu zinazoitwa *filimayaya* ambazo asili yake zinatoka Nchi ya Burundi, Congo na Rwanda; ndiyo wanaoziingiza zile nyavu na zile nyavu zinahatarisha maisha yote ya viumbe hai vilivyopo kwenye Ziwa Tanganyika. Hata yale ambayo Mheshimiwa Chipando, Mbunge wa Kigoma alikuwa anayazungumzia wala si ya uongo, ni ya kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maisha ya Watanzania wa ukanda wa ziwa yanategemea uvuvi. Niiombe Serikali, juhudi ambazo imeanzisha kwa sasa za kupiga marufuku na kufanya ile *operation* inayofanyika kwa sasa ndizo zifanyiwe kazi kuliko yale mawazo ya kufunga ziwa. Unapofunga ziwa hujapata suluhu, suluhu ni kwenda kufanya *operations* ambazo zitawafanya wale wamiliki waweze kuacha uvuvi haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua tu iliyofanyika juzi, *operation* ambayo imefanywa ndani ya Mkoa wa Kigoma na mpakani mwa Mkoa wa Katavi imewafanya wale wavuvi haramu na wengi wao ni watu wanaotoka *DRC Congo* na wanaotoka Burundi wamekimbia. Wengine wanasubiri sasa hali itakapokuwa imepoa warudi tena kwenye yale maeneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali, katika hiki kipindi ndipo ambapo wafanye *operation* ya bila kikomo ili kutoa tatizo la uvuvi haramu. Suala la kufunga Ziwa, sisi ndiyo tunaowanyanyasa wananchi wetu. Burundi hawafungi Ziwa na Congo hawafungi Ziwa; tunaofunga ni sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, samaki hawana mipaka. Inapokuwa huku kumekuwa na hali ya unafuu, wale Wakongo ndiyo wanaokuja kuvuna rasilimali ambazo tumejiwekea sisi wenyewe. Ninaomba hili wakalifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia kwenye eneo la miradi iliyoletwa na Serikali. Mkoani kwangu nimepokea fedha za maendeleo, nimepata fedha za kujenga kituo cha afya, tumepata fedha za kujenga zahanati na miradi ya elimu. Tatizo lililopo kwenye Ofisi ya TAMISEMI, vibali kwa ajili ya miradi hiyo kufanyika hawatoi. Wanapeleka fedha, zinafika zinakaa. matokeo yake zile fedha zitatolewa kipindi cha mwishoni. Unapoziruhusu mwezi Mei, haziwezi kufanya kazi, mwezi Juni mwishoni zinarudi tena Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali waharakishe kutoa vibali ili waweze kufanya ile miradi ikamilike kwa sababu malengo

ambayo wameyafanya ni kwenda kutekeleza ile miradi ya maendeleo. Hili ni la muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia kwa kuishauri Serikali kwenye eneo la hewa ukaa. Serikali tumekuwa tukiishauri mara kwa mara, kwenye eneo hili lazima tuweke mkakati wa uvunaji wa hewa ukaa ili tuweze kupata fedha za ziada ambazo zitaisaidia Serikali kwenye miradi ya maendeleo. Kwa bahati mbaya sana kumekuwa na urasimu mkubwa sana kwenye eneo hili. Mkoani kwangu tuna msitu ambao umekaa zaidi ya miaka mitatu, tunataka uwekezaji uwekezwe lakini maamuzi ya kutoka Serikalini yanachukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hili walifanyie kazi watoe ule urasimu ambao unafanyika, waondoe vikwazo ili watu waweze kupata haki na stahiki za kwao. Tuna misitu mingi ambayo ipo kwenye halmashauri ikiwemo misitu inayomilikiwa na *TANAPA*. Huko wakiweka sheria ambazo zinaweza zikaruhusu uvunaji, Taifa litapata fedha nyingi na wanapata chanzo kipya cha mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Selemani Kakoso. Nilimtaja Mheshimiwa Fadhili Sandali Chilombe, Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli wajiandae.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba iliyo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi ambazo ameendelea kuzifanya, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamesema. Kila mtu anaona nini kinaendelea ndani ya hii nchi. Kwa hiyo, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi anazoendelea kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kujielekeza kwenye changamoto ya barabara. Tatizo la barabara ni kubwa na limesemwa, kila Mheshimiwa Mbunge anayesimama hapa ataongelea *the same*. Hata hivyo, ninaipongeza Serikali kwenye *angle* hiyo kwamba kabla sijaingia Bungeni nilikuwa ninasikia watu wanasema bwana Bajeti ya *TARURA* ni ndogo iongezwe na mwaka huu Serikali imefanya uamuzi wa kizalendo, imeongeza bajeti. Hii ni safari nzuri yenye mwelekeo mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja pongezi hizo, ninaomba kushauri mambo yafuatayo:- Kuna shida kubwa sana Serikalini, sijaingia Bungeni na hapa kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakiyasema hayo mambo. Moja kati ya shida kubwa ni kwamba Serikali inapanga bajeti, ikishapanga ile bajeti, fedha inayofika sasa kwenye utekelezaji wa hiyo bajeti ni ndogo. Sasa ukiangalia tatizo la *TARURA* lilivyo halafu ukaipelekea hela ndogo, shida kwa kweli zinaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaishauri Serikali, ninajua ina vipaumbele vingi, inatakiwa ifanye kazi nyingi kila kitu kinafanywa na Serikali, lakini moja kati ya vipaumbele vikubwa ambavyo Serikali inatakiwa kuvifanyia kazi, ni kupeleka fedha kwenye barabara za *TARURA*. Kwa kufanya hivyo ninaamini changamoto zitapungua kwa kiwango chake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu wa pili, Serikali iongeze usimamizi wa kazi za *TARURA*. Ziko baadhi ya sehemu katika nchi hii, kazi zinazofanywa na *TARURA* siyo nzuri, haziko kwenye viwango. Kuna maeneo ukienda leo unakuta daraja limejengwa halina nondo kabisa. Matokeo yake ni nini? Yapo maeneo daraja moja limejengwa, *in a span of less than 10 years* limejengwa mara mbili. Sasa unaweza ukajiuliza kwamba fedha inayopelekwa ni ndogo, halafu tunajikuta tunaenda kujenga palepale kwa sababu kwenye eneo hilo hiyo barabara ni muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawajengi kwa kiwango, madhara yanayotokea ni nini? Ukiangalia maeneo mengi ya nchi, utakuta kwamba ziko barabara kila mwaka zenyewe ndiyo huwa zinapitiwa.

Barabara zingine haziguswi, kwa sababu gani, kiwango cha fedha ni kidogo na pale wanapojenga hawajengi katika kiwango kinachotakiwa. Kwa hiyo ninaishauri Serikali iongeze usimamizi kwenye barabara za *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine, alisema juzi hapa Mheshimiwa Naibu Waziri wakati anajibu swali, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, alisema hivi, "Mtandao wa barabara za *TARURA* nchi hii upo kilometa 144,429.77". Ukienda kuangalia taarifa, hiyo maana yake ni kwamba ukubwa huo wa barabara ni sawasawa, hao watu wa *TANROADS* wana kilometa 37,435.04, hii ni 25% tu ya barabara ambazo *TARURA* wanazihudumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye huu mtandao wa kilometa 144,000, ni kilometa 3,053 tu ndiyo zenye lami, hizo za *TARURA*, kilometa 3,053 pekee ndiyo zenye lami. Ukiangalia, kiwango hicho cha barabara ni zile ambazo ziko mijini, maana yake ni kwamba maeneo mengi ya vijiji hayana lami kabisa. Kwenye jimbo langu hakuna lami hata sentimita moja. Sasa hiyo naamini siyo Tunduru Kusini peke yake, maeneo mengi yapo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, Waheshimiwa Wabunge wamesema hapa, kumbe kuna Mifuko ilishaanzishwa kwa ajili ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kwenda kujenga hizo barabara. Ninaomba Serikali sasa ianzishe mkakati kwamba pamoja na hiki kilichofanyika sasa, kizuri, chema cha kuongeza bajeti, ninaomba hii iwe *routine* kila mwaka tuwe tunaongeza bajeti angalau kidogokidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu leo hii tunavyoongea kuna hizo kilometa nilizozitaja hapo, lakini mwakani tukifika hapa, barabara za *TARURA* zinazidi kuongezeka. Jimboni kwangu, juzi hapa niliuliza swali, ninahitaji kupasua barabara 20. Maana yake ukubwa huu ambao sasa hivi *TARURA* wana umiliki, mwakani siyo hivi na maeneo mengine yako hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi wenyewe mashahidi, katika kila eneo la mtu anapotoka hapa, kuna vile vitu vinaitwa vitongoji,

vimekuwa vinatakiwa vipandishwe hadhi viwe vijiji, barabara zitapasuliwa maana yake *TARURA* inazidi kuongezewa eneo lake. Kwa hiyo ninashauri kwamba Serikali itengeneze mkakati wa kuhakikisha kwamba huu uongezaji wa hela, kila mwaka ziongezeke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye hilo, zile barabara zinaongezeka, 60% ya watu nchi hii wanakaa vijijini na uzalishaji wote tunaoutegemea kwenye uendeshaji wa nchi kwa maana ya chakula na mambo mengine, unatokea vijijini. Ninaishauri Serikali pia ianze kutengeneza mkakati wa kuhakikisha kwamba kila mwaka, kila jimbo linapata angalau kilometa tano za lami. Tukianza safari hiyo tutafika, vinginevyo watajikuta wanatengeneza mijini tu, vijijini huku hakuguswi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili, ninatoka Tunduru, kwa ulinganifu Wilaya ya Tunduru ina *square kilometer* za mraba zile ziko 18,776, nikilinganisha na Mkoa wa Mtwara, una kilometa za mraba 16,707. Wilaya ya Tunduru ina halmashauri hii moja wakati tunawazidi Mkoa wa Mtwara kwa zaidi ya *square kilometer* 2,000. Mtwara wana halmashauri tisa, nimeweka hiyo kama ulinganifu. Vilevile, Mkoa wa Ruvuma ninaotokea mimi una halmashauri nane, kuna watu 1,981,884 katika mkoa huo, kati ya hao wananchi 400,000 wa Mkoa wa Ruvuma wanatokea Tunduru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni nini? watu 1,500,000 *plus* wanatokea kwenye zile halmashauri saba ambazo ukigawa unapata wastani wa watu 224,000. Ninalenga kusema nini? Ninaiomba Serikali, tumeshaleta hili ombi mara nyingi ile halmashauri igawanywe ni kubwa mno. Hapa panakuwa hapana ulinganifu, kwenye mkoa tu wenyewe, sisi tupo watu 400,000, halmashauri nyingine zina watu 200,000 *plus*, eneo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaiomba Serikali, Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakuja ku-*wind up*, wananchi kule wanataka kusikia nini kauli ya Serikali kwenye kipande hiki? Ninaomba sana Serikali kwenye *angle* hiyo watusaidie, Tunduru, hili Bunge lisiishe lazima tuwe na halmashauri nyingine kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho wakati ninaelekea kumaliza mchango wangu, ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. Watu wamempongeza na mimi ninasema tu, wakati ule anateuliwa hapa, Hayati Lukuvi alipewa nafasi ya kusema, alisema kumhusu Mheshimiwa Waziri Mkuu. Yaliongelewa maneno, nikawa nahisi kwamba mbona kama kuna chumvi inaongezwa, lakini baada ya kuwa ameanza kazi, ninaona zile sifa zilikuwa chache, anastahili zaidi. Anafanya kazi na kwa kweli anatupeleka kwenye dira iliyo njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwake, aende na atengeneze *mechanism* ya kufuatilia kwa sababu sasa anapotoka huku nyuma mambo yanakuwa *business as usual*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi zangu nyingine, ninaomba kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa, Mheshimiwa Brigedia Mohamed Abbas pamoja na Katibu Tawala wake anaitwa Mama Mary Makondo. Mkoa wa Ruvuma ni mkubwa, lakini mkoa ule umetulia sana, ametoka kusema mtu mmoja hapa "Ukiona vinaelea, vimeundwa". Ukimya ule siyo wa hivi hivi, yako mambo yanatokea kule, lakini wale watu wanayamaliza, lazima tuwape sifa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mkuu wa Wilaya ya Tunduru. Wilaya ni kubwa nimetoka kusema hapa, lakini imetulia ni kwa sababu wao wanafanya kazi. Kipekee, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru, anapambana mno. Kuna watu wana halmashauri ndogo, lakini kwenye utendaji Halmashauri ya Tunduru ni kati ya zile ambazo zinafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakupongeza wewe, ninampongeza Mheshimiwa Spika kwa sababu moja tu, hapa ndani sisi ni wageni lakini mnatupa nafasi tunaongea. Ninawashukuru na ninawapongeza kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsanteni kwa kunisikiliza.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Fadhili Sandali Chilombe. Nilimtaja Mheshimiwa Salehe Mbwana Mhando na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli na Mheshimiwa Cecilia Paresso wajiandae.

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuwa miongoni mwa wachangiaji wa Hotuba ya Makadirio ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Ninaomba kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali kusimama katika Bunge lako Tukufu kuchangia hotuba hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pongezi kwa viongozi wetu Wakuu wa Nchi yetu wakiongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sambamba na Mheshimiwa Makamu wa Rais na pia Mheshimiwa Waziri Mkuu wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, itoshe tu kusema, "Kusema sana si hoja, kutenda ndiyo hoja", hii ndiyo dhima ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunashuhudia namna siku 100 tu katika awamu hii ya pili ya kipindi chake cha pili anachomaliza, ahadi alizozitoa na utekelezaji wake huhitaji hata kutafuta kwa tochi. Unaona kwa vitendo na kwa matokeo na haya ndiyo ambayo Watanzania wanampenda na wanamtumainia sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa na mimi kujielekeza kwenye kuchangia hoja ya Hotuba ya Waziri Mkuu. Katika kuchangia hoja hii, mimi nimejipa muda mwingi sana wa kupitia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini ikiongozwa na dhima ile ya Dira ya Maendeleo ya Taifa letu ya 2050 ambayo Bunge hili na bajeti hii ambayo tunaanza kuijadili leo, inatuanzishia safari hiyo chini ya Mpango wa Nne wa 2026/2027 na 2030/2031 yenye maudhui yanayosema: "Mageuzi katika kukuza uchumi na kuzalisha ajira."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutafsiri dhima hii ya mageuzi katika kukuza uchumi, moja kwa moja kwa mawazo yangu na kwa

fikra zangu, nimeyatafsiri maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miaka mitano iliyopita. Huu ni mwendelezo, kazi ilishaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, ninataka kufungamanisha, kwa mfano tu, mageuzi makubwa yaliyofanyika katika uwekezaji wa bandari zetu, Bandari ya Tanga, Bandari ya Dar es Salaam na Bandari ya Mtwara, tayari ni safari ambayo imeanzishwa katika kutekeleza Mpango huu wa Nne wa Dira ya Maendeleo wa 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mageuzi yale yaliyofanywa ndiyo yanayokuja kuunganishwa na jambo linalozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi humu ndani. Mapinduzi makubwa ya bandari na mimi kama Mheshimiwa Mbunge ninayewakilisha wananchi wa Jimbo la Kilindi kutoka Mkoa wa Tanga na Tanga tuliguswa na uwekezaji mkubwa wa zaidi ya shilingi 400,000,000,000 kwenye uwekezaji wa Bandari ya Tanga ambayo sasa inatoa matokeo makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema, kiunganishi kikubwa katika zoezi hili, hatua hii ni uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu ya barabara. Pengine niseme tulichelewa, ilibidi wakati ule hatua ya uwekezaji kwenye bandari ilitakiwa iende sambamba na uwekezaji mkubwa kwenye barabara zetu hasa hizi za *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuzungumzia Barabara ya kimkakati ambayo inaanzisha kuunganisha Bandari ya Tanga kutoka Tanga – Segera, Segera – Korogwe, Korogwe – Handeni na hatimaye kutoka Handeni – Kibirashi - Kiteto – Chemba – Kwa Mtoro, Singida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii korido ambayo ilikuwa inatakiwa ipokee makontena, mizigo kwa njia rahisi kabisa, ilitakiwa iwe hii Barabara ya lami ambayo kipande chake kilichobaki ni kutoka Handeni – Kibirashi – Kiteto – Chemba – Kwa Mtoro. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa ziara aliyofanya katika Jimbo letu la Kilindi na akajionea kwa macho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alishaanzisha kwa maono hayo akiwa anaangalia uwekezaji mkubwa wa bandari, akaanzisha ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha lami kutoka Handeni – Kibirashi – Chemba na akaanza na kilometa 20 mwaka 2023 kutoka Handeni – Mafuleta, hatimaye akaagiza tena zijengwe kilometa 30 kutoka pale Mafuleta kwenda Kileguru kilometa 30, jumla ni kilometa 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Serikali, twende tukatekeleze maono haya ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tumechelewa, hivi tunavyozungumza, katika zile kilometa 20, kilometa 10 tu zimekamilika kwa miaka minne. Ninaomba sana, katika kutafsiri mageuzi katika kukuza uchumi, barabara hii ni ya muhimu, ni ya kimkakati na katika bajeti hii inayoanza katika kutekeleza Dira ya 2050 na huu Mpango wa Nne wa dira hii. Hii barabara iwe kipaumbele katika mipango yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inaondoa sasa hivi mizigo inayoshuka Bandari ya Tanga inalazimika tena kurudishwa Dar es Salaam kwenye mizigo mingi inayopokelewa kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Huu ni mgogoro, lakini njia rahisi ambayo ilikuwa tungekuwa tumeanza mapema na sasa hivi hatujachelewa, tukiamua tunaweza tukaenda kwa *speed,* tukaitoa Barabara ile mpaka Kibirashi, Kibirashi ikaendelea kwenda Kiteto, Kiteto kwenda Chemba kule Kwa Mtoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pale Singida ianzishwe Bandari ya Kwala namba mbili, ipokee mizigo pale iingie kwenye *SGR*, iendelee na safari kwenda mikoa mbalimbali na nje ya nchi kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na barabara hii kwa kiwango cha lami kwa Wanakilindi bado tuna uhitaji na hii wilaya ina changamoto kubwa sana za barabara hizi hizi za *TANROADS* kutoka pale Songe kwenda Gairo, lakini kutoka Songe kwenda kwa Lugulu, barabara hizi hazipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ushauri twende na mipango na kazi zinazotoa matokeo, tutoke sasa kwenye barabara kujengwa kwa kiwango cha tope, tuwe na mpango madhubuti wa kila mwaka kwamba hizi barabara zifanyiwe matengenezo kwa kiwango cha moram au changarawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua inayoendelea sasa hivi ya *surface grading* unaondoa hata ile changarawe ya mwaka juzi, mwaka jana unaleta tope, unajaza mvua inakuja tunarudi palepale, fedha za umma zinapotea na matokeo hayaonekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani nione tuje na mpango kwa *TANROADS* tuseme sasa matengenezo ya kawaida yawe kwa kiwango cha changarawe, tuone ma-*tipper* yanamwaga changarawe kipindi ambacho tunatengeneza barabara ili ziweze kupitika mwaka mzima, lakini huu mpango wa *surface grading* tunapoteza fedha, hakuna matokeo na mwisho wa siku tunazorotesha uchumi wa wananchi wetu na uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la *TARURA*, Jimbo la Kilindi lina mtandao wa barabara za *TARURA* kilometa 1,520. Bajeti ya *TARURA* bilioni 2.5, jiografia ya Kilindi ni ya milima na makorongo mapana. Mimi nina madaraja nane, Daraja la Lukole, Tamota, Sambu unakwenda pale Gombero, unakwenda kule Saunyi, unakuja hapa Vunila, barabara moja limefanyiwa usanifu ni bilioni 4.3 wastani, unapokea bilioni 2.5!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza kata nne zimejifunga hazifikiki; Kata za Kilwa, Lwande, Hagwi, Saunyi na changamoto yake ni madaraja. Sasa niulize kwa bajeti ya bilioni 2.5 hiki kitendawili kinakwenda kuteguliwa vipi? Kwa hiyo, ninaunga na Wabunge wenzangu wote, tuhakikishe kwamba *TARURA* inaongezewa na bajeti na tufanye zoezi, sasa hivi tunakwenda ku-*phase out REA,* ule mpango wa *REA* na usimamizi wake urudi kwenye barabara za *TARURA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa eneo la barabara ninaomba niishie hapo, ninaomba sana tuchukue juhudi na tuamue, kupanga ni kuchagua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ninaomba niingie kuhusu migogoro ya ardhi ya wakulima na wafugaji. Ukurasa wa 27 umeeleza vizuri sana. Hili ninataka niwaambie miongoni mwa Wilaya zenye changamoto kubwa na Kilindi imo, lazima tukubali tatizo na ili uweze kutatua tatizo ni lazima utambue kwamba nina tatizo na hili tatizo ninaamini ni la nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ninataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Mwenyekiti wa Bunge na Serikali, migogoro ya wakulima na wafugaji, lipo tatizo la msingi, lakini tu hatutaki kuli-*address*. Wapo wafugaji wakorofi wachache ambao wao wanaleta matatizo kwa ukorofi wao, lakini hiyo siyo hoja ya msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ni kwamba sisi tuna mifugo, tuna watu wanaojishughulisha na shughuli za ufugaji, hizi ni shughuli za kiuchumi lakini hakuna sehemu za malisho. Wote tunatoka kijijini hapa, asimame mtu aseme mifugo yetu kwenye kijiji chetu inalishiwa sehemu fulani, asimame hakuna. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha hapa tuna mifugo milioni 76, mifugo maeneo rasmi ya malisho hayapo nini kinatokea? Mifugo inahudumiwa kwenye maeneo yenye matumizi mengine kama ya kilimo hifadhi na kadhalika. Sasa utakwepaje migogoro hiyo kama hali ndivyo ilivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niiombe Serikali hili jambo ni kubwa, ni mtambuka, linahitaji kukaliwa chini kufanya tafakari. Leo hata kule kwenye matumizi yaliyotengwa matumizi bora ya ardhi, kwenye maandishi utaona kumetengwa maeneo ya mifugo, kwenye uhalisia kule hakuna huo ndiyo ukweli. Kwa hiyo, lazima tukakae tutafute ufumbuzi wa eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukienda kwa Afisa Mifugo atakupa takwimu ya mifugo na ni kweli kwenye kata hiyo mifugo ndiyo hiyo, ukienda atakupa idadi ya majosho na ukienda utayaona, ukienda atakupa idadi ya minada na ukienda utaiona, nenda kamwambie nipeleke kwenye malisho ya mifugo, hutapata jibu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salehe…

**MHE. SALEHE M. MHANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe wito au nitoe ushauri kwa Serikali, Wizara husika TAMISEMI, Ardhi, Mifugo tukae tutafakari huu uchumi, lazima hii shughuli iwe na maeneo rasmi ya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Salehe Mhando.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamtaja mchangiaji anayefuata ninaomba niwatangaze wageni ambao wapo Bungeni muda huu.

Tuna wageni 37 wa Mheshimiwa Paul Christian Makonda, Mbunge ambaye ni Waziri wetu wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Wageni hao ni washindani wa nafasi ya Mwakilishi wa Tanzania katika Mashindano ya *Miss World* 2026 Nchini Vietnam na wameongozwa na watendaji wa Wizara, karibuni sana washindani wetu ninawaombea kila la kheri kwenye mashindano yenu, lakini pia mshindi ambaye atakwenda Vietnam basi arudi na ushindi Tanzania karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa Rebeca Sanga ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nipende kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kuweza kunipa nafasi ili

niweze kuchangia mchango wangu kwenye Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika Nchi yetu ya Tanzania kuhakikisha kwamba tunapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, nimshukuru Makamu wa Rais na viongozi wote wa Serikali ambao wanafanya kazi kwa juhudi kubwa kuhakikisha kwamba sisi Watanzania tunaendelea kuwa salama, lakini pia tunapata maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru mambo yaliyofanyika katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam, Wilaya ya Ilala tumefanya mambo makubwa kipindi kilichopita tumejenga shule nyingi kwenye sekta ya elimu ambayo shule za mfano. Ukiangalia katika Wilaya ya Ilala tuna shule nyingi ambazo ni shule za kisasa na shule zenye lifti na shule ambazo zinawafanya watoto wetu ili waweze kukaa katika mazingira salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo nichukue sasa nafasi hii kutoa mchango wangu kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kama tunavyojua kwamba nchi yetu ina ugeni 2027 kwa ajili ya Mashindano ya *AFCON,* lakini watu wote tunajua kwamba Mkoa wetu wa Dar es Salaam kwa hali ulionao kwa sasa miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam imeharibika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi tumeona mvua imenyesha kubwa barabara nyingi ambazo zinaweza kupitisha magari zilikuwa zimefungwa. Pia ukichangia na ujenzi ambao unaendelea wa miundombinu katika Mkoa wa Dar es Salaam hali ni mbaya sana. kwa hiyo, ninaiomba Serikali au ninashauri kwamba Mkoa wetu wa Dar es Salaam haiwezekani ukapangiwa mpango kama mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mkoa wetu wa Dar es Salaam ukiangalia watu ambao wanaishi katika Mkoa wa Dar es Salaam ni watu wengi. Kwa sasa hivi siyo ajabu ukakaa kwenye foleni masaa mawili mpaka matatu, sasa nikiangalia tunakwenda kupata wageni 2027 na ujenzi wa barabara zetu au miundombinu ya barabara zetu

za Mkoa wa Dar es Salaam, barabara moja meta 300 au meta 500 inajengwa kwa mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba Serikali ije na mpango wa kuhakikisha kwamba tunapokwenda kwenye hii fursa ambayo tumeipata ambayo ni ya kiuchumi, ya kijamii pamoja na kidiplomasia kwamba sisi Mkoa wa Dar es Salaam tunakwenda kuonekana kwamba tuko vizuri, lakini pia tunakwenda kuitangaza nchi yetu kwa kuonekana kwamba ina miundombinu mizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Mkoa wa Dar es Salaam mindombinu yake ni mibovu sana. Pia ucheleweshwaji wa wakandarasi wetu, mkandarasi anaanza kutengeneza barabara. Tuna barabara ambazo zimeanza kutengezwa 2019/2020 mpaka leo hazijamalizika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongelea Barabara ya Kinyerezi – Bonyokwa – Kibamba ambayo inakwenda mpaka Jimbo la Ubungo. Hii barabara ni barabara ya kilometa 6.3, tangu imeanza kujengwa 2020 mpaka leo haijawahi kumalizika. Hii barabara ni barabara ambayo wananchi wako karibu na barabara. Kwa hiyo, wananchi wameweza kutoa sehemu zao za nyumba zao ili barabara iweze kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kutokana na mvua zinazonyesha sasa hivi hizi nyumba ambazo ziko pembezoni mwa barabara zingine zimevunjika kuta zingine zimeharibika, lakini pia imeleta usumbufu mkubwa kwa wananchi, hawawezi sasa kuingia katika nyumba zao kwa sababu barabara haijakamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba kama kunakuwa bado hakuna pesa za kutengeneza hiyo barabara imalizike ni afadhali pesa zikusanywe kwanza halafu baadaye ndiyo barabara itengenezwe. Kwa sababu barabara inachukua muda mrefu miaka mitano na inaleta usumbufu kwa wananchi. Kwa hiyo ninaomba sana sana hilo jambo walizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, TAMISEMI ilianzisha mkakati wa kujenga barabara meta 300, meta 200 ili baadaye waweze kuunganisha. Barabara hiyo imejengwa Tabata Bima ambayo inakwenda mpaka stendi ya Kimanga, lakini sasa hivi naona wameacha huo mkakati. Hizi barabara ambazo zinapita kwenye hizi kata zetu ni barabara muhimu sana na zinapitisha watu wengi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni lazima hizi barabara zetu ambazo zinapita kwenye kata zetu zina watu wengi, lakini pia ndiyo kata ambazo zinajishughulisha na mambo mengi. Mfano Dar es Salaam, mvua ikinyesha hakuna mfanyabiashara yeyote ambaye anafanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kutakuwa kuna foleni kubwa ya magari, lakini pia hata watu wa boda boda hawawezi kufanya kazi, hata mama ntilie wetu hawawezi kufanya kazi. kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri Mkuu tunakuomba katika suala la mipango ya bajeti tunaomba Mkoa wetu wa Dar es Salaam msiweze kuupangia mipango kama vile wanavyopangia mikoa mingine. Kwa sababu Mkoa wetu wa Dar es Salaam una watu wengi, lakini pia ndiyo mkoa ambao unachangia pato kubwa katika Nchi yetu ya Tanzania. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ije na mpango maalum kwa Mkoa wa Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Kibamba nimeona Serikali inataka kujenga Kiwanda cha Madawa Mloganzila, lakini ukiangalia barabara ambayo inakwenda Mloganzila ambayo inapitia Kiswopa ni barabara ambayo siyo nzuri. Kwa hiyo, ili watu waweze kuona kule kwamba ni sehemu ambayo wanaweza wakaanzisha biashara zao na kwa sababu wanapeleka miradi ya Serikali ni lazima hii barabara iweze kutengenezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ni jambo la fidia, fidia ya watu. Maeneo ambayo wanayachukua Serikali kabla hawajaanza kufanya Miradi ya Kiserikali ninaomba wananchi walipwe, hili jambo Mheshimiwa Waziri Mkuu analijua. Alikuja Jimbo la Segerea – Kipawa mpaka sasa hivi Kipunguni hawajamaliziwa fedha zao na hao wananchi sasa hivi wako katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia sasa hivi kuna tatizo la mvua wameweka matenti, tunaomba sana sana, wamebaki wachache, tunapongeza hata hao waliolipwa, lakini hawa watu wengine waliobaki tunaomba walipwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninataka kuongelea Mheshimiwa Waziri Mkuu ni jambo la Kariakoo. Tunajua kabisa kwamba Kariakoo kuna wafanyabiashara wengi na Kariakoo ndiyo sehemu ambayo inatuingizia mapato mengi. Hata hivyo, mvua ikinyesha pale, kuna mifereji ambayo ilijengwa muda mrefu kwa sasa hiyo mifereji imezidiwa ina maana ikinyesha mvua tu kwa saa mbili au saa moja Kariakoo haipitiki, maji ni mengi, watu hawawezi kwenda kununua vitu. Kwa hiyo, hiyo italeta picha mbaya ukizingatia sisi tunakwenda kupokea ugeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alikwenda katika Jimbo la Kawe, Kata ya Mabwepande pale kuna barabara ambayo inatoka Mabwepande inakwenda Bandari, tunaomba sana sana hiyo barabara ijengwe,ni muhimu sana kwa wakazi wa Kawe…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa kengele yake ya mwisho imelia hivyo, ninashukuru sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Rebeca Sanga, Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga ajiandae.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Rebeca Sanga.

**MHE. REBECA S. NSEMWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia bajeti hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Awali ya yote nimshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ameweza kunipa afya njema ya kuwa mahali hapa siku ya leo. Nimshukuru sana pia Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nianze katika sekta ya afya kama ambavyo imeandikwa katika ukurasa wa nane na wa tisa, kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Tunaipongeza sana Serikali kwa kuanzisha huduma ya Bima ya Afya kwa watu wote na kwa awamu ya kwanza wameweza kutoa bima kwa watu milioni moja laki nne hamsini na saba elfu mia sita na mbili, tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuanza kugharamia magonjwa sugu kwa watu ambao hawana uwezo au wasiojiweza, magonjwa haya yameelezwa kama vile saratani, figo, moyo, kisukari na mifupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali, nikijaribu kuangalia watu ambao tunasema hawana uwezo ni wale watu ambao watakuwa-*addressed* na Maafisa wetu wa Ustawi wa Jamii, watakuwa *ranked* kwamba hawana uwezo. Hata hivyo, nikijaribu kuangalia kwa magonjwa haya sugu ninaomba twende kwa ugonjwa wa figo, kulingana na mfumo wa maisha uliopo sasa hivi watu wengi sana wanapata matatizo ya figo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia kufanya *dialysis* katika hospitali zetu za Serikali ina *cost* shilingi ngapi? Tukaja kuona kufanya *dialysis* mara moja ina *range* kuanzia 150,000 mpaka 180,000. Mara nyingi wagonjwa hawa wa figo hufanya *dialysis at least* mara tatu kwa wiki inategemea na *accumulation* ya sumu kwenye mwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia mtu ambaye anaweza akafanya *dialysis* mara tatu kwa wiki kwa *range* ya shilingi 150,000 ina

maana kwa wiki anatumia shilingi 450,000, kwa mwezi atatumia 1,800,000. Gharama hii ni kubwa sana kwa Watanzania. Hivyo basi, niombe tunashukuru Serikali inasema itagharamia kwa watu wasio na uwezo, lakini hata kwa watu wa kati hata kwa watu wenye uwezo ambao hawako katika mfumo rasmi wa ajira jambo hili hawawezi kulimudu hata kidogo fedha hii nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina shaka kwamba magonjwa kama haya yakiingia katika familia tayari yanaenda kuleta umaskini. Kwani mtu huyu ambaye anafanya *dialysis* tunamtegemea mara nyingi kuwa *weak,* hawezi kuwa *active* kama mwanzo na *just imagine* mtu huyu akifanya mara tatu kwa wiki ina maana hawezi kufanya kazi zake za uzalishaji kama ilivyokuwa mwazo. Hivyo, niombe Serikali itusaidie huduma zote za magonjwa sugu zigharamiwe na Serikali kwa watu wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kusema katika Mkoa wangu wa Njombe ninaotoka hakuna Kituo cha Kusafishia Damu *(Dialysis)* hivyo wananchi wanapata wakati mgumu aidha waende Mbeya au kwa sasa kuna Kituo kimeanzishwa Iringa, waende Iringa. *Just imagine* mgonjwa aliyefanyiwa *dialysis* atoke kijijini huko Makete ndani Kipagalo asafiri mpaka afike Iringa anafika amekwishachoka kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tafadhali tunaomba Kituo cha Kusafishia Damu katika Hospitali ya Mkoa wa Njombe kiwekwe, ugonjwa huu umeongezeka kwa kiasi kikubwa na kwa sehemu kubwa unatokana na *life style* ya wananchi wetu, hali ambayo imekuwa ikijitokeza katika eneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie suala la mikopo ya 10% kwa akina mama. Tunashukuru sana Serikali yetu kwa kuweka sera ya kuhakikisha kila halmashauri inatenga 10% ya mapato yake ya ndani kwa ajili ya kuweza kuwakopesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tujaribu kuwasaidia hawa akina mama. Mfumo wa kupata zile fedha ni mgumu mno kwao.

Mfumo ule unaweza ukawa unawa-*favor* watu ambao wana *exposure*, watu ambao ni *well educated*, lakini kwa wale akina mama wa *interior* (ndani vijijini) ukimwambie aandike andiko, anaandikaje jamani? Hali hii inakuwa ni ngumu inawapa wakati mgumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali, tunaomba iwaelekeze Watendaji wetu wa Vijiji, wa Mitaa, waweze kuwasaidia hawa akina mama katika ku-*structure* yale maombi yao na wasiwa-*charge* kitu chochote, kwani wanakutana na changamoto. Akina mama wanapotaka kuandikiwa maandiko anatakiwa atafute mtaalam na amlipe. Sasa, atamlipa kwa hela gani? Mtu mwenyewe anaenda kuomba mkopo wenyewe wa shilingi 400,000. Andiko mtu anakwambia unisaidie nikulipe shilingi 200,000. Kwa hiyo, tutakuta azma nzuri ya Serikali inaweza isitekelezwe kwa sababu tu hatujaweka mfumo mzuri. Ninaishauri Serikali tuliangalie suala hili kwa namna nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iwasaidie akina mama ile mikopo yao kupata watu wa kuwaelekeza, itolewe kulingana na mazingira wanayotoka. Kwa mfano, wananchi wa Mkoa wa Njombe wao ni wakulima. Kwa hiyo, akina mama wengi sana wa vijijini wao ni wakulima. Basi, tupate Maafisa Kilimo ambao watawaelekeza wale akina mama na kuwasaidia kuweza kulima kilimo bora na chenye tija. Kwa hiyo, wakipata ule mkopo wanaweza kwenda kulima kilimo chenye tija *and then* waweze kupata mazao mengi zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mwisho ninaomba nichangie suala la uanagenzi. Tunashukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kuweza kugharamia kozi za uanagenzi kwa wanafunzi 5,746 kwa mwaka huu wa fedha. Tunaomba, idadi hii ni ndogo sana. Vijana wengi wako mtaani na vijana ambao hawana ajira ni rahisi sana kutumika kufanya uovu wowote. Kwa hiyo, ninaomba, ili kujiepusha na hili Ofisi ya Waziri Mkuu iongeze idadi ya kozi ya uanagenzi kwa vijana. Iongeze ili wale vijana wawe wengi, lakini pia tukishawapa ile kozi tusiwaache mtaani. Tuwashike mkono tuwasaidie ili waweze kupata mikopo ya

halmashauri na hatimaye waweze kujiajiri. Kwa kufanya hivyo kozi hii itakuwa ina tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vijana wazuri pale wanasoma useremala, tuombe Serikali baada ya kutoka pale iwasaidie waweze kupata *tender* za ku-*supply furniture* katika ofisi za Serikali. Tusiwaache tu mtaani, kwamba tutajisifu tumetoa kozi ya uanagenzi lakini je, ina *impact*? Kwa hiyo, ninaomba tufuatilie *impact* ili wale vijana wakitoka pale tukawasaidie kuwashika mikono, tuwatafutie *tender*, tuwatafutie kazi ili wawe na kitu cha kufanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Rebeca Sanga. Nilimtaja Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga na Mheshimiwa Cecilia Paresso atamalizia.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na maono makubwa ambayo ameyafanya ambayo anaendelea kuyatenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na taasisi zake na Wizara zote ambazo ziko chini yake kwa kazi kubwa ambayo ameifanya, pia kwa hotuba nzuri na uwajibikaji uliotukuka ambao ameanza kuuonyesha katika nchi yetu. Tunampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii kumpongeza Mkuu wangu wa Mkoa wa Songwe, Mheshimiwa Jabiri Makame pamoja na viongozi wengine wote wa mkoa, lakini Mkuu wa Wilaya, Wakurugenzi na watumishi kwa ujumla, kwa namna ambavyo tumekuwa na ushirikiano katika kutekeleza na kuleta maendeleo katika Mkoa wetu. Ninawapongeza sana namna hiyo na tukiendelea hivi nina uhakika mkoa wetu utapiga hatua kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka kuchangia maeneo machache tu, lakini ninataka nianze kwanza, Baba wa Taifa alituambia maadui wakubwa wa Taifa letu aliwataja watatu, na mimi leo nitaongeza ili wawe wanne, maadui wakubwa wa Taifa letu. Maadui hao alisema ni suala la umaskini, ujinga, maradhi na suala sasa la ukosefu wa ajira kwa vijana. Hawa maadui ni sumu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme ninaipongeza sana Serikali ya Awamu ya Sita imechukua hatua kadhaa kuhakikisha kwamba inapambana na hao maadui na tunawatokomeza. Mpaka sasa hivi tunaona ujenzi wa viwanda unaoendelea katika nchi yetu katika maeneo mengi. Hii ni kwa sababu tunataka kupunguza umaskini, tunataka kuongeza ajira kwa vijana, lakini pia tunataka kujenga uchumi ulio imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita kuweka ruzuku kwenye kilimo, pamoja na sekta nyingine za uzalishaji, pamoja na bajeti zao kuongezeka ili tuweze kupunguza umaskini, ili tuweze kujenga uchumi imara, ili tuweze kuhakikisha tunaondokana na ujinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona ukarabati wa bandari mbalimbali unaofanyika, uwekezaji mkubwa unaofanyika, lakini tunaona ufufuaji wa Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)* yote haya yana msingi wa kutaka kupambana na kupunguza umaskini tulionao, lakini kutengeneza ajira kwa wananchi wetu wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona utalii; Tanzania imebarikiwa kuwa na vivutio vingi vya utalii vizuri vya asili, lakini jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuvutia watalii, hili ni kwa sababu tunataka kupambana na hao maadui ambao nimewasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona ujenzi wa barabara mbalimbali unaoendelea katika nchi yetu na hasa katika maeneo mbalimbali. Ujenzi wa maghala unaoendelea, yote haya ni katika kutaka kukabiliana na umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona ujenzi wa shule na madarasa mbalimbali, vyuo, ujenzi wa zahanati, ujenzi wa hospitali, kuanzisha mambo mbalimbali. Yote haya ni katika kutaka kupambana na hao maadui wakubwa na sisi Wanajimbo la Vwawa tuko bega kwa bega katika kuhakikisha kwamba tunapambana na hao maadui wakubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka kupambana na umaskini. Hatufurahii tunapoona 25% ya Watanzania wanaishi katika umaskini. Hatufurahii kuona watoto wetu hawasomi na kupata elimu iliyo nzuri. Tunataka wapate elimu nzuri, wapate maarifa mazuri, wajifunze teknolojia za kisasa ili maisha yao yawe mazuri na yaboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivyo, sisi Wanavwawa tunaiomba sasa Serikali ya Awamu ya Sita iendelee kutuunga mkono Wanavwawa kwa kufanya mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, tunaomba Manispaa ya Mkoa wa Songwe. Mkoa wetu ni wa mwisho kuanzishwa. Mkoa wetu ni mkoa pekee ambao hauna manispaa wala halmashauri ya mji hatujapata bado. Tunaiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri Mkuu atusikie. Sasa ni wakati muafaka Mkoa wa Songwe tunastahili kupata manispaa ili iweze kuchochea kuleta maendeleo zaidi katika Mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana tuliahidiwa kujengewa stendi ya mkoa, lakini na Soko la Mazao la Kimataifa. Mkoa wetu ni wa kilimo, tunahitaji mazao yetu yauzwe kwa Watanzania, lakini pia kwa taasisi mbalimbali kutoka nje ya nchi. Tunataka soko pale, tunataka stendi pale. Ninaomba Mheshimiwa Waziri Mkuu atusikie sasa, mwaka huu ianze kujengwa. Ninajua iko kwenye bajeti, basi hela zikitoka mapema ikajengwa itatusaidia sana kupunguza umaskini na kuhakikisha kwamba Wanamkoa wa Songwe na Wanajimbo la Vwawa wanapiga hatua kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji barabara. Barabara ya kutoka Vwawa – Londoni – Isalalo – Msia – Isalalo tuliahidiwa kwamba itaanza kujengwa, tunaomba sasa mwaka huu ianze kujengwa tuone matokeo. Barabara ya kutoka Ihanda – Ipunga ni muhimu sana kwa

uchumi kwa sababu kule ndiyo uzalishaji mkubwa unakotoka. Mahindi yanazalishwa kwa wingi, kahawa inazalishwa kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Barabara ya kutoka Vwawa – Ndolezi – Iyula, ni kiunganishi kikubwa sana. Zao la kahawa litaweza kupata manufaa na hizi barabara zikikamilika nina uhakika mkoa wetu utapiga hatua kubwa na tutatoa mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji Bandari Kavu pale Mpemba. Bandari hii tumeimba kwa muda mrefu, ninashukuru kwa kuona jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita ilizozichukua katika kuhakikisha kwamba tunaanza kuijenga hii bandari. Sasa, ninaona kama tuko polepole sana, ninaomba tuongeze kasi ili ile Bandari Kavu ijengwe pale Mpemba mizigo isafirishwe na *TAZARA*, isafirishwe ifike pale, basi wananchi wale, wale wafanyabiashara wa kutoka sehemu mbalimbali nchi jirani wachukue mizigo yao pale. Tutakuwa tumechangia uchumi mkubwa, tutakuwa tumejenga uchumi mkubwa wa Mkoa wa Songwe na nchi kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wetu tunahitaji vyuo vya elimu ya juu. Hatuna chuo hata kimoja hata cha ngazi ya kata hatuna. Ni wakati muafaka umefika kwa mkoa wetu uangaliwe kwa sura ya kipekee kabisa, ili tupate angalau chuo chochote cha elimu ya juu kiweze kuwaandaa vijana wetu wawe na ujuzi unaostahili, wawe mahiri waweze kushiriki katika ujenzi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji maji katika kata mbalimbali. Pale Vwawa tuna changamoto ya maji. Ninamshukuru Mheshimiwa Rais alileta Mradi mkubwa wa Maji ule wa Mto Momba. Bado haujakamilika, ndiyo unaanza uko kwenye hatua ya awali, lakini pale pana changamoto kubwa ya maji. Ninaomba basi jitihada zifanyike ili kile Kisima cha Ichenjezya na maeneo mengine basi yaweze kupatiwa maji kwa kuangalia vyanzo vingine vilivyopo wakati tunasubiri huu mradi mkubwa kuweza kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukamilishaji wa maboma Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi kubwa sana na sisi Mbozi katika Taifa hili

ndiyo ninafikiri wilaya ya kwanza kuwa na maboma mengi ambayo wananchi walijitolea kwa nguvu zao wakaanza kujenga. Kulikuwa na maboma 1,520, mpaka sasa hivi bado mengi hatujayakamilisha. Ninaomba Serikali tuweke mkakati wa kuhakikisha kwamba haya maboma tunayakamilisha kadri itakavyowezekana. Pale Iboya tunajenga kituo cha kukagua mizigo mbalimbali, ambacho kitajengwa na *TANROADS*. Tunaomba kile kituo kijengwe haraka ili kupunguza foleni ya Tunduma ikaguliwe pale na mambo yaende. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kabla sijahitimisha niongezee mambo mawili. La kwanza, ninaishauri Ofisi ya Waziri Mkuu; tulianzisha madaraka mikoani, tulifanya ugatuaji wa madaraka. Hii sera ni ya muda mrefu, kuna haja sasa ya kuipitia vizuri kuangalia kama je, tumekidhi na kufikia matarajio tuliyoyatarajia? Ugatuaji wa madaraka mikoani ni muhimu sana, lakini tuone kwamba kweli namna tunavyokwenda namna tunavyoendesha TAMISEMI, tunavyoendesha Serikali za Mitaa tunafikia yale malengo tuliyokusudia kuyafanya. Hili ninafikiri ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ili kutatua tatizo la vijana, ninashauri waangalie uwezekano wa kuitisha kongamano la Kitaifa la kushirikisha wadau mbalimbali wa kujadili upungufu na ukosefu wa ajira, ili kusudi tuweze kutatua hili tatizo la Watanzania wote. Sekta binafsi zishirikishwe ipasavyo kuhakikisha hili tatizo tunalitokomeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, tunamalizia na Mheshimiwa Cecilia Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi ya uhai na afya njema ambayo anaendelea kutujalia na kutufikisha siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ninakishukuru chama changu, Chama Cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kuwa Mbunge wa Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ninawashukuru sana kwa imani yao kwangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua nafasi hii pia kumshukuru Mwenyekiti wetu wa UWT Taifa Mama yetu Mheshimiwa Mary Chatanda kwa kuendelea kutuongoza, kutulea na kutuimarisha ili tuendelee kuwa viongozi bora. Ahsante sana Mama Chatanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoendelea kuwafanyia Watanzania, kazi zinazozingatia na kujali utu wa Watanzania. Katika kazi kubwa anazofanya, moja ni kuendelea kusimamia na kuimarisha amani ya nchi yetu kwa kuwa amani ni msingi wa maendeleo ya jambo lolote lile. Hongera sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka amekuwa kiongozi wa nchi yetu katika kipindi kilichopita na hata sasa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuhakikisha Watanzania wanapata maendeleo na maendeleo yanawafikia kwenye vijiji vyetu, kata zetu, wilaya na hata katika miradi ya Kitaifa, kwa maana ya miradi kimikakati. Tunamshukuru sana kwa upendo wake kwa Watanzania na ndiyo maana wakati wa uchaguzi aliaminiwa na Watanzania na akapata kura nyingi za ndiyo za kishindo na za heshima kwa kazi kubwa anazofanya na anazoendelea kutufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachukua pia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ya kumsaidia Rais pamoja na Mawaziri na Naibu Mawaziri, pamoja na Serikali yote ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi wanayowafanyia Watanzania. Tuna imani wataendelea kuhakikisha kwamba ile dhamira ya Mheshimiwa Rais ya kuwaletea tabasamu Watanzania, wao kama wasaidizi wake wa karibu inaenda kuwafikia Watanzania kwa ari na kwa moyo na kwa nguvu kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia mikutano ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeona kazi anayoifanya na kupitia ziara anazofanya ameendelea kurejesha imani ya Watanzania. Tunamwombea mafanikio, asonge mbele kwa kasi hiyo hiyo, aendelee kuwafikia Watanzania popote pale walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita mchango wangu katika sekta ya elimu. Kufuatia mabadiliko ya mitaala, lakini kupitia mabadiliko ya Sera ya Elimu ya Mafunzo na Ufundi ya Mwaka 2014 pamoja na toleo jipya la mwaka 2023, sekta hii inaenda kukabiliwa na mabadiliko makubwa ambayo yanahitaji rasilimali fedha pamoja na rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba tutakapoanza utekelezaji wa Sera hii mwaka 2028, Serikali itakuwa imeshafanya maandalizi yote muhimu na ya kutosha kuhakikisha kwamba wale wanafunzi wote wakimaliza darasa la sita, wanapoanza kidato cha kwanza, kwa kuwa sera inaelekeza kwamba sasa elimu ya sekondari itakuwa ni sehemu ya elimu ya msingi na itakuwa ni sehemu ya elimu ya lazima, basi wanafunzi hao waweze kupata masomo na kufika madarasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kupunguzwa kwa muda huo na kutokana na makadirio ya awali ya wanafunzi wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza, kwa mujibu wa takwimu mbalimbali tunatarajia kwamba ifikapo mwaka 2028 kidato cha kwanza tutatarajia kuwa na wanafunzi 2,973,195. Hili ni ongezeko kubwa la mara moja na ongezeko hili litahitaji maandalizi ya kutosha na maandalizi haya yanapaswa kuanza sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapi ambayo yanatakiwa kuanza na yapi ambayo ni mahitaji? Tunapotarajia wanafunzi hao ninaomba nitaje kwa uchache mambo ambayo yanahitajika. Tunahitaji vyumba vya madarasa 35,564 kwa uwiano wa darasa moja kwa wanafunzi 45. Tunahitaji walimu wapya 35,000 kwa uwiano wa mwalimu mmoja kwa wanafunzi 45. Pia, tunahitaji matundu ya vyoo kwa wanafunzi wa kiume 31,000 kwa uwiano wa tundu moja kwa wavulana 25. Vilevile,

tunahitaji matundu ya vyoo kwa watoto wa kike 41,268 kwa wasichana na kwa uwiano wa tundu moja kwa wasichana 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kuwa na maabara 9,366. Tunahitaji mishahara kwa ajili ya walimu wapya, tunahitaji vitabu, tunahitaji gharama za uendeshaji, pamoja na mambo mengine. Haya niliyoyataja ni kwa uchache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizi, maana yake Serikali katika mwaka huu wa fedha tunaoanza kuujadili 2026/2027 tunahitaji kiasi cha shilingi trilioni 2.12 ili kuanza maandalizi ya kuingiza wanafunzi 2,973,195 kidato cha kwanza ifikapo mwaka 2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ninaipongeza Serikali kupitia hotuba ya Bajeti ya Waziri Mkuu aliyoisoma hapa, wameshaanza hatua za awali ambazo ni hatua muhimu kwa kuweka matarajio ya kutenga kiasi cha shilingi trilioni 1.77 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa Sera hii na kuhakikisha hawa wanafunzi wote ifikapo mwaka 2028, waweze kuingia kidato cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu, ni matumaini kwamba utengaji wa bajeti kwenye vitabu ni jambo moja, lakini utekelezaji ili sasa tuweze kwenda kutekeleza kujenga madarasa na mambo yote yanayohitajika ni hatua ya pili. Ni rai yangu kwa Serikali, tuone basi maandalizi yanaendelea kufanyika utekelezaji unaanza ili kuhakikisha hawa wanafunzi itakapofika mwaka 2028 wote waweze kuingia kidato cha kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi na huo ndiyo mchango wangu. Ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Cecilia Paresso.

Waheshimiwa Wabunge, huyo ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho kwa muda huu wa mchana, nitawataja Waheshimiwa watano ambao wataanza jioni ili waweze kujiandaa. Tutaanza na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima, Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, Mheshimiwa Asha Salum

Motto, na Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi; hao ndiyo wataanza jioni.

Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru kwa utulivu wenu, usikivu wenu na umakini wenu kuanzia asubuhi hadi sasa, pande zote; upande wa Wabunge upande wa Mawaziri kwa hoja mbalimbali au michango mbalimbali iliyotolewa kwa Ofisi ya Waziri Mkuu.

Baada ya kusema hayo, ninawatakia mchana mwema. Ninasitisha Shughuli za Bunge hadi Saa 11.00 Jioni.

*(Saa 6.58 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

Mwenyekiti *(Mhe. Cecilia D. Paresso)* Alikalia Kiti

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA Serikali**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano ya Hoja ya Serikali, Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Tunaanza na Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima na Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu wajiandae.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, ili nichangie hoja iliyo Mezani kwetu. Kwa kuanza ninachukua nafasi hii kumpongeza Dkt. Samia Suluhu

Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini kwa miongozo anayoitoa kwa nchi yetu na hususani anaposhughulikia suala hili la mafuta ambalo tunaona kabisa nchi za jirani na mpaka Ulaya sasa hivi katika vituo vingi vinaandikwa "*no fuel*". Hongera sana kwa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru na kumpongeza pia mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kazi nzuri anyoifanya na kwa uratibu wa hii hotuba, ambayo imesheheni takwimu, changamoto zimebainishwa na ametupa matumaini nini kifanyike ili kutatua hizo changamoto. Ninawapongeza Manaibu Waziri wa Wizara hii, ninawapongeza vilevile Mawaziri wa Nchi katika Ofisi hii; tuna Profesa Kabudi na Profesa Shemdoe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina wasiwasi na Mheshimiwa Waziri, TAMISEMI ameishi, alikuwa Mkurugenzi, akawa Katibu Tawala wa Mkoa, akawa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, TAMISEMI hana cha kujifunza, achape kazi. Vilevile, kama nilivyosema, ana Manaibu wachapakazi wazuri, lakini pia, kuna Manaibu wa Wizara nyingine ambazo zipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, kitabu hiki kimejaa takwimu. Nitatoa ushauri katika maeneo mawili, eneo la kwanza ni suala la Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu hiki kimetupa matumaini makubwa sana kwamba, Serikali yetu itaenda kufanya maboresho na itaendelea kufanya maboresho makubwa katika sekta ya kilimo. Miradi ya umwagiliaji itaendelea kutekelezwa, utoaji wa pembejeo za ruzuku kwa mazao ya kimkakati utaendelea, utoaji wa mbegu na vilevile uimarishaji wa ushirika na masoko. Hili ni jambo jema sana kwa sekta yetu ya kilimo, lakini sehemu nyingine ni kuongeza thamani ya mazao yetu na hapa nitachangia kidogo; katika kuongeza thamani ni jambo la muhimu sana, ili tusiendelee kuuza nje mazao ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kusini tuna zao la korosho, ninaipongeza Serikali kwa kuanzisha Kongani ya Viwanda vya Korosho pale Maranje, Halmashauri ya Mji wa Nanyamba. Kazi nzuri imeanza

kufanywa, ujenzi umeanza, *warehouse* mbili zimekamilika, lakini kizuri zaidi ni utekelezaji wa Dira yetu ya 2050 kwa sababu, dira ile inasema kwamba, mipango mingi itekelezwe kwa kushirikiana na sekta binafsi. Hapa tunapoongea kuna kampuni mbili kubwa zimeanza ujenzi wa viwanda viwili vya kubangua korosho, ambavyo kimoja kinaweza kubangua tani laki moja kwa hiyo, kwa viwili vitabangua tani laki mbili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo zuri ni Serikali yetu imetoa fedha kwa Bodi ya Korosho kuanza ujenzi wa kiwanda ambacho kitabangua tani 30,000 kwa hiyo, mkononi tuna uhakika mwakani tutakuwa na tani 230,000. Sasa hivi uwezo wetu wa kubangua ni tani 120,000, kwa hiyo, tukijumlisha na hizi tani 230,000, tuna uhakika mwakani tunaweza kubangua nusu ya korosho ambazo zinazalishwa Tanzania. Hongera sana Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili nina ushauri mmoja tu kwamba, hawa wawekezaji wa sekta binafsi wamefika tayari na ujenzi umeanza. Ninaiomba Serikali yangu ifanye mambo matatu, la kwanza ni, lazima tuweke *special incentive*. Tuwape vivutio rasmi hawa wawekezaji, ili tusirudi nyuma kwa sababu, huko nyuma tuna historia ya viwanda vya korosho. Tumekuwa na viwanda 12, lakini vyote vilifungwa na uzalishaji ukasimama kwa hiyo, tusirudi tulikotoka, tuwape *special incentive* hawa wawekezaji ili kazi hii ya ubanguaji iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, kazi wanayoifanya ni kubwa sana na korosho zetu zitaongeza thamani kwa sababu, hatutashughulika na korosho tu, hawa sasa watashughulika na ganda la korosho, watashughulika vilevile na tunda la korosho kiasi kwamba, mkulima sasa atapata fedha kwenye korosho yenyewe, atapata fedha kwenye ganda la korosho na atapata fedha kwenye tunda la korosho. Kwa hiyo, thamani ya korosho itakuwa imeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, hao wawekezaji wanakuja kutoa ajira kwa nchi yetu kwa hiyo, lazima vilevile tuhakikishe kwamba, hii *special incentive* inahakikisha kwamba waajiriwa wengi watakaoajiriwa pale wawe vijana wa Kitanzania, wawe *skilled* au

*unskilled,* wawe vijana wa Kitanzania. Hii itawezekana tu kama, nilivyosema, tutawapa *special incentive,* lakini vilevile suala lingine la msingi ni utaratibu ambao utawawezesha kupata malighafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, hawa watu wanatarajia kutupa ajira, tusiwape utaratibu wa kawaida, lazima wawe na utaratibu maalum wa kuhakikisha wanapata korosho nje ya utaratibu wa sasa na si utaratibu ule wa soko la awali kwa sababu, soko la awali viongozi wengine wa *AMCOS* wanatumia vibaya na hivyo kuwadhulumu wakulima. Lazima tuandae utaratibu maalum kuhakikisha viwanda vyetu hivi vinapata korosho ya uhakika, ili visije vikafungwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kongani hii ya Viwanda vya Korosho ipo kilometa 30 kutoka mkuza wa gesi asilia kwa hiyo, ili tuwape motisha ni lazima tuwapelekee gesi kwenye eneo hili la uwekezaji. Kule Mtwara kuna maeneo mawili muhimu, lile Eneo la Malanje na Eneo la Msijute, Mtwara Vijijini, nao tuwapelekee gesi asilia ili wawekezaji waweze kutumia nishati hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nimefurahishwa sana na kauli ya Waziri Mkuu kwamba, Wizara ya Kilimo ishirikiane na Wizara ya Viwanda na Biashara kuhakikisha tozo za holela kwenye sekta ya kIlimo zinakomeshwa na kuagiza halmashauri ziache kuweka tozo holela kwenye mazao ya kilimo. Hapa isiwe tu kwa halmashauri, kuna taasisi nyingi zinapeleka tozo kwenye mazao yetu ya kibiashara na hivyo kushusha bei ya mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye zao la korosho kuna zaidi ya taasisi nane zinachota ushuru kule na hivyo kusababisha kushusha bei kwa mkulima. Kuna *TMX* wanachukua fedha kule, kuna hizi *RS* wanachukua fedha kule, kuna Bodi ya Korosho yenyewe inachukua fedha, lakini kuna *TARI* Naliendele wanachukua fedha na taasisi zingine. Hawa vilevile kwa sababu, hapa tunapitisha bajeti zao za matumizi mengine kwa nini wakachukue fedha kule kwa mkulima? Kwa sababu, hata kama wanaweka *charge* ndogo, lakini mfanyabiashara anapokwenda kununua anabebeshwa *charge* ile, anapunguza bei kwa mkulima. Tuondoe hizo tozo, ili mkulima apate

bei ambayo ina tija kwa zao lake la korosho na mazao mengine ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mchango wangu wa pili utajikita kwenye Serikali za Mitaa. Ukisoma Ibara ya 146 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeeleza madhumuni ya kuanzishwa kwa Serikali za Mitaa kwamba, ni kupeleka madaraka kwa wananchi. Huko nyuma, kama walivyosema wachangiaji waliopita kwamba, kulikuwa na viprogramu mbalimbali vya kupeleka maboresho kwenye Serikali za Mitaa, hapa katikati tumejisahau, hakuna mipango hiyo na hivyo, suala la upelekaji wa madaraka kwa wananchi linakuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Serikali Kuu ina mkono mkubwa sana kwenye shughuli zinazoendelea kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ndugu zangu hatuwezi kuendesha maendeleo ya nchi hii kwa kutegemea maagizo kutoka Dodoma, ni lazima tuziwezeshe Serikali za Mitaa na kuziwezesha Serikali za Mitaa ni lazima ziwe na maamuzi, ziwe na *autonomy* na vilevile ziwe na uwezo wa kifedha, ziwe na vyanzo vya uhakika vya mapato. Halmashauri zetu hazina vyanzo vya uhakika vya mapato; vyanzo vya uhakika vya mapato vimebaki Serikali Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba na kwa sababu, Mheshimiwa Rais amefanya maboresho mazuri sana, ameihamishia Ofisi ya TAMISEMI kwa Waziri Mkuu, ninatarajia sasa Mheshimiwa Waziri Mkuu, kama ilivyosemwa kwamba, Waziri wa Nchi mwenye dhamana TAMISEMI, Mheshimiwa Profesa Shemdoe, ameishi katika mazingira haya, wataratibu haya mageuzi. Lazima kuwe na *reforms* ya kutosha kuhusu Sera yetu ya Ugatuaji. Hadi sasa hivi hatuna sera, lazima tuje na sera za ugatuaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuna Sheria ya Ugatuaji ndiyo maana leo tukiamka tunafanya hivi, kesho tukiamka tunafanya hivi. Lazima tuje na hiyo sheria, ili ugatuaji katika kupeleka mamlaka ngazi ya chini ufanywe kisheria na siyo kwa utashi wa mtu. Vilevile tubadilishe kanuni na miongozo ambayo inaendesha Mamlaka za Serikali za Mitaa; Sheria nyingi, kanuni nyingi zimepitwa na wakati, lakini vilevile ukisoma

Dira yetu ya 2050 inasema, ili tufanikiwe ni lazima tutekeleze mambo kwa isivyo kawaida, tukiendesha Serikali za Mitaa kama *business as usual* hatuwezi kutekeleza malengo ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yangu TAMISEMI, Ofisi ya Waziri Mkuu, itayafanya mabadiliko haya. Ninakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

Nilimtaja Mheshimiwa Rashid Mohamed Mtima, ajiandae Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Pia, ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa mbele yako hapa na kutoa mawazo yangu kwa hoja hii, ambayo ipo mbele yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nichangie katika maeneo kadhaa; moja, ni eneo la Wizara ya Kazi, Ajira na Mahusiano. Eneo hili kwanza ninachukua nafasi kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa anayoifanya katika sekta hii. Na-*declare interest*, mimi kwa miaka 10 nimekuwa Katibu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania, kwa hiyo, nimeona namna anavyowashika mkono wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepitia taarifa hii, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais katika eneo la kuendelea kujenga maisha ya wafanyakazi baada ya kustaafu kwa maana eneo la hifadhi ya jamii, Mheshimiwa Rais ametatua tatizo ambalo lilikuwa linafanya wafanyakazi wakose amani baada ya kumaliza kazi. Hapa nasema suala la Serikali hii ya Awamu ya Sita kuamua kulipa deni lile la *pre*-99 la michango ya watumishi ambao hawakuchangia huko mwanzo kabla ya kuanzisha Mfuko wa *PSPF*, ambao ilifika shilingi trilioni 4.7. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alivyopewa tu kijiti hiki kwa mara ya kwanza alilipa shilingi trilioni 2.15 kwa *non cash bond,* lakini sasa hivi ukiangalia thamani ya Mfuko huu wa Utumishi wa Umma umefika shilingi trilioni 13.9 baada ya kumaliza deni hili la *pre-*99. Hili tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda tena kumpongeza Waziri Mkuu, ambaye Wizara hii ipo chini yake na Waziri wa Kazi, ndugu yangu Mheshimiwa Sangu, nimeona ameanza vizuri. Nimekaa kwenye sekta hii kwa miaka 10, kwa mara ya kwanza wakati bajeti hii inaandaliwa Waziri aliwaalika viongozi wote wa vyama vya wafanyakazi na kubadilishana nao mawazo na baadaye kushiriki katika kushuhudia bajeti hii wakati inasomwa. Hili ni jambo kubwa sana kwa maana limewaweka karibu wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyama vya wafanyakazi ni sehemu ya kuandaa mazingira bora ya wafanyakazi sehemu ya kazi na sisi kwa sababu, tumejishirikisha kwenye shirika la kazi duniani na mikataba tukaikubali, basi suala la kuhakikisha kwamba, tunakuwa karibu na tunasimamia vizuri vyama vya wafanyakazi ni suala ambalo ni la muhimu sana. Ninataka nishauri jambo kidogo hapa, kule kwenye vyama vya wafanyakazi yapo masuala hayaendi vizuri; huko mwanzo tunakumbuka tulikuwa na JUWATA, baadaye tukawa na *OTTU*, tukawa na *TFTU*, baadaye tukaenda vyama vya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaenda kwenye vyama vya kisekta, mfumo ulikuwa mzuri sana kwamba, kila chama kilipewa sekta maalum, lakini katikati hapa toka 1995 mpaka sasa Katiba za vyama zikabadilishwabadilishwa katika hatua ambayo sekta moja, chama kimoja, kikaenda kwenye sekta zingine. Kwa hiyo, kuna migogoro ambayo haitoi taswira nzuri ya hivi vyama kwenye kutenda kazi na kuwatumikia wanachama wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, badala ya kuwatumikia wanachama wao, basi wao wanagombana, kwa maana ya kugombania wanachama na hasa chama kinachoshughulikia Serikali za Mitaa na kile ambacho kinashughulikia Wafanyakazi wa Serikali kuu,

wanagombania sana wafanyakazi wa sekta ya afya. Kwa hiyo, katika eneo hili ninashauri kwamba, ofisi hii au Wizara ione kwa namna gani inaweza ikaweka mipaka, ili vyama hivi vi-*concentrate* kwenye kuwahudumia wanachama badala ya kugombania wanachama. Huo ndio ulikuwa ushauri wangu kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili ni Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hapa ninataka nioanishe ni kwa namna gani tunaendana na mipango yetu kwenda kule kwa wananchi. Kama tunakumbuka, tumechangia hapa Mpango wa Miaka mitano, tumepata taarifa au Hotuba ya Mheshimiwa Rais; hotuba yake ukiangalia kama kuna kitu cha mwisho cha ku-*conclude,* katika hotuba yake alisema ni tabasamu kwa Watanzania kwa miaka mitano hii, lakini ukisema miaka mitano hiyo, tutaenda kutoa tabasamu kwa nyenzo ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaenda kutoa tabasamu kwa nyenzo ya Mpango wa Miaka Mitano, huu ambao nao tumeuzungumzia hapa. Tunapoelekea kwenye Mpango wa Miaka Mitano maana yake ni tunatekeleza kwa mpango wa mwaka mmoja hadi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti hii ndiyo *landing ground* ya mipango yetu inayokuja, nikajiuliza nikisema tabasamu kwa Mtanzania ni maeneo yapi ambayo ukiweza ukifanya utawagusa, nikasema kama kuna maeneo ya msingi ya kwanza ni pale ambapo tunaenda kum-*assure* Mtanzania eneo lake la kujishughulisha katika maisha yake, huyu Mtanzania anafanya nini? Kama tutaenda kugusa pale tutamtengenezea tabasamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, ni eneo la huduma, ustawi. Je, akitaka kumpeleka mtoto shuleni anapokelewaje? Anapata mazingira ya namna gani? Anapougua anapata mazingira yapi? Maeneo haya mawili tuki-*capitalize* tukaweka juhudi kubwa ndipo tutatengeneza tabasamu kwa Watanzania. Tabasamu hii tutaitengeneza kwa miaka mitano, huu ni mwaka wa kwanza tunataka tuanze, ninadhani ni eneo la kwanza ambalo tunatakiwa tuweke mazingira mazuri ya kwenda huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikaangalia kwenye bajeti ya TAMISEMI nimeona maeneo mengi ambayo yamezungumza mafunzo katika *level* ya Mkoa na nini, lakini nikasema hapa na nishauri kidogo. Ushauri wangu ni kutengeneza eneo zuri la kuanzia kwenda kutengeneza tabasamu na tabasamu hili kule tukisema eneo la uzalishaji na eneo la ustawi wa jamii, walioko maeneo haya ni wafanyakazi wa Serikali za Mitaa, ni watu ambao wananchi wanafanya nao kazi moja kwa moja, sasa je, katika bajeti hii tumeliwekaje hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Serikali tunapelekaje kule kwenye Halmashauri namna ya kutekeleza mazingira mazuri kwa mwaka huu wa kwanza ili baada ya miaka mitano tuone tabasamu. Nilitamani kuona namna ya kwenda kuwajengea uwezo kule kwenye Serikali za Mitaa ili watafsiri haya mawazo ya mpango wa miaka mitano wa kuleta tabasamu kwa wananchi. Kwa hiyo, nilitamani kwenye bajeti hii tuone ni mikoa inaandaliwaje kwenda kuwawezesha Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifika kwenye Serikali za Mitaa je, tunaandaje kutoka kwenye halmashauri yenyewe kwenda kwenye kata? Leo tuna Afisa Kilimo kule Mcholi chini kabisa Jimbo la Newala Mjini...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kidogo. Ninatamani twende tukamwekee malengo ambayo yataenda kumgusa mwananchi ili aweze kupata tabasamu kwa kuzalisha korosho vizuri na akaona faida ya yeye kuwa na akampenda huyu mtumishi kuwa sehemu ya maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Yagi Maulid Kiaratu, wajiandae Mheshimiwa Salum Motto na Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi, lakini nichukue fursa binafsi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu na mwingi wa rehema. Vilevile nitumie fursa hii kukishukuru sana chama changu, Chama Cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Mwenyekiti wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo alisimamia mchakato wa uchaguzi kuanzia kura za maoni hadi uchaguzi mkuu na hatimaye leo niko hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wa Jimbo la Singida Mjini kwa imani kubwa waliyoonesha kwangu wamenichagua kwa kura nyingi nami mbele yako ninawaahidi kwamba nitawatumikia kwa weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikiliza hotuba ya Waziri Mkuu nimeisoma mara kadhaa, nimeielewa. Taarifa hiyo imetueleza watu tumetoka, mafanikio tuliyoyapata, lakini nini makusudio na matarajio ya wananchi wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kupongeza kwenye makusanyo ya mapato, Serikali imefanya vizuri sana kipindi hiki. Kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 mpaka kufikia Februari tayari walishakusanya shilingi bilioni 26.63 dhidi ya bajeti ya makadirio ya mwaka huo ambayo ni trilioni 25.68 sawa na 103.7%. Haya ni mafanikio makubwa sana na hii inaonesha namna gani sasa nchi inajipanga kwenda kujitegemea na kupunguza utegemezi wa kutoka nje, vilevile uwezo wa kuhudumia jamii ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri zetu pia zimechangia, ziko halmashauri 184, ziko zinazokusanya kwa kiasi kikubwa ziko zinazokusanya kwa kiasi cha kati, lakini ziko zinazokusanya kiasi kidogo. Miongoni mwao zipo zinazofikia malengo na zipo zisizofikia malengo kwa sababu mbalimbali. Ninaiomba sana Serikali izisaidie halmashauri ili ziweze kupata fedha na kuhudumia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya eneo ambalo ninataka kuongelea ni fedha ambazo zinakusanywa na halmashauri kwa niaba ya Serikali, lakini sehemu inayotakiwa kurejeshwa huwa hairejeshwi kabisa au inarejeshwa kidogo au haipatikani kabisa. Nitoe mfano wa kodi ya ardhi, Halmashauri zinakusanya kodi za ardhi zinafikisha Serikali, zinapaswa kurudishwa 20%, lakini haijahi kurejeshwa hata siku moja, tukumbuke fedha hizi zinakuwa ziko kwenye bajeti na zinaathiri bajeti kwa maana ya kutofikia malengo. Vilevile, zinaathiri utekelezaji wa shughuli za halmashauri kwa maana ya kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano wa Halmashauri ya Manispaa ya Singida ambayo imekusanya shilingi milioni 999.1, ambapo ilitakiwa irejeshewe shilingi milioni 199.8, sawa na shilingi milioni 200, lakini hazijawahi kurejeshwa. Shilingi milioni 200 kwenye bajeti ya halmashauri ni pesa kubwa sana. Ninaomba basi taratibu za kisheria zifuatwe na fedha hizo ziwe zinarudishwa kwa wakati ili ziweze kufanya kazi zilizokusudiwa kwa mwaka husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ina kila sababu ya kuzisimamia halmashauri. Tunaona kabisa ziko halmashauri zinakusanya kidogo na hivyo kutoa huduma kwake ni shida. Ninaomba kupitia miradi mikakati halmashauri zipate fedha na miradi hiyo mara nyingi inakuwa imesimama mwaka mzima kuweza kukusanyika. Mfano, mzuri halmashauri zinajengewa stendi zinajengewa masoko. Ninaiomba Serikali Halmashauri ya Manispaa ya Singida ina soko kongwe sana, soko lililojengwa mwaka 1958 linahatarisha walaji, linahatarisha wanaofanya kazi katika eneo hilo lakini pia uwezekano wa halmashauri kupata mapato mazuri unakuwa mdogo. Ninamwomba Waziri Mkuu kupitia nafasi hii basi Serikali ione namna ya kusaidia wananchi wa Manispaa ya Singida kupata soko zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee habari ya afya. Kwa muda mrefu Halmashauri ya Manispaa ya Singida ilikuwa haina Hospitali ya Wilaya, ni miaka miwili tu tuliachiwa ile ilikuwa Hospitali ya Mkoa kuwa Hospitali ya Wilaya lakini ikiwa haina kitu chochote. Historia ya hospitali hiyo imejengwa mwaka 1950 na kwa wakati wote imekuwa ikikarabatiwa tu, inakosa miundombinu mingi ya muhimu kama chumba cha wagonjwa mahututi, wodi zimechakaa, *OPD* ndiyo haifai

kabisa. Ninamshukuru Naibu Waziri wa TAMISEMI alifika na amejionea, lakini niombe sasa tupate fedha tujenge hospitali nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hospitali ndiyo imeanza ina mapungufu makubwa ya watumishi, kwa maana ya waganga na wauguzi. Tunaye Daktari Bingwa mmoja tu wa Magonjwa ya Wanawake, hakuna Daktari Bigwa wa Magonjwa ya Watoto, hakuna Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Ndani *(physician)* lakini hatuna wateknolojia wa madawa, hatuna wateknolojia wa mionzi, hatuna fundi sanifu wa vifaatiba, pia hatuna watalaam wa dawa za usingizi. Hospitali kubwa yenye hadhi kama hiyo kukosa wataalam wote hao siyo sawa. Tunaomba sana TAMISEMI watuangalie watuletee wataalam hao ili tuweze kufanya vizuri katika suala zima la tiba tutekeleze yale ambayo tumeahidi wananchi katika Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiongelea suala la elimu tumefanya vizuri sana, tumejenga madarasa na shule mpya, tumejenga shule ya sekondari ya wasichana kila mkoa, tumejenga shule za amali, tumepata ajira mpya, lakini bado kuna mapungufu katika miundombinu. Nitoe mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Singida mpaka kipindi kilichopita ilikuwa na Shule ya *A Level* moja tu ambayo ni shule kongwe ya Mwenge Sekondari. Ninamshukuru Rais leo tunavyoongea zimeongezeka shule tano za *A-Level. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kilichofanyika ni kujenga mabweni, na madarasa na matundu ya vyoo tu, lakini iko miundombinu muhimu iliyosahaulika. Watoto wale wanakaa *boarding,* hakuna *dinning hall,* wala hakuna jiko, vyakula vinapikwa mahali ambapo hapafai, lakini watoto wanakula ovyo nje, mara mabwenini mara madarasani, siyo sawa kwa afya za watoto wetu. Tunaomba tunapojenga shule hizi basi angalau miundombinu hii muhimu iangaliwe ili watoto wetu wakae katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la *TARURA* kama ambavyo wamesema wenzangu. Kwa kweli tunayo shida kubwa ya barabara, hapa ninavyoongea Mji wa Singida unahudumiwa kwenye mtandao wa barabara za *TARURA* kilometa 523 tu, takwimu ambayo

ni ya zamani sana. Mji wa Singida unakua kwa kasi, ukiangalia unavutwa na Mji Dada wa Dodoma, tuna zaidi ya kilometa 2,000 ambazo hazijaingia kwenye mtandao, tunaomba Serikali ifanye mapitio ya kila mara ili kupata uhalisia wa urefu wa barabara, lakini bajeti pia ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Waziri Mkuu kwa namna ambavyo ametoa tamko mbele ya Bunge hili kwamba sasa anaamrisha hela zote ziende kwenye Mfuko na tuzitungie sheria zisitumike bila kibali maalum ili lengo zima la kutengeneza barabara likamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakiri maslahi, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Afya na Masuala ya UKIMWI; tumetembelea, tumeangalia lakini leo niongelee kidogo kuhusu UKIMWI. Hapa bado kuna shida, wote tunafahamu historia ya ugonjwa huu ulianza zamani, ukapewa majina mbalimbali slimfiti, Juliana na kadhalika, pia zamani watu walikuwa wanakonda watu wanaogopa UKIMWI, lakini leo hakuna anayekonda wala hakuna anayeonekana kwa macho kwamba ana UKIMWI.  Hii inawafanya watu kupunguza kasi ya upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu ya Watanzania zaidi ya milioni 60 wanaopima hata robo hawafiki, hii maana yake elimu bado haijafika kwa wananchi au kuna kupuuza, hivi ni lazima Serikali ifuatilie kuhakikisha kila mtu anatambua hali ya mwili wake. Wale wanaobainika wana matatizo tayari wanapata tiba na kwa sababu ni tiba endelevu za kila siku walio wengi wameacha na hili ni tatizo kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, tulienda konga moja Ilala, maeneo ya Pugu, katika watu 700 waliacha matumizi ya dawa waliofanikiwa kurejeshwa ni watu 200 tu, sasa ni hawa walioonekana huko majumbani wako zaidi ya hawa. Kwa hiyo, tuna kila sababu ya kuongeza elimu, ufuatiliaji kuhakikisha wale wanaopatikana wanatumia dawa, kwa ajili ya nguvu kazi ya Taifa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. YAGI M. KIARATU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie kidogo, hasa suala la uraibu wa dawa za kulevya na UKIMWI. Tumegundua kwamba hawa watu wanaendana na Dar es Salaam ni wengi mno, huko tunakoenda watakuwa wengi zaidi. Wako wasiofika kwenye vituo na wako wanaofika kwenye vituo. Serikali iliangalie vizuri na waathirika wengi ni vijana ambao ndiyo nguvu Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Asha Salum Motto, aweze kuchangia.

**MHE. ASHA S. MOTTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa ninampongeza Waziri Mkuu kwa hotuba nzuri, hotuba yenye matumaini kwa Watanzania, ninaomba mchango wangu nijielekeze kwenye sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tunavyojua Serikali inafanya kazi kubwa sana katika kuendeleza sekta hii ya afya hasa kutengeneza miundombinu, lakini pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kupewa tuzo bora iliyotokana na kuzuia vifo vya mama na mtoto, hongera sana Dkt. Samia Suluhu Hassan, kazi zake zinaonekana na jitihada zake zinaonekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza pia Serikali kwa kutengeneza Kiwanda kikubwa sana cha Dawa kile cha Arusha, ifikapo 2030 kiwanda kile kinaenda kutuheshimisha, zamani dawa tulikuwa tunapata 80% zinatoka nje, 20% sisi wenyewe, ifika 2030, 80% itatoka ndani na 20% tutategemea kutoka nje. Hii ni hatua kubwa sana kiwanda hiki kinaenda kutuheshimisha Nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Afya ina mambo mengi sana, ninaomba nijielekeze kwenye magonjwa sugu hususani suala zima la ugonjwa wa figo. Ugonjwa wa figo ni miongoni mwa magonjwa ambao unaendelea kukua kwa kasi sana, magonjwa haya

hasa kwa sasa yanaathiri sana vijana kuliko miaka ya zamani. Takwimu ya ugonjwa wa figo Tanzania inaonesha asilimia saba ya Watanzania wana ugonjwa wa figo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu waliogunduliwa na ugonjwa wa figo wanafikia takribani 8,800, watu wanaotumia *dialysis* mpaka sasa wamefikia 3,800, watu 5,000 mpaka sasa hivi bado hawatumii hii huduma ya *dialysis*. Ukiangalia takwimu hiyo unaona kabisa idadi ya wagonjwa wanaohitaji huduma ya *dialysis* imeongeze kama mara tatu kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita. Mwaka 2019 wagonjwa wa figo walikuwa 1,017, mwaka 2023 wagonjwa hawa wa figo waliongezeka kufikia idadi ya watu 3,200, ukiangalia 2025 wagonjwa wa figo wamefikia zaidi ya wagonjwa 3,300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, magonjwa haya yanayo visababishi mbalimbali, lakini visababishi hivi ukiangalia hasa kuna kisukari, *pressure*, mtindo wa maisha ambao ulaji wa chumvi, mafuta na pombe au sigara. Ukiangalia takwimu vijana wengi ndiyo wanaoathirika sana na ugonjwa huu, ninaomba niishauri Serikali ichukue ugonjwa huu wa figo kama *agenda*, niwashauri Wabunge wenzangu ugonjwa huu unaenda kuteketeza nguvu kazi ya Taifa. Baada ya miaka 10 ijayo kama hatutaweza kuthibiti ugonjwa huu wa figo vyanzo vinavyosababisha ugonjwa wa figo hakika nguvu tunayoitumia ndani ya Bunge hili kufanya uwekezaji mkubwa, kuwa-*invite* wawekezaji katika miradi mikubwa tutafanya kazi ya bure kwa sababu miradi inaenda kutekelezwa na nguvu kazi ambazo tunaenda kuzitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nishauri ikiwezekana tuongeze bajeti kwenye Wizara hii ya Afya hasa kwenye kitengo hiki cha magonjwa sugu ili kufanya *awareness* ili tuweze kupambana na gonjwa hili na changamoto hizo ambazo zinasababisha ugonjwa huu. Kama ambavyo Serikali ilipambana na ugonjwa wa UKIMWI, kama ambavyo Serikali ilipambana na magonjwa haya ikiwemo kifua kikuu kutafuta kinga. Hivyo hivyo, ugonjwa huu wa figo tuchukue kipaumbele ili kunusuru nguvu kazi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichangie katika sekta ya uchumi wa bluu. Mpango wa Maendeleo ya Taifa umeeleza kuwa uchumi wa bluu kuwa ni mpango wa mkakati katika kukuza uchumi wa Taifa kwa kutumia rasilimali zinazotokana na mito, bahari pamoja na maziwa. Kule Mkoa wa Mtwara tumebahatika kuwa na bahari ambayo ina rasilimali nyingi sana zinazotokana na bahari ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Mkoa wa Mtwara una wafanyabiashara ambao tayari wameshaji-*engage* katika suala zima la kuvuna zao la mwani, kufuga majongoo, kusindika samaki, lakini wavuvi wadogo wadogo wapo wengi sana ambao wanavua samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, ninaomba nishauri Serikali, kwa kuwa pia tuna bahari kubwa ambayo ina pweza, ina *prawns* na samaki wengi, mazao haya ya bahari yanachochea kipato kikubwa sana Nchini Tanzania. Ukiangalia takwimu ya uchumi mwaka 2024, asilimia kubwa ya kipato kile ilitokana na mchango huu wa mazao haya ya Bahari. Ilichangia *USD* dola takribani 180.6. Unaona ni namna gani uchumi unaotokana na rasilimali za bahari unachangia kiasi kikubwa sana uchumi wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri hapa sasa; kwa kuwa tuna uwezo wa kuvua samaki hao tunaomba Serikali kuongeza kupeleka vifaranga vya samaki na kutupatia vifaranga vya *prawns* ili tuweze kufuga kwa wingi zao hili ili liweze kuongeza tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wale wadogo wadogo ambao tayari wameshajiingiza katika kusindika vyakula vile wapewe mafunzo, mitaji, waongezewe elimu ya kutosha ili waweze kuongeza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie suala la mwisho linalohusu maendeleo ya jamii. Ninaipongeza sana Serikali kwa kutupatia mikopo ya 10% kwenye sekta hii ya maendeleo ya jamii. Kwenye hizi 10% kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu; wanawake wanapata asilimia nne, vijana asilimia nne na watu wenye ulemavu wanapata asilimia mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Mkoa wa Mtwara una jumla ya wanawake 158,165. Takwimu ya maendeleo ya jamii inaonesha kuwa Mkoa wa Mtwara Mwaka wa Fedha 2024/2025 ina jumla ya vikundi ambavyo ni rasmi 1,142. Kati ya vikundi hivyo vikundi 661 tu ndivyo vilivyopata mikopo; vikundi 481 havijapata mikopo kutokana na sababu mbalimbali, ikiwemo suala zima la *NIDA*, wengine walikuwa na mikopo sehemu nyingine, lakini pia kulikuwa na upungufu wa fedha ambazo zilisababisha vikundi vingine kutopata mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishauri Serikali; lakini kabla sijashauri; hata ufuatiliaji wa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwenda kuhamasisha vikundi bado kasi ni hafifu, kasi ni ndogo sana. Hii ninaona itakuwa ni changamoto ya Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Mtwara una kata 191. Nimefanya ziara kwenye kata zote 191 mwezi Januari. Kila nilipopita changamoto inakuwa kwamba hawamfahamu Afisa Maendeleo ya Jamii, wakati Waziri wa TAMISEMI mwaka jana alitoa tamko kwamba kila kata kuwe na Maafisa Maendeleo ya Jamii, lakini kila nilipokanyaga hawamfahamu. Kila nilipopita malalamiko ni kwamba hatupati mikopo, hatuna mikopo, wengine tumekosa vigezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia takwimu ni kubwa sana, wanawake ni wengi, vikundi vilivyobaki ni vingi na vikundi hivi vilivyopata mikopo bado kiasi walichopata ni kidogo sana. Ninaiomba Serikali itie nguvu; hasa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, ninaomba iliangalie suala hili kwa mapana zaidi ili kuwawezesha wanawake hawa waweze kupata mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge ninaomba kukumbusha tena Kanuni yetu ya 76 inafafanua staha ndani ya Bunge. Ukisoma Kanuni ya 76(3)(c) inasema tukipita mbele, pembeni au kuizunguka siwa au kati ya kiti cha Spika na Mbunge anayesema. Waheshimiwa ninaomba

tukumbuke hii kanuni mara kwa mara, hasa panapokuwa na wachangiaji humu ndani ya Bunge.

Tunaendelea, nilimwita Mheshimiwa John Francisco Nzilanyingi.

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kabla sijasema ninaomba nianze kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametujalia afya na uzima na hata tumekutana hapa tukiwa salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni mara yangu ya kwanza ninachangia kwenye hoja hii na kusimama mbele ya Bunge hili, nitumie fursa hii sana kuwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Nyamagana kwa namna ambavyo wananipa ushirikiano na hivyo kuifanya kazi yangu ya Ubunge kuwa nyepesi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwa nimeyasema hayo ninaomba sasa nami nichangie kwenye maeneo machache ambayo yameguswa kwenye hoja ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitapita kidogo upande wa TAMISEMI. Kwa bahati njema nimekuwa Mjumbe wa Kamati ya TAMISEMI, nimepata fursa ya kuyachakata kwa upana masuala yanayowagusa Watanzania moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee sana nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI Profesa Shemdoe. Kwa kipindi kifupi ambacho nimekaa naye Mheshimiwa Profesa ameonesha uhodari mkubwa sana. Sambamba na Profesa Shemdoe nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mwigulu. Kwa kipindi ambacho ameifanya kazi ya kupita kwenye mikoa mbalimbali amefanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipokuja kule kwetu Mwanza, Wanamwanza walimwona kama mtu wa tofauti sana kutokana na kazi njema alizokuja kuzifanya. Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kipindi

kifupi ameleta matumaini pale ambapo Watanzania walionesha kukata tamaa, ameleta nuru pale ambapo Watanzania waliona giza. Mheshimiwa Waziri Mkuu ameleta matumaini na kuwaunganisha watu ndani ya kipindi kifupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mantiki hiyo nikubaliane na wenzangu; ya kwamba kazi zote hizi zinazofanywa na wasaidizi wa Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI pamoja na Mheshimiwa Waziri, Mkuu ni kazi ambazo zinaakisi mipango na nia njema ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambayo imejielekeza kuleta maendeleo sawasawa na mapenzi ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande wa Wizara hii ya TAMISEMI nimeisoma bajeti hii kwa mapana, lakini nimeiona ipo changamoto kubwa sana upande wa *TARURA*. Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakubaliana na mimi; ninapochangia kwenye mpango huu wa bajeti tumekaa sana na Profesa Shemdoe, lipo jambo la dharura kwenye upande wa *TARURA*. Barabara nyingi kwenye majimbo yetu zimeharibika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo yalitoka yakapelekwa kwa Mameneja wa *TARURA*, wameleta maombi ya dharura, Wizara imekwishafanya tathmini ambapo tayari imebaini kinahitajika kiasi cha zaidi ya bilioni 90 kwenda kukabiliana na changamoto ya dharura ya mafuriko na kuharibika kwa miundombinu ya barabara kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuishauri Serikali, kwa sababu kazi nzuri imekwishafanyika, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ai-*push* Serikali iweze kutoa fedha ili tukaweze kupambana na kuondoa adha ya changamoto za barabara ambazo zimekatika katika majimbo yote. Hii haihitaji kuchukua muda mrefu sana kwa sababu fedha hizi ni kwa mpango wa dharura. Haitakuwa na maana kubwa sana fedha zimeombwa mwezi Machi wakati wa mahitaji halafu ziletwe mwezi Juni au Julai; dhana halisi ya dharura haitakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upande huo huo wa TARURA ipo sheria moja ambayo pengine tuliipitisha kwenye Bunge hili hili ambayo inatufanya kurudi huko tulikotoka. Sheria hii ni kandamizi sana. Watendaji wa *TARURA* chini ya Waziri wa TAMISEMI wanafahamu. Ipo changamoto ya kuharibika kwa barabara. Unaweza ukakuta barabara imetoboka shimo kidogo tu, imeharibika sehemu ndogo sana, lakini kwa namna sheria hii ilivyo Meneja wa *TARURA* wa Wilaya ambaye si Meneja wa *TARURA* wa Mkoa hana mamlaka ya kuidhinisha fedha kwenda kufanya ukarabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninajaribu kufanya *analysis* katika Jimbo langu la Nyamagana; kuna changamoto kubwa sana ya mashimo pale Liberty. Nilijaribu kuzungumza na meneja wangu wa *TARURA* akaniambia thamani ya fedha iliyokuwa inahitajika kuziba pale haivuki hata milioni tano; lakini kwa utaratibu ulivyo hata kama kingelikuwa ni kiraka cha shilingi milioni moja ni lazima aandikiwe Meneja wa Mkoa aletewe Waziri ije kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndani ya Bunge hili ili ipitishwe kwenda kuziba kiraka cha shilingi milioni moja; kitu ambacho hatuwatendei haki Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tukubaliane; maisha ya Watanzania wengi tunaowawakilisha kwenye majimbo yetu yanaguswa moja kwa moja kwenye suala la miundombinu ya barabara. Ninataka nikwambie, katika Jimbo langu la Nyamagana, mtandao wa barabara ni zaidi ya kilometa 1,225. Nilikuwa ninajaribu kufanya hesabu kidogo kwa haraka haraka, nikasema kama tutakwenda na utaratibu wa namna fedha zinavyokwenda kutengeneza hizi barabara itatuchuku zaidi ya miaka 150 Nyamagana kuenea lami kwenye mitaa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nini kifanyike; nimekwisha kushauri huko nje na hapa ninaomba nishauri. Jimbo la Nyamagana ambalo ndilo Jiji la Mwanza makusanyo yetu ya fedha za ndani ni zaidi ya bilioni 30. Nilikuwa ninataka kuishauri Serikali na kuiomba sana; sisi watu tunaotoka kwenye Majiji, tunaotoka kwenye Manispaa watupe vibali ili tuweze kukopa fedha tujenge barabara kwa wakati ili tuweze kuwasaidia wananchi wetu kuondokana na changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *simple logic* tu, dunia ya leo nikirejea maneno ya marehemu Mengi, aliwahi kusema wakati anazungumza na moja ya makongamano ya vijana. Alisema kuwa huwezi kuwa tajiri bila kukopa na ndiyo maana hata sisi mradi wetu wa reli tulilazimika kukopa na hatimaye tunayaona manufaa yake leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakitupa kibali sisi watu wa Mwanza wa Jimbo la Nyamagana tukaenda benki tukachukua fedha bilioni 50 au 60, kwa kuanzia, barabara ambazo tungezijenga kwa zaidi ya miaka 30, ninataka nikuhakikishie kuwa ndani ya kipindi cha miaka mitatu karibu robo ya barabara zote ndani ya Jimbo la Nyamagana zitakuwa zimejengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nje na hilo nigusie kidogo upande wa 4:4:2; kwa maana ya fedha ya 10% ya vijana, akina mama na watu wenye ulemavu. Tunafahamu kuwa huko nyuma fedha hizi zilikuwa zinatoka kwa utaratibu maalum; lakini hapo katikati zikasimama. Kwa dhamira ya dhati na upendo wa Mheshimiwa Dkt. Samia kwa Watanzania fedha hizi zimerejeshwa tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikwambieni ukweli, kwamba malengo ya fedha hizi kwenda kuwahudumia wananchi wetu ili waweze kupata mikopo kwenye halmashauri zetu si sawa na vile ambavyo ilikusudiwa. Watanzania wengi wenye sifa hawapati hizi fedha; na mimi nimejaribu kufuatilia kwa *research* ndogo, takriban 75% – 80% ya waombaji hawapati hizi fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii yote ni kwa sababu ya ukiritimba. Lipo jambo moja ambalo wakati wa kupita pita lilikuwa linanisikitisha sana. Ukienda huko chini kwenye kila kata tuna Maafisa wa Maendeleo ya Jamii. Utaratibu wa kuzitoa fedha hizi unavyofanyika; wanaweka hayo matangazo, lakini hakuna taarifa inayopelekwa kwa wananchi kwenda kuwahamasisha na kuwapa elimu. Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii wamebaki kuwa ni watu wa ofisini kusubiria kupokea maombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa dhana halisi ya kuwatumikia Watanzania, jambo la kwanza wanapaswa watoke wawafuate

wananchi walipo, wakaitishe mikutano, wawahamasishe wawaeleze masharti na namna gani wanaweza wakazipata hizi fedha ili ziweze kuwasaidia kuinua uchumi wa mmoja mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi letu la vijana linahangaika na ajira na hii ni ajenda ya nchi ama pengine ni ajenda ya dunia. Serikali haiwezi kuajiri watu wote. Namna pekee ya kuwasaidia vijana wapate ajira ilikuwa ni kupitia fedha hizi za 10% kwa vijana pamoja na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niishauri sana Serikali, Profesa Shemdoe, waangalie namna mpya ya usimamizi wa hizi fedha, fedha hizi kwenye baadhi ya maeneo zinakwenda benki, zinakaa huko zaidi ya mwaka hazijawahi kuguswa wakati Watanzania wenye uhitaji wapo wengi. Kwa hiyo nitumie sana fursa hii kuiomba Wizara husika pamoja na Serikali, iangalie namna bora ambayo itaweza kuwasaidia Watanzania na hatimaye kijana wa Kitanzania, mama wa Kitanzania na watu wenye ulemavu waliopo ndani ya nchi yetu waweze kunufaika na mikopo hii ambayo Dkt. Samia Suluhu Hassan ameendelea kuitoa kwenye Taifa letu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. JOHN F. NZILANYINGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha nitumie fursa hii kumpongeza sana Dkt. Samia, amefanya kazi nzuri, nchi imetulia, wananchi wanafanya kazi zao kwa amani. Niwahakikishie tu wananchi ambao wanatusikiliza, sisi wawakilishi wao tupo macho kuifanya kazi iliyo njema ya kuishauri Serikali. Zaidi ya yote nina uhakika, kwamba matumaini aliyoyaahidi Mheshimiwa Dkt. Samia ifikapo 2030 yanakwenda kuonekana kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Lucy Edward Mwakyembe, wajiandae Mheshimiwa Mvita Mustafa Ali, Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano pamoja na Mheshimiwa Shaffin Ahmedali Sumar.

**MHE. LUCY E. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami kwa kunipa nafasi ya kuongea tena katika Bunge lako hili Tukufu kwa ajili ya kuchangia hoja ambayo imewasilishwa na Waziri Mkuu ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa upekee ninapenda nimpongeze Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutunukiwa shahada ya heshima ya udaktari ambayo imetoka katika Jimbo la Chuo Kikuu Nasarawa Nchini Nigeria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa uongozi wake thabiti; ambapo aliweza kuahidi kabla ya kuingia madarakani; kwamba atakapoingia madarakani ndani ya siku 100 ataweza kuyatekeleza mambo mengi. Mambo hayo ni pamoja na elimu, afya, mambo ya maji, na miundombinu. Pia tumeona kuwa hata kwa upande wa bima ya afya ameweza kuwafikia wananchi zaidi ya milioni moja na laki nne pamoja na kaya laki mbili na sabini na sita elfu na nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende pia kumpongeza Mheshimiwa Rais ameweza kutoa ajira za walimu 7,000 na ajira 5,000 kupitia upande wa afya. Ameweza kuhakikisha kuwa analeta fursa ya vijana kwa kuanzisha Wizara ya Vijana na kuwamwagia mabilioni ya shilingi. Bilioni 200 ameziweka kwa ajili ya vijana ili kuweza kuongeza uchumi katika maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel Nchimbi ambaye anamsaidia Mheshimiwa Rais katika kutekeleza majukumu yake. Tunaona kuwa amezindua mpango wa kitaifa wa pamoja kati ya waajiri, vyuo vya ufundi stadi pamoja na vyuo vikuu kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ukurasa wa tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Dkt. Mwigulu Nchemba ambaye ni Waziri Mkuu pamoja na watendaji wote wanaomsaidia kazi, bila kumsahau Profesa Shemdoe ambaye yupo katika Wizara ya TAMISEMI, nami nikiwa mjumbe wa Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichangie upande wa ajira kwa vijana. Tumeona lengo la Serikali kutaka kukuza ajira kwa vijana na wanafanya kazi kupitia ajira zilizo rasmi na zisizo rasmi, ajira za Serikali na za sekta binafsi. Kwenye upande huu ninaomba Serikali pamoja na sekta binafsi pale zinapotangaza fursa za ajira basi ninaomba kwanza tuangalie vijana wa kizalendo ambao wanajitoa kutumikia sekta hizo, sekta binafsi na sekta za Serikali bila kulipwa posho zozote, wameamua kwa uzalendo wao kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa inapotokea ajira kupitia sehemu hii, ninaomba sana nishauri Serikali waangalie vijana hawa, itafute namna ya kuwaingiza kwenye ajira. Idara ambazo wanazitumikia vijana hawa ni idara hizo hizo zinazoletwa katika kuhitaji wafanyakazi. Ni idara zile zile wanazozifanyia kazi lakini kitendo kinachokuja kujitokeza wakati kazi zinapotangazwa wanakuwa hawafai katika idara zile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Serikali iwasaidie vijana hawa wa Kitanzania ambao ni wazalendo katika kuwaingiza sehemu hizo za ajira. Pia, ninapenda kuipongeza zaidi Serikali; inaendelea kuzitoa fursa za ajira kwa vijana kwa asilimia nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nigusie kwenye 10% zinazokusanywa kwenye halmashauri kupeleka kwa vijana, watu wenye ulemavu pamoja na wanawake. Hapa mimi nitagusia kwa upande wa wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona halmashauri nyingi zinajitahidi kutoa mikopo kwa ajili ya wanawake. Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amehakikisha

maisha ya wanawake yanakuwa mazuri. Mama amewatua wanawake ndoo kichwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuwatua ndoo kichwani wanawake, Mama ameamua kuleta tabasamu kwenye familia, lakini kwa upande huu wa mikopo ambao halmashauri inatakiwa itoe kwa ajili ya wanawake, mikopo hii haiwafikii wanawake, tabasamu lile linaishia njiani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lile tabasamu ambalo Mama anataka kulipeleka kwa ajili ya Watanzania hawa linaishia njiani. Maisha ya familia yanakuwa ya kujikokota na tunajua mama ni nguzo muhimu naye kwa Taifa la sasa kwenye familia. Kwa hiyo, tunaomba Maafisa Maendeleo ya Jamii, wamebaki kukaa ofisini, hawawafuati wanawake, wakawapa elimu jinsi ya kuomba mikopo, jinsi ya kufanya biashara kutokana na hiyo mikopo, jinsi ya kutumia hizo pesa kwenda kwenye biashara ili ikuze biashara zao na jinsi ya kurudisha mikopo hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba sana Serikali na ninatoa ushauri, Maafisa Maendeleo ya Jamii, washuke, wasimame kutoka ofisini, wasibaki ndani ya ofisi. Kazi ya sasa ya Mheshimiwa Dkt. Samia anataka watu kuwafikia wananchi. Tumemwona Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, amefika ndani ya mikoa na wilaya kuwasikiliza wananchi, kusikiliza kero za wananchi na Maafisa wa Maendeleo ya jamii, wanatakiwa wafike kwa wananchi, kwa wanawake hawa wa Kitanzania ili kuhakikisha wanawafikishia mikopo hii ambayo inatolewa na Serikali, lakini bila ya kuwasahau vijana na watu wenye ulemavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanatakiwa wakatoe elimu kule, wamejifungia na hapa ninaona ule utaratibu wa upimaji malengo ambayo ni *PEPMIS* inawahusu wafanyakazi ambao ni Maafisa wa Maendeleo ya Jamii, ambao wengine hawatoki katika idara zao kuwafuata wanawake. Tunaomba, tunaomba sana, wanawake hawa wafikishiwe tabasamu ambalo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amewaahidi wanawake wa Kitanzania kuwafikishia ndani ya mwaka wa fedha 2026/2027. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nigusie kwenye madeni ya watumishi. Ninajua sasa hivi Serikali inapitia changamoto kubwa, lakini kuna madeni ya watumishi ambayo yapo yanaonekana. Hapa niwapongeze sana baadhi ya halmashauri, wamehakikisha wanafuta madeni ya watumishi pamoja na madeni ya wazabuni. Wamepunguza madeni kwa asilimia kubwa sana madeni haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana na lengo la Serikali ninajua kwenye bajeti yake hii imetenga fedha nyingi kwa ajili ya kupunguza madeni hayo. Mimi niiombe tena Serikali wasaidie mzigo ule kwa halmashauri kupunguza madeni yale, hususan madeni yasiyokuwa ya mishahara, yafutwe na ikiwezekana yasizalishwe tena au yazalishwe kwa uchache, kwa sababu, madeni yanafutwa, lakini yanaendelea kuzalishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yanazalishwa vipi? Katika kipindi ambacho watumishi wamepewa ajira ile hamahama ya watumishi, amefikishwa wilaya nyingine anataka kuhama kurudi wilaya nyingine; hii nayo inazalisha madeni ya watumishi. Kwa hiyo, ninaomba hapa kwa kuishauri Serikali iongeze nguvu ya kulipa madeni ya watumishi, lakini iongeze nguvu ya kulipa madeni ya wazabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa muda huu, nami ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Mvita Mustafa Ali na Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano ajiandae.

**MHE. MVITA MUSTAFA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijalia afya ya leo kuweza kuhudhuria ndani ya Bunge lako hili Tukufu. Pia nikushukuru na wewe kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia Bajeti ya Waziri Mkuu iliyoletwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru sana wanawake wa Mkoa wa Kusini walionipa ridhaa kuja kuwawakilisha, kuwasemea

changamoto zao na kutoa maoni yao. Ninaahidi mbele yako kwamba, sitawaangusha na nitawatumikia ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishukuru sana pia Chama changu Cha Mapinduzi kwa kunilea tangu nikiwa Mwenyekiti wa Tawi hadi kufika taifani na hivi leo nimekuwa Mbunge wa Viti Maalum, ninawasemea wanawake wenzangu wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Kusini. Ninakiombea kwa Mungu Chama hiki kiweze kushika madaraka awamu bila kutetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninatoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna anavyoipambania nchi yake, pamoja na wananchi wake kiujumla. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninathubutu kusema Mama huyu ni wa mfano, mwenye maono na mzalendo na ninamwombea pia abarikiwe yeye na kizazi chake, pamoja na familia yake na jamii ya Watanzania anaotuongoza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kumpongeza Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wangu kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa namna anavyoipambania Nchi ya Zanzibar kwa kuleta maendeleo makubwa na kutuliza amani ndani ya Nchi ya Zanzibar. *Insha Allah* naye Mwenyezi Mungu atampa busara na hekima ya kuongoza vyema Zanzibar, Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu mkubwa ninapenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na wananchi wake wa Jimbo la Iramba Magharibi kwa upendo wao mkubwa waliouleta, walioufanya, kutuletea mchapakazi huyu ndani ya Bunge letu hili Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina furaha zaidi pale ninapomwona Mheshimiwa Waziri Mkuu akihudumia ama akifanya ziara kwenye mikoa tofauti tofauti na kuyachukua matatizo ya Watanzania akayaona kama ni matatizo ya kwake. Kitendo hiki cha Mheshimiwa Waziri Mkuu kinadhihirisha kwamba yeye ni mtu mwenye utu, mwenye

ubinadamu na mwenye ustaarabu. Itoshe kusema kwamba ninamwombea naye dua kwa Mwenyezi Mungu *Insha Allah* Mungu ampe hatma njema na amuone mja wake. Amina. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu mimi ni mdogo nitajikita zaidi kwenye sekta ya uvuvi hasa uvuvi wa bahari kuu. Ninaipongeza sana Serikali yangu sikivu kwa kutambua umuhimu wa wavuvi wadogo hasa wale wanaovua ukanda wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii imeamua kwa makusudi kuwaletea meli ambayo imefika Februari na ni meli yenye njia ya mshipi wa kina kirefu (mita 22) kwa lengo la kupunguza ukali wa wavuvi hawa, kwa lengo la kuwaongezea kipato wavuvi hawa na kwa lengo pia la kuongeza kipato cha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kushauri Serikali yangu tukufu. Kwa kuwa Tanzania ni sehemu ambayo ina bahari kuu ndani yake; ni dhahiri kwamba wananchi wengi wa maeneo hayo ya bahari kuu, ni wenye kufanya shughuli za uvuvi hasa uvuvi wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Zanzibar kuna maeneo yapo karibu sana na ukanda wa bahari kuu, takribani kutoka maeneo wanayoishi wavuvi hao unaweza ukatumia takribani masaa mawili au masaa matatu. Maeneo hayo ni machache ambayo ninayoyajua yapo Katika Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kusini Unguja. Maeneo hayo ni Vijiji vya Jambiani, Mtende, Kizimkazi, na Makunduchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo wanayokwenda kuvua hujulikana kwa jina maarufu fungu mbaraka. Maeneo hayo ya fungu mbaraka ni maeneo ya bahari kuu kama tujuavyo bahari kuu kabisa (kina kirefu cha maji). Ninahurumia sana wavuvi hawa wadogo wadogo wanaokwenda kuvua bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza wanapoondoka kufikia eneo hilo la uvuvi la bahari kuu, kwanza kabisa kinachopotea kwa wao ni mawasiliano. Maeneo hayo hayana mawasiliano kabisa na tuangalie

ukaribu wa kutoka kijijini wanakoishi na wanakokwenda kuvua takribani masaa matatu tu, lakini ndani ya masaa matatu wakifika mawasiliano yale hupotea kabisa. Hii inadhihirisha uchungu wanaoupata wakati wanapokuwa kwenye kazi zao za kutafuta riziki. Huwa takribani kwa muda wa siku tatu au nne wanapokwenda kuvua, wanashindwa kupata mawasiliano na familia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyenzo zao pia wanazotumia kufikia huko haziridhishi na ni duni. Ni nyenzo za zamani, mara nyingi hutumia maboti ya mbao ama *fibre* ndogo. Kama tujuavyo bahari kuu ni sehemu ya hatari, lakini pia ni sehemu yenye kina kikubwa sana cha maji. Hata hivyo, vyombo vyao wanavyotumia ni vyombo duni kama tulivyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kubwa kwa Serikali, wavuvi hawa waweze kusaidiwa kwa hali na mali. Ingawa Serikali yetu imeshanunua meli nayo ni moja, lakini pia ninaiomba Serikali yangu inunue meli japo za *size* ya kati kuweza kuwapatia wavuvi hawa wanaovua sehemu ya ukanda wa bahari kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwahurumie waume zetu hawa, kaka zetu hawa, ndugu zetu hawa. Maana kadhia wanayoipata inakuwa ni kubwa sana. Ninasema hayo kwa sababu mimi ni mdau, lakini pia ni mkazi wa maeneo hayo ambayo nipo karibu na bahari kuu. Hivyo, ninaiomba sana Serikali yangu sikivu iweze kuwasaidia, ishirikiane na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar waweze kusaidiwa wavuvi hawa wadogo wadogo wanapokwenda maeneo ya bahari kuu kwenda kuvua, wapatiwe boti angalau za *size* ya kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivyo, tutawasaidia sana kukuza kipato chao, lakini pia zile ajira kwa vijana nazo pia tutaziinua sana kwa sababu maeneo haya vijana wanapokuwa wamefanya mtihani na hawakufaulu, basi kazi yao kubwa wao hujishughulisha kuingia kwenye uvuvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama Serikali tunahitaji kuongeza ajira kupitia vijana na kupitia sekta hii ya uvuvi wa bahari kuu, basi lazima tuwasaidie wavuvi hawa kuwapelekea boti ndogo

ndogo zenye miundombinu za kuwasaidia, za kuweza kuwapatia kipato zaidi, lakini pia kuongeza pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kusema hayo kwa sababu ni mara yangu leo ya kwanza, lakini nimeamua kuzileta changamoto za wenzangu. Ninashukuru sana kupata nafasi hii na ninashukuru sana kwa kuwasilisha changamoto za wenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ramadhani Hamza Singano, Mheshimiwa Shaffin Sumar pamoja na Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa wajiandae.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nikushukuru kwa kuniona ili niweze kuchangia Hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia kila rehema za kuwepo hapa. Mwenyezi Mungu ambaye hata ambayo bado hayakuwa anajua ikiwa yatakuwa, yatakuwaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu kipenzi Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mapenzi makubwa ya kuwa Rais wa maono kugusa nyoyo za watu, lakini kuwa na mipango ambayo siku zote inaleta tija katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Waziri Mkuu, ambaye naye ni kiongozi wa maono akitembea kama alivyo Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hili tumelidhihirisha pale ambapo alikuwa katika ziara za kimikoa, alipopita katika Mkoa wa Tanga, lakini Wilaya ya Lushoto halafu akafika Jimbo la Bumbuli ambalo mimi ndiyo mwakilishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru pia Kamati ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii iliweza kufika Bumbuli Jimbo ninaloliwakilisha katika Kiwanda cha Mponde na walitoa tabasamu kubwa kwa

wananchi wa Mponde kwa kuongelea, kupokea na kushauri kuhusu matatizo ya kiwanda hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiongozi mzuri utamwona. Katika mashairi ya Ndugu Shaaban Robert alieleza sifa ya viongozi wazuri na viongozi wabaya, lakini viongozi wabaya alitumia mnyama kuku kwa sababu kuku ni mnyama yupo karibu sana na binadamu. Kwa kutumia lugha za vinaya na lugha za majazi akasema:

"Kuku akipata nyama, hukimbia ale peke,
japo wenzake watamuandama waishike,
katu hatokubali, iondoke mdomoni,
atatafuta mahali, ajilie kwa makini,
kuku akipata nyama, hukimbia ale peke." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama Samia hayuko hivyo. Mama Samia yuko kama yule kiongozi aliyesifiwa na mwanafalsafa mmoja akiitwa Christopher Robin akamwambia: *"You are braver than you believe, you are stronger than you seem and you are smarter than you think."* Christopher Robin walikuwa wakibishana sana na huyu jamaa yake, lakini kwa sababu ni mzalendo hakuacha kumsifia. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye yale maeneo machache ambayo ninataka niyagusie. Kwanza kabisa ni eneo la afya. Ninashukuru sana Katika Jimbo la Bumbuli Mama Samia wakati ameingia tayari ametupatia zahanati 17. Mambo ya ajabu sana, mapinduzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna vituo vinne vya afya ambavyo viwili wakati wake vilianza na vingine ameviboresha hapo nyuma. Niombe sasa kidogo, maana imeandikwa katika Waraka wa Kwanza wa Wathesalonike 5:17-18 kwamba, "Ombeni pasipo na kikomo na shukuruni katika kila jambo." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiki Kituo kimoja cha Milingano, kimejengwa lakini hakijaweza kukamilika. Sasa ili tabasamu liwafikie wana Bumbuli niombe katika Wizara hii ya TAMISEMI sasa

wakikumbuke kituo hiki ambacho kitaleta tabasamu kwa Watanzania walioko Bumbuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nihame niende kwenye eneo la elimu. Eneo la elimu Katika Jimbo la Bumbuli kuna mageuzi makubwa na Mama Samia avishwe taji lake.  Hata hivyo, zipo shule chache kwa sababu ya umbali, basi hapa tutahitaji kupata mabweni kutoka eneo moja linaitwa Kwebamba kuja Kata ya Milingano, Sekondari ya Mibukwe. Kumbukeni Waheshimiwa Wabunge, umri tuliosoma sisi miaka ile ni tofauti na sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabinti wanachukuliwa kule kilometa 30, wanaenda sekondari inabidi wapangishiwe maeneo ya kuishi bila uangalizi. Kwa hiyo, eneo hili linahitaji mabweni ambayo yatasaidia watoto wa kike kupata haki yao ya elimu katika hali ya utulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekee kwenye eneo la vijana, wenzangu wamegusa maeneo mengi muhimu. Ninaomba nikumbushie tu suala la *NIDA* ni tatizo na niombe tamko maalum litoke ili wale wanaopaswa kutekeleza hilo wafanye mara moja, kwa maana vijana wanakosa fursa hii ya mama Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekee tena katika eneo muhimu, eneo nyeti la barabara. Kwanza nianze kuomba kabla sijashauri niombe Barabara ya Mbelei – Ibaga – Mgwashi – Mkongowi – Milingano kilometa  42 ni barabara ya kimkakati. Ilijengwa kidogo na *TARURA*, lakini labda ni kwa sababu ya bajeti ghafla wakaondoka. Niombe hii ikumbukwe ili kuzidi kuleta tabasamu kwa Watanzania walioko pembeni mwa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara nyingine ambayo ni kipaumbele pia kwa Wanabumbuli ni kilometa  22 kutoka Soni hadi Bumbuli – Dindila, lakini awamu ya kwanza kilometa  22 upande wa Bumbuli na kilometa  9.3 kwa upande wa Korogwe Vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ni mengi muda ni mchache, lakini niombe kuna barabara ya kimkakati inayounga majimbo matatu: Jimbo la Mlalo, Jimbo la Lushoto, Jimbo la Bumbuli na

hatimaye Korogwe Vijijini kilometa 87.3 ambayo ni Barabara ya Magamba – Mlola – Makanya – Milingano – Mashewa, hii nayo ni barabara ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa muda ni mfupi niende kushauri kwa wenzangu wa *TARURA,* mimi ni Mhandisi niliyesajiliwa na Bodi ya Uhandisi nilitaka niwashauri kidogo katika mambo ya kitaalam. Muda usipotosha basi nitafikisha kwenye meza ya ndugu yangu Mheshimiwa Shemdoe ili aweze kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kwa sababu ya mvua nyingi na mabadiliko ya tabia ya nchi ndiyo yanasababisha hilo. Basi ni vizuri sanifu zetu ziwe ni *Climate Resilience Design*, kwa maana miundombinu iweze kustahimili mvua nyingi katika maeneo ya milima na maeneo mengine ya tambarare, lakini mifereji ya pembeni *(side drains)* ziwe za kutosha, lakini na mitaro ya kupunguza kasi ya maji ambayo kitaalam wanaita *catch water drains*. Kwa sehemu za tambarare kuna vitu vingine tunaita *mitre drains* zikiwekwa za kutosha zitaweza kuondoa maji haraka barabarani, lakini kutumia makaravati mengi na madaraja kwa maeneo ya milima huwa barabara zetu hazina tofauti na mfano wa nyoka kwa sababu ya kwenda na *contour* za milima..

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaweza ukakuta mto mmoja umeukatiza mara tano. Kwa hiyo, maeneo ya milima yapewe kipaumbele cha makalavati ili maji ndiyo adui wa kwanza. Wakati ninasoma Chuo Kikuu profesa wangu alinishangaza sana aliniambia adui wa kwanza wa barabara ni maji, adui wa tatu ni maji, wa pili na wa tatu kwenye barabara ni maji. Kwa hiyo, hii alikuwa akionesha msisitizo kwamba maji yasipotafutiwa njia yana kawaida ya kutafuta njia yake na hapo ndipo uharibifu utakapokuwa unatokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuwe tunadhibiti maporomoko katika maeneo ya milima. Tujitahidi kuweka *buffer zones* ambazo mtu haruhusiwi kufanya shughuli zozote za kibinadamu ikiwepo kilimo na kupanda nyasi pamoja na miti rafiki ambayo itazuia mmomonyoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende eneo lingine, mambo ni mengi, lakini nitayaandika ila niende eneo la ushirikishwaji wa jamii katika kutunza barabara. Hili jambo hapo nyuma lilikuwepo na wenzetu wa *TANROADS* kabla ya *TARURA* zilikuwepo hata kambi za ujenzi, ilikuwepo pale Mkuranga, ilikuwepo kambi ya ujenzi pale Manga ukielekea Tanga na maeneo mengine. Hizi zilifanya vizuri kwa sababu *emergence* zikitokea (dharura zikitokea) walikuwa wakizikabili mara moja. Sasa kwa sababu sina wasiwasi na *TARURA*, sina wasiwasi na wataalam wa Tanzania ninadhani walikalie hilo waliangalie upya, lakini jamii ishirikishwe kwa matengenezo madogo madogo na mikataba midogo midogo ambayo ni *community-based contracts*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutoa elimu ni muhimu kwa jamii hii athari gani itapatikana ikiwa mifereji itakuwa haijadhibitiwa, ikiwa mifereji itakuwa imezibwa na watu wanaofanya shughuli za kilimo. Pia, kuunda vikundi vya ulinzi wa barabara kwa maeneo husika, leo barabara imekuwa ndiyo moyo wa Watanzania, barabara leo kama haipitiki, shughuli za biashara hazitafanyika, watoto hawataenda shule kwa sababu zitabomoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende pia katika eneo la kuweka vipaumbele katika barabara: barabara zetu ni lazima tuziwekee vipaumbele, tutenge barabara kwa makundi, ziwepo barabara za kiuchumi kwa maana ya barabara ambapo tutapitisha mazao na kwenda kwenye minada na masoko. Ziwepo barabara za huduma muhimu kwa mfano huduma za hospitali, lakini na kwenda shule, hizi barabara zipewe kipaumbele. Ukiangalia katika mtandao, Wilaya ya Lushoto ni zaidi kilometa 1,200 na kwa Bumbuli tuna kilometa 544. Kwa kuwa haya mambo ni ya kitaalam zaidi niombe niyafikishe kwenye meza ya Waziri ndugu yangu Mheshimiwa Shemdoe, nami sina wasiwasi naye, atayafanyia kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache nikushukuru sana na niwashukuru viongozi wetu kwa kujitahidi kuonyesha tabasamu kwa Watanzania. Ninashukuru sana kwa kupata nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako.

**MHE. RAMADHANI H. SINGANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Shaffin Ahmediali Sumar.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote ninaanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uhai na hatimaye tumeweza kukutana leo hii. Ninampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri anayoifanya kwa ajili ya Watanzania. Ninamshukuru sana pia kwa kuniteua kuwa miongoni mwa wagombea kupitia Chama Cha Mapinduzi na hatimaye leo hii nipo mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru sana wananchi wote wa Jimbo la Uyui kwa kuniamini na kwa kunichagua na hakika nitawatumikia. Bila kusahau, ninampongeza sana Jemedari wetu, Mwenyekiti wetu wa Mkoa wa Chama Cha Mapinduzi, ndugu Said Mkumba kwa namna anavyotushauri na kuendeleza masuala ya chama katika mkoa wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau, ninampongeza sana Mkuu wetu wa Mkoa, ndugu Paul Matiko Chacha kwa namna ambavyo anaifanyia kazi Tabora yetu kwa kushirikiana na timu yake ya Ulinzi na Usalama. Hakika Tabora sasa hivi inapiga hatua za maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niseme suala moja la huzuni ambalo limetokea sasa hivi kwa bahati mbaya katika Jimbo langu la Uyui Kata ya Ilolangulu, Shule ya Msingi ya *MCBS* Roma hivi sasa inaendelea kuteketea na moto. Ninaomba nitumie nafasi hii kuwapa pole wahanga wote, lakini jambo la kushukuru ni kwamba hakuna mtoto au mwanafunzi hata mmoja aliyepoteza maisha. Zimamoto wameshafika na wanaendelea kusaidiana na wananchi Mungu asimame nao katika kipindi hiki kigumu na mimi pia niko pamoja nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo chetu cha Maendeleo ya Jamii Tengeru kilianzishwa mwaka 1963 ni dhahiri kwamba chuo hiki kimekuwa cha zamani, lakini ni miongoni mwa vyuo vichache ambavyo vilianzishwa hapa Tanzania baada ya uhuru. Pamoja na uchakavu wa chuo hiki bado kinafanya kazi nzuri sana. Nimpongeze sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa chuo hiki na cha kihistoria ameanza kupeleka fedha kwa ajili ya mabweni na jengo la utawala, tunamshukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jengo la utawala limeshakamilika kwa takribani 80% kilichobakia ni kipande kidogo wanahitaji kama bilioni 4.7 hivi ili jengo likamilike ikiwa ni pamoja samani zote zinazohitajika. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, namna ambavyo anafanya kazi nzuri, namna ambavyo anawatetea Watanzania, ninaomba na hii sehemu ya Tengeru atuone kwa jicho la huruma atusaidie hizo fedha tuweze kukamilisha huo mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo kama hivi vinatuzalishia vijana ambao wanaenda kufanya kazi za maendeleo ya jamii. Hawa ndiyo wanaenda katika kata mbalimbali wanashirikiana na jamii, kuisaidia jamii kupata maendeleo. Sasa vijana wanapokuwa wametoka chuoni na kwenda kwenye kata mbalimbali nafasi wanapata kazi za Maafisa Maendeleo ya Jamii, lakini wanakosa usafiri wa kwenda kuwazunguzukia jamii. Ninaiomba Serikali ione namna bora ya kuwasaidia hawa Maafisa wetu wasibaki kuwa ofisini tu, wasaidiwe usafiri waweze kuitembelea jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mifuko yetu ya Hifadhi ya Jamii sasa hivi inafanya vizuri sana. Hapa nimpongeze sana Waziri wa Kazi, Ajira, Mheshimiwa Deus Sangu anasimamia vizuri, anazifanyia kazi vizuri. *NSSF* imekuwa ikifanya vizuri mwaka hadi mwaka na uwekezaji wa *NSSF* sasa hivi kwa kweli ni mkubwa sana, unaridhisha. Tunaridhika kwa sababu fedha hizi ni fedha za Watanzania tunaona kabisa zinaenda kufanya kazi na faida inapatikana. *NSSF* wamewekeza kwenye kiwanda cha sukari, lakini pia *NSSF* wanaenda kumalizia jengo la Mzizima *Towers* ambayo inaenda kukamilika mwezi Desemba, 2026. Mwakani *Insha Allah* Dkt. Samia Suluhu Hassan ataenda kuzindua panapo uzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji kama huu ndiyo unahitajika katika nchi yetu. Leo ukitizama Mfuko wa *PSSSF* nao pia wamewekeza vizuri katika Kiwanda cha Ngozi kilichopo Kilimanjaro ni uwekezaji mzuri sana. Sisi Watanzania na Serikali yenyewe tunatakiwa tuunge mkono juhudi za Mifuko yetu ya *NSSF*. Nitaiomba sana Serikali yetu kwamba, kwa kuwa tuna Kiwanda cha Ngozi ambapo pia viatu vya aina mbalimbali vinatengenezwa vikiwemo vya kijeshi, basi Serikali yetu kupitia majeshi yetu wanunue viatu vyote kutoka kwenye kiwanda chetu cha ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TARURA* imezungumziwa sana hapa na wengi sana wanalalamika kuhusiana na suala zima la barabara. Nami pia katika jimbo langu ni muathirika wa barabara. Bajeti inayopangwa kwa *TARURA* kwa mwaka haiendani na uhalisia wa wingi na mtandao wa barabara. Kwangu bajeti iliyopo ni bilioni 1.5 kwa mwaka hivi tunavyoongea katika bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026 fedha ambazo zimepelekwa *TARURA* hazizidi hata milioni 350. Kwa hali hii tunawasaidiaje Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Serikali iangalie namna mbadala katika tozo ambazo zimewekwa kwa ajili ya barabara kupitia *TARURA,* basi hizo fedha ziweze kupatikana kwa wakati. Nitatoa mfano mdogo sana ambao unafanana na mifano mingi ya Waheshimiwa Wabunge waliochangia hapa kabla yangu. Nina Barabara moja ambayo ni ya Ndono – Ufuluma – Makazi ina kilometa 43 tu, lakini leo tunavyoongea huu ni mwaka wa saba barabara hiyo haijafanyiwa marekebisho hata kidogo, hali ni mbaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakazi wanaoishi katika hizi kata tatu ni zaidi ya kata 52,000 kufuatana na Sensa ya 2022. Wakazi 52,000 wanakosa huduma ya barabara, lakini barabara hii katika msimu na msimu unaanza katikati ya mwezi Aprili na kuelekea mwishoni mwa mwezi Aprili. Kwenye msimu barabara hii inasafirisha tumbaku yenye thamani ya bilioni 22. Hakika hii inaonyesha kwamba *TARURA* haina uwezo wa kuhudumia hii barabara ambayo ina kilometa 47 tu. Ninaomba sana ama fedha ziongezwe kwa *TARURA*, ama hii

barabara ipewe kipaumbele basi ipandishwe hadhi iwe chini ya *TANROADS* iweze kuhudumiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa juhudi za Dkt. Samia Suluhu Hassan, sisi katika Mkoa wetu wa Tabora tunanufaika na Mradi mkubwa wa Maji kutoka Ziwa Victoria. Kwa kweli mradi ni mzuri na ifikapo mwaka 2028 nina uhakika kwamba wilaya zote za Mkoa wa Tabora zitakuwa zinatumia maji ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushauri, maji ya Ziwa Victoria kwa Manispaa ya Tabora Mjini yamefika sehemu inaitwa Bwawa la Igombe. Kutoka Bwawa la Igombe miundombinu iliyopo inasambaza maji haya, lakini pale pale pembezoni mwa Bwawa la Igombe kuna vijiji vingi ambavyo bado havijanufaika na maji ya Ziwa Victoria na havimo katika mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba sana Waziri Mkuu kupitia Wizara husika ya Maji aangalie utaratibu wa kuwasaidia wananchi ambao wako pembezoni mwa Bwawa la Igombe kwa sababu tukisubiri mradi huu ukamilike na uwafikie ni muda mrefu. Tunaweza tukapata *solution* ya muda mfupi tukawasaidia hawa wananchi wakanufaika na maji ambayo Mama Samia ameyafanyia kazi kwa juhudi kubwa na anataka kuona kila kitongoji kinapata maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuja na programu nzuri ya uanagenzi. Hii programu ni nzuri na imetengewa fedha vizuri. Kuna theluthi moja ambayo inatokana na mapato ya *SDL* yanayokusanywa na *TRA*. Fedha hizi zinapokusanywa kila mwezi kabla ya tarehe saba (7) huwa zinaenda *TRA* na ni fedha za uhakika…

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda umekwisha?

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ndiyo, muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie. Ninaomba hizi fedha ambazo zinavyokusanywa na *TRA*,

inafanya kazi nzuri ya kukusanya zaidi ya makadirio, basi fedha kwa ajili ya wanagenzi iweze kutolewa kwa usahihi na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Fagason Aron Nkingwa na Mheshimiwa Alan Thomas Mvano na Mheshimiwa Janeth Peter Pinda wajiandae.

**MHE. FAGASON A. NKINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuzungumza yale ambayo kama Waheshimiwa Wabunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tunaenda kuyazungumza leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kukushukuru wewe lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna ambavyo anaendelea kulipambania Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijazungumza mengi ninataka niseme jambo moja. Ninapenda nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, muumba wa mbingu na nchi, aliyetusababisha Wabunge wote tuliokuwemo humu ndani tukiwa salama kwa sababu ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ni mara ya kwanza kusimama kwenye Bunge hili, lakini nimesimama kwenye Bunge hili kwa sababu ya wananchi wangu wa Jimbo la Mbogwe. Jimbo langu la Mbogwe lina wananchi takriban 362,825, walipo wananisikia, wananiona lakini Mwenyezi Mungu ananiona zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza niunge hoja mkono kabla sijasahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizungumze yale ambayo Rais huyu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameyafanya kwenye Jimbo la Mbogwe. Jimbo

la Mbogwe, kama nilivyozungumza mapema, lina wananchi 362,825, lakini yapo maendeleo makubwa aliyoyafanya kwenye Jimbo la Mbogwe, ikiwemo ahadi yake ya siku 100 ameweza kutupa watumishi zaidi ya 156.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ahadi zake za siku 100, pia ameweza kunipa shilingi 1,500,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule zilizopo Wilaya ya Mbogwe, lakini Mama huyu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye Jimbo langu la Mbogwe, ameweza kujenga shule ya amali yenye zaidi ya shilingi 1,600,000,000 ambayo ipo pale kwenye Jimbo langu la Mbogwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais huyu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameweza kujenga shule ya *VETA* yenye zaidi ya shilingi 1,300,000,000 kwenye Jimbo la Mbogwe. Ninaomba nizungumze kuhusiana na hii shule ya *VETA* iliyojengwa kwenye Jimbo langu la Mbogwe. Tunafahamu na tunatambua kwamba, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametoa mkopo wa zaidi ya shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuhakikisha tunawasaidia vijana, akina mama na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kwenye Jimbo langu la Mbogwe tumeweza kupokea zaidi ya shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuhakikisha tunawabeba vijana pamoja na akina mama, tunawapa mikopo kuhakikisha wanajiendeleza katika maisha yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe ushauri. Katika Jimbo langu la Mbogwe tunao vijana wengi sana, ninao vijana takribani 14,000, lakini vijana hawa wanahitaji mikopo inayotolewa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameleta mikopo hii, lakini niiombe sana kama Serikali, kwa sababu tunazo shule ambazo zina mafunzo ya hawa vijana, hususan kwamba tumeletewa pikipiki nyingi ambazo zinakuja kwa vijana. Juzi nimepokea pikipiki zaidi ya 51 kwa ajili ya vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana, Serikali iliangalie hili tunawapa vijana wetu pikipiki, lakini hatuwapi mafunzo. Kutowapa mafunzo vijana wetu tunasababisha ajali nyingi zinatokea, watu wanavunjika miguu, watu wanapoteza maisha kwa sababu ya kukosa uzoefu kwa maana ya kwamba tunazo shule za kuwafundisha vijana wetu ili waelewe namna gani wataendesha vyombo hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali itusaidie, kwa sababu tunazo shule ambazo zitaenda kuwasaidia hawa vijana. Tunapowapa mikopo na kuwanunulia bodaboda tuwaombe sana watusaidie kuwalipia mafunzo ili waweze kujifunza kuhakikisha kwamba wanaendesha bodaboda hizi au pikipiki hizi, kwa sababu wasipofanya hivyo tutaingia kwenye changamoto kubwa ya kuwapoteza ndugu zetu, ajali zimekuwa nyingi kwa sababu hatuna mafunzo ya hawa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Waziri kwenye Jimbo langu kama nilivyozungumza ninao vijana wengi, lakini vijana hawa wanatamani na wanatambua kwamba Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anawapa vifaa kwa ajili ya kuhakikisha wanajiendesha. Ninaomba tuje tutengeneze mfumo wa kuwafundisha vijana wetu waendeshe pikipiki kwa kufuata mfumo wa kuepuka ajali. Kwa sababu ajali zimekuwa ni nyingi, ukizingatia vijana wetu kama tunavyojua tuna vijana wa aina mbili. Wapo vijana wanaojiita *Gen-Z*, lakini vijana hawa wa *Gen-Z* tunao wa aina mbili: tunao vijana wa *Gen-Z* wenye akili timamu, lakini tunao vijana wa *Gen-Z* ambao hawafai kabisa kwenye nchi hii. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninalizungumzia hili? Leo kuna changamoto ya kutolewa nyeti. Jambo hili la watu kutolewa nyeti limekuwa ni changamoto sana kwenye Taifa letu. Nimwombe Waziri jambo hili tunatakiwa tulichukulie *serious* sana kwa sababu jambo hili limekuwa ni kubwa, watu wameuawa na wamejeruhiwa. Kwa hiyo, nikiwa kama kijana niliyesimama hapa jambo hili haliwezekani, kwa nini? Ninamshukuru sana Mheshimiwa Waziri husika, leo ametupatia mfano kwamba wanaume wapange foleni washikane mabega. Sasa mwanaume akimshika mabega mtu mwingine ionekane ametolewa dhababu tunasema. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana kwenye jambo hili kama Taifa tuwe *serious* sana kwenye mambo ya hovyo kwa maana ya kwamba jambo hili linatuumiza. Jambo hili limesababisha ndugu zetu wameuawa, wamejeruhiwa kwa sababu ya mambo ya hovyo. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. FAGASON A. NKINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba unipe dakika moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nilizungumzie hili jambo la nyeti. Jambo hili la nyeti, niwaombe hata Mawaziri, jambo hili ni kubwa, jambo hili linadhalilisha Taifa. Leo tunakaa kujadili… *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. FAGASON A. NKINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Alan Thomas Mvano, wajiandae Mheshimiwa Janeth Peter Pinda, Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga na Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa nafasi hii. Awali ya yote kwa kuwa nami ni mara ya kwanza ninasimama mbele ya Bunge hili Tukufu, ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu ambaye ameendelea kutujalia kheri na afya njema sisi wote ambao tuko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii vilevile, kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwanza kabisa kwa kuaminiwa na Watanzania

kwa kupigiwa kura nyingi za kishindo na kwa ushindi mkubwa alioupata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikishukuru Chama Cha Mapinduzi kwa kuniteua chini ya vikao alivyoviongoza yeye mwenyewe. Mimi ndugu yenu, kusimama na kuomba ridhaa kwa wananchi wa Kakonko na ninawashkuru sana wananchi wa Kakonko kwa kuniamini na kunichagua ili niweze kuwawakilisha katika Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ahadi yangu ni kwamba sitowaangusha, nitafanya kazi usiku na mchana kwa nguvu zangu zote na kwa akili yangu yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa vilevile, kupongeza kazi kubwa ambayo anaifanya Mheshimiwa Rais wetu. Sisi kule Kakonko na Mkoa wa Kigoma kwa ujumla, niseme Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ametupatia heshima kubwa sana wananchi wa Mkoa wa Kigoma. Hii ni kwa sababu miaka ya nyuma watu walikuwa wanaichukulia Kigoma kama eneo ambalo halifai. Watu walikuwa wanaamini watumishi ambao wanafanya vibaya Serikalini wakipelekwa Kigoma maana yake wamepewa adhabu, lakini leo Mheshimiwa Rais huyu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameionesha heshima ya wananchi wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu miaka ya nyuma hatukuwa tumeunganishwa na barabara za lami kuelekea mikoa mingine, lakini leo ukitoka Mwanza, ukitoka Dar es Salaam, ukitoka Tabora, ukitoka kona yoyote ya nchi hii ukienda Kigoma utafika kwa barabara za lami, huyo ndiye Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya Kakonko, kwa miaka minne ambayo Mheshimiwa Rais wetu aliongoza Taifa hili, kipindi kile cha kwanza alituletea fedha nyingi za maendeleo jumla ya fedha alizozileta ni shilingi 28,910,712,714.65. Ninaomba Mheshimiwa Rais huyu apokee shukurani nyingi sana kutoka kwa wananchi wa Kakonko. Ndiyo maana tuliona hospitali ya wilaya ilijengwa, stendi mpya ya kisasa ikajengwa, chuo cha *VETA* kikajengwa, barabara

zikajengwa, shukrani nyingi sana na pongezi nyingi sana zimwendee Mheshimiwa Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitumie nafasi hii kuwapongeza viongozi wote wanaomsaidia Mheshimiwa Rais wetu. Kwa nafasi ya pekee nimpongeze sana Waziri Mkuu wetu, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba anafanya kazi kubwa sana. Wasilisho alililoleta hapa kwetu linaonesha namba ambavyo tunaona matumaini makubwa katika Taifa letu na nimesimama hapa kwa kweli kumtia moyo na kuwaambia Watanzania kwamba, Serikali tuliyonayo na viongozi tulionao, Mawaziri tulionao na Naibu Mawaziri tulionao, wanafanya kazi kubwa sana, wanapaswa kutiwa moyo ili waendelee kufanya kazi kwa moyo wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi hiki kifupi, ninaendelea kutoa shukurani kwa Serikali yetu hii. Mwaka huu Wilaya yetu ya Kakonko imepokea jumla ya watumishi 142. Serikali yetu hii imefanya kazi kubwa sana, ninamshukuru sana na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ametuletea mbegu ya ruzuku ya alizeti tani 10 kwa kipindi kifupi hiki. Vilevile, tunashuhudia ujenzi wa soko la kisasa katika Wilaya yetu ya Kakonko. Hayo ni mambo ambayo lazima niyaseme ili Watanzania wajue kazi kubwa ambayo Serikali yetu inafanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo hayo, nimekuwa nikifuatilia michango ya Wabunge wengine na kwa kweli nimejifunza mengi na nimesimama hapa kusema kwamba, pamoja na mambo mengine yote, bajeti iliyowasilishwa kwetu na mipango iliyowasilishwa inaonesha namna ambavyo Taifa letu linakwenda kuzalisha kwa kiwango kikubwa mazao ya kilimo, mazao ya uvuvi, kwenye utalii na sekta nyingine za uzalishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili tuweze kufika huko tunahitaji fedha. Kwanza kabisa lazima tukubali kwamba, fedha tunazozipata kutoka kwenye makusanyo lazima zitumike vizuri kwa uwazi na kwa uwajibikaji. Wale wote ambao hawatatumia fedha zetu vizuri lazima wachukuliwe hatua ili fedha zote zinazopatikana kutoka kwenye sekta zote ziweze kuelekezwa kwenye maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Wilaya ya Kakonko yapo mambo ambayo tunatamani kuona yanafanyika. Kwenye upande wa afya, tunatamani kuona kata saba ambazo hazina vituo vya afya nazo zinapata vituo vya afya, lakini vilevile, tunatamani kuona maeneo yale yaliyotengwa kwa ajili ya chuo cha uuguzi, basi chuo hicho kikaanzishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kilimo vilevile, tunatamani kuona tunakuwa na kiwanda cha kuchakata zao la muhogo. Vilevile, tuone kwamba ile miundombinu ya umwagiliaji ambayo imechakaa ifanyiwe kazi ili wakulima wetu waweze kuzalisha katika misimu yote. Vilevile, tumetenga ekari zaidi ya 1,000 kwa ajili ya kilimo cha parachichi, tunatamani kuona eneo hilo linaendelezwa ili mambo yaweze kwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye upande wa barabara mvua zilizonyesha zimeathiri sana maeneo yetu, watu wa Itumbiko, Katanga na Njoomulole wanashindwa kufanya shughuli zao kwa sababu mvua zimeharibu miundombinu ya barabara. Kwa hiyo, maeneo yote hayo yanahitaji fedha ili wananchi wetu waweze kufanya shughuli zao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mkoa wa Kigoma yapo mambo tunatamani kuona yanafanyika. Kwanza kabisa, tuna reli ya kisasa ambayo mradi wa ujenzi unaendelea *lot six*, tunatamani kuona Serikali imeweka kipaumbele katika eneo hilo ili tuweze kukuza biashara na nchi za jirani zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Ziwa Tanganyika ni ziwa la kimkakati, tunahitaji kuona tunakuwa na meli nzuri kwa ajili ya kusafirisha watu wetu. Tumeshuhudia siku chache zilizopita watu nane wamepoteza maisha, lazima kama Taifa tuweke meli nzuri kule ili watu wetu waweze kusafiri vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba uniruhusu nitoe mapendekezo yangu kwa bajeti hii…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. ALAN T. MVANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Janeth Peter Pinda, wajiandae Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga, Mheshimiwa Ado Shaibu Ado na Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo.

**MHE. JANETH P. PINDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia kwa siku hii ya leo, lakini kabla sijaendelea ninaomba sana nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenipa afya njema mpaka siku hii ya leo nami kuweza kuchangia katika Bunge lako hili Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii pia kumshukuru sana Mama yangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo amekuwa akisimamia shughuli za maendeleo na kutufanya sisi wananchi tuishi katika amani, lakini tukikua kiuchumi siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi ambavyo anamsaidia Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutekeleza shughuli za Serikali. Nimemfahamu vizuri Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba alivyokuja kwenye ziara kule Katavi. Amekuwa akifanya kazi nzuri sana na kutatua changamoto za wananchi mbalimbali *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii pia, kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa kuniamini, lakini pia Chama changu Cha Mapinduzi kwa kunipa ridhaa ya kuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Katavi na kuweza kuwawakilisha wananchi wa Mkoa wa Katavi katika Bunge hili. Ninawaahidi kwamba

nitashirikiana na Wabunge wenzangu kuhakikisha changamoto zote tunazifikisha kwa Serikali ili waweze kuzitatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza sana mama yangu Mwanamvua Mrindoko, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, kwa namna ambavyo akisimamia shughuli za maendeleo na uchumi za Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja sasa katika kuchangia hotuba ya bajeti ya Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mkoa wetu wa Katavi ni mkoa wa kimkakati, ni mkoa unaokua kiuchumi siku hadi siku, lakini Mkoa ule wa Katavi hauna barabara za kuunganisha mikoa, zaidi ya barabara ile ya Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo imetoa pesa kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami kwa kiasi cha kilometa. Niwaombe sana wale wanaozisimamia, mamlaka hizo waweze kuharakisha mipango hii ya ujenzi wa barabara ili iweze kukamilika kwa wakati ili wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kunufaika kwa barabara hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali pia, kwa zile barabara za ndani, ninaendelea kusisitiza kwamba Mkoa wa Katavi bado hatuna barabara, niiombe Serikali ituongezee pesa kwa ajili ya zile barabara za *TARURA* ili wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kunufaika na kuweza kujiendeleza zaidi kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende moja kwa moja kwenye suala zima la afya. Tunaishukuru sana Serikali kwa namna ambavyo imekuwa ikiboresha hasa miundombinu ya afya. Tumepata Hospitali kubwa sana ya Mkoa ambayo inahudumia wananchi wa Mkoa wa Katavi, lakini haina uzio, pia na hospitali zetu za wilaya. Ninapenda kuitetea Hospitali ya Wilaya ya Mlele, tumepata hospitali nzuri, lakini haina uzio, ninaomba mamlaka zinazohusika ziweze kutusaidia ili hospitali ile iweze kupata uzio. Kituo cha Afya cha Usevya nacho hakina uzio, ninaiomba Serikali kuweza kukipatia uzio kituo hicho cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda moja kwa moja katika Kituo cha Afya Chamalendi, tunaishukuru Serikali imeweza kutoa pesa za ujenzi, lakini ujenzi wake unaenda taratibu sana kiasi ambacho wananchi wa Chamalendi wanapata changamoto kubwa katika suala zima la matibabu, hasa pale wanapohitaji masuala ya upasuaji, na kadhalika. Ninaomba wale ambao wanaendelea kusimamia eneo hilo la ujenzi waweze kuharakisha ujenzi huo, ili wananchi wa Chamalendi waweze kupata huduma hizo za afya kwa uharaka na zenye uhakika. Ninaomba pia, katika Kituo cha Afya cha Kibaoni, tunashukuru tumepata Kituo cha Afya kule Kibaoni, Mpimbwi, lakini hakina huduma za mionzi, kama *x-ray* na *ultrasound*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimetoka kuzungumzia suala la shida za barabara. Wananchi tunaozunguka maeneo yale kikiwemo Kituo hicho cha Chamalendi tunapata shida kuitafuta au kuifikia hospitali ya Wilaya, kwa ajili ya kupata huduma za mionzi. Ninaomba zile mamlaka zinazohusika basi ziweze kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaenda moja kwa moja katika suala la uwekezaji, kama nilivyozungumza kwamba, Mkoa wa Katavi ni wa kimkakati, unakua kiuchumi siku hadi siku. Mkoa wetu wa Katavi una madini na wananchi wengi kutoka sehemu mbalimbali, wageni kutoka nchi mbalimbali wanafika Mkoa wa Katavi; basi ninaiomba Serikali kuweka vizuri Sheria ya Utoaji wa Leseni za Uchimbaji. Zitolewe baada ya kujiridhisha kuwa, hao waliopo katika ardhi hiyo ndiyo hasa wahusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itapunguza migogoro pamoja na malalamiko, hasa migogoro ya ardhi, katika eneo hilohilo la uchimbaji wa madini. Ninaomba sana wale wachimbaji wadogowadogo basi waweze kutambulika, lakini pia, ikiwezekana na wenyewe waweze kupewa elimu zinazohusiana na shughuli nzima za uchimbaji wa madini, hii itasaidia kuondoa migogoro na malalamiko. Ninachukua nafasi hii sasa kuiomba Serikali kusimamia eneo hilo la uchimbaji wa madini, wale waliopewa leseni za uchimbaji wa madini kuangalia wasiende kuchimba karibu na vyanzo vya maji au mito. Hii itasaidia

kuepusha uharibifu wa miundombinu, lakini hasa madhara ya viumbe hai wakiwepo binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mambo mengi, ninaomba tu niyawasilishe hayo kwa leo. Hivyo, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Musa Godfrey Mbuga na Mheshimiwa Ado Shaibu Ado ajiandae.

**MHE. MUSA G. MBUGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi ya kuchangia hotuba hii. Ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniazima uhai na ninaendelea kumwomba aendelee kuniazima ninapotimiza majukumu ya Wana-Kisesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapoelekea kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ninaanza kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu, kwanza kwa fedha nyingi ambazo amezileta kwetu Kisesa na kwa maendeleo makubwa. Muda hauwezi kutosha kuelezea moja baada ya lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia wasaidizi wake; Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Nchimbi, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Waheshimiwa Mawaziri wote. Ninawapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri kwa sababu, kwanza wamekuwa ni wasikivu, wanatupa muda wa kutusikiliza na wanatatua kero zetu. Kwa hiyo, Waheshimiwa Mawaziri tunawashukuru na tunawapongeza sana pamoja na Waheshimiwa Manaibu Waziri wote. Hotuba yetu au ya Mheshimiwa Waziri Mkuu imeeleza utekelezaji wa 2025/2026 na imeeleza mwelekeo wa Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mambo machache ya kushauri kutoka kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Ni hotuba ambayo imesheheni mahitaji ya Watanzania na ni hotuba, ambayo inajibu hoja na haja nyingi sana za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwenye suala la uratibu wa maafa. Pamoja na mambo mengi mazuri ambayo yameelezwa

kwenye hotuba, ninalo jambo la kushauri kwenye uratibu wa maafa ambayo kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni Ukurasa wa 95. Tumekuwa tunapitia maafa mengi na hata Jimboni kwangu Kisesa baada ya mvua hizi nyingi kutokea na hatuwezi kumlaumu yeyote, hizi mvua zilizonyesha ni baraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi baraka zimekuja na changamoto, Malaika wa awamu hii nadhani alipoambiwa kwenda kufungulia maji akafungulia zaidi ya kiwango kwa hiyo, kwa Kisesa ikaleta shida kubwa; yapo maafa makubwa maeneo mbalimbali, kwa mfano Kijiji cha Nh'anga na sehemu zingine nyingi. Sasa zinapotokea changamoto kama hizi tunajua upo Mfuko wa Maafa ambao uko chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini hauna bajeti ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wetu wa Mkoa, pamoja na *DC;* kwanza ninawashukuru na ninawapongeza, Mheshimiwa Namlingi Macha pamoja na dada yangu Fauzia Ngatumbura. Wamekuwa wanajituma sana kwenye mambo mengi, lakini changamoto ni linapokuja suala la maafa bajeti haitoshi. Kwa hiyo, hata mwananchi anapopata shida ni suala la kwenda kumpa pole, lakini pole inasaidiaje wakati mtu hana chakula? Pole inasaidiaje mtu hana pa kujihifadhi? Kwa hiyo, ninaishauri Serikali, ninaishauri Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, iongeze bajeti kwenye kipengele cha maafa, ili zinapotokea changamoto kama hizi iweze kuwa rahisi kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu nyingine ambayo ninataka nishauri ni suala la maendeleo ya vijana, ambayo kwenye hotuba iko ukurasa wa 84, maendeleo ya vijana; Serikali ya Awamu ya Sita imechukua hatua madhubuti kabisa ikaanzisha Wizara maalum ya Vijana na tumeona hatua mbalimbali ambazo zimetolewa ikiwa ni pamoja na hii mikopo ya shilingi bilioni 200, kwa ajili ya vijana na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu ambacho ninataka niishauri Serikali ni hizi fedha, ukiangalia zimetawanywa kwenye Wizara mbalimbali, zipo zilizoenda Wizara ya Mifugo tumeona wametoa shilingi bilioni saba na kitu, zipo zilizoenda kwenye Wizara ya Uvuvi huko na Kilimo na

sehemu mbalimbali. Ninashauri hizi fedha zingekuwa *centralized* sehemu moja, pawepo na *one stop center,* kama ambavyo *REA* wamefanya kwenye ule mradi wa kujenga *petrol station* vijijini fedha zote zimepelekwa Azania kwa hiyo, yeyote anayetaka kujenga *petrol station* vijijini anaenda *REA,* anapata maelekezo, ana-*comply* na *EWURA,* anakutana na fedha Azania, inaondoa milolongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri pia, kwenye suala la maendeleo ya vijana hizi fedha zinazotolewa, kwa ajili ya wanawake, kwa ajili ya vijana, ziwe sehemu moja ambapo mwananchi anapokwenda anakutana na huduma zote. Pamoja na kwamba Wizara ya Vijana haina *technical team* ya kutosha, wanaweza wakachukuliwa wataalam kutoka Wizara ya Mifugo, Wizara ya Kilimo na Wizara zingine wakapelekwa kwenye Wizara ya Vijana, ili kijana wa Kitanzania anapojkwenda kuomba mkopo akutane na huduma zote. Sehemu moja inaondoa mkanganyiko, inaondoa tafsiri mbalimbali kwa hiyo, ninashauri suala la hii mikopo ya shilingi bilioni 200 iwe sehemu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ninaishauri Serikali ni kilimo. Serikali imefanya vizuri sana kwenye mambo mengi. Ninajikita kwenye kilimo cha pamba maana wananchi wangu wa Kisesa ni walimaji wakubwa wa pamba na kilimo, kwenye hotuba yetu, kiko *page* ya 24 na 25.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya juhudi kubwa kwenye zao la pamba ikaanzisha kilimo cha mkataba, *contract farming,* lengo ni kuleta tija kwenye kilimo, kwa maana ya Mfumo wa *BBT*. Changamoto ya huu mfumo inakuja inapofika kwenye suala la ununuzi; suala la kuwa na mnunuzi mmoja linaondoa ushindani. Ni kweli, bei ya pamba ni suala la *global, it's a global price* kwa hiyo, inakuwa *determined* na *market force*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, panapokuwa na ushindani kwenye ununuzi hata bei inapokuwa imeshuka ni rahisi kwa mwananchi, ni rahisi kwa mkulima kuamini kuwa, bei imeshuka kuliko panapokuwa na mnunuzi mmoja. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali, kwenye hiki kilimo cha mkataba waangalie *component* ya kuwa na wanunuzi wengi kuliko

kata nzima kuwa na mnunuzi mmoja na ukiangalia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. MUSA G. MBUGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana, ninamalizia. Ukiangalia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ameeleza jinsi ambavyo wananchi wamekuwa wanakopa fedha zao kwa hiyo, ikiwa wataboresha hii sehemu tutaondoa hayo yote. Muda ungetosha ningeeleza mambo ya Tembwa, lakini itoshe tu kusema ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante sana kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, ajiandae Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, ajiandae na Mheshimiwa Margaret Mwanza Sitta.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona, ili niweze kutoa mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nina imani kwamba, kutokana na nafasi yetu tumekuwa tunapewa hapa uwiano wa kuchangia; kwa siku sisi *ACT* tumeambiwa, kwa nafasi yetu ya Waheshimiwa Wabunge tisa, tuna nafasi ya kuchangia angalau mchangiaji mmoja kwa siku, huwa tunapewa hivi kutoka Ofisi ya Katibu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naona hizi ni dakika za jioni, isije ikahesabiwa dakika za jioni tukakatwa juu kwa juu tukashindwa kujipambanua. Ule msingi wa kwamba, nafasi yetu ya kuchangia mchangiaji mmoja izingatiwe, ili Bunge lipate kusikia mawazo yetu pia. Nimepata faida ya kuwasikia wachangiaji wenzangu, Waheshimiwa Wabunge na wengi wamejikita katika kuchambua hoja mbalimbali ambazo zipo katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, lakini mimi nitachukua njia tofauti nikitambua kwamba, Hotuba ya Waziri Mkuu katika Bunge la Bajeti siyo hotuba ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii siyo hotuba ya kisekta, hii siyo hotuba itayojikita kwenye maduhuli tu ya Serikali na namna ya kuyatumia.

Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ndani yake inabeba tafakuri ya mwaka uliopita wa fedha. Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inabeba maono ya Serikali katika mwaka ujao wa fedha kwa hiyo, mimi nitajielekeza katika maeneo ambayo kwa maoni yangu yamebeba ukimya mkubwa sana katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Yako maoni, yako maeneo, mimi ninaona yalipaswa kuwemo kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu au yalipaswa kupewa uzito wa kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona hotuba hii imebeba ukimya katika maeneo hayo na kwa ajili ya muda nitayataja machache. Eneo la kwanza, nimesoma Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kurasa zote 122; sijaona kwenye ukurasa wowote, sijaona kwenye aya yoyote, sijaona kwenye sentensi yoyote, kuhusu Katiba Mpya, Tume Huru ya Uchaguzi na mageuzi ya kisiasa nchini kwetu. Hatua hii ya Hotuba ya Waziri Mkuu kukaa kimya juu ya jambo hili muhimu sana sisi tunaipa tafsiri kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho ninalolijenga mimi, mpaka nitapokuwa *proved wrong* wakati ujao, hii inanipa ishara kwamba, Serikali imeipuuza, hailipi uzito na haitaki ajenda ya Katiba Mpya, huo ndiyo msimamo wangu. Sasa ninatoa ujumbe kwa Serikali na Chama Cha Mapinduzi, ujumbe wa kwanza ni Watanzania si wajinga wanaelewa hali halisi ya kisiasa ya nchi yetu na wanajua bila Katiba Mpya, bila Tume ya Uchaguzi na bila mageuzi ya kisiasa ndani ya nchi yetu…

**MHE. ESTER A. BULAYA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado, kuna Taarifa.

Mheshimiwa Ester Bulaya.

## TAARIFA

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru tu kwa mchango wake, Mheshimiwa Ado, mdogo wangu na mimi nilikaa sana hapo. Ninaomba nimpe Taarifa kwamba, kwenye Ilani ya

Chama Cha Mapinduzi chini ya Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumedhamiria ndani ya miaka hii mitano ya Awamu ya Sita Watanzania watapata Katiba Mpya. Ukimuangalia anavyozungumzia suala la Katiba Mpya amemaanisha, ndiyo maana kwenye ilani ya chama chetu tumeiweka. Ninaomba nimpe hiyo Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa unaipokea Taarifa hii?

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa nyingine.

**MHE. ADO S. ADO**: Mheshimiwa mwenyekiti, Taarifa ya Mheshimiwa Bulaya siipokei. Siipokei kupitia hoja yangu namba mbili, ambayo ninaelekea kuitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujumbe wangu kwa Serikali na Chama Cha Mapinduzi, ujumbe namba mbili, Katiba Mpya sio ajenda ya CCM, Katiba Mpya sio ajenda ya Serikali, Katiba Mpya ni ajenda na mali ya Watanzania. Ukimya huu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu unamaanisha Serikali imeihodhi ajenda hii.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado, kuna Taarifa. Mtoa Taarifa yuko wapi? Sawa, Naibu Waziri.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumpa Taarifa Mheshimiwa Ado kwamba, Serikali iliyopo madarakani ni ya Chama Cha Mapinduzi na inatekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa hiyo, hakuna namna utatofautisha Chama Cha Mapinduzi na Serikali iliyoko madarakani na Watanzania. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado, unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa mwenyekiti, siipokei Taarifa hiyo. Sijasema Serikali ni mali ya nani, hilo ni somo lingine la Katiba, mkufunzi yuko pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema Katiba Mpya ni mali ya Watanzania. Watanzania wana haki kwenye hotuba kama hizi zinazobeba maono, kujua mchakato wao wa Katiba Mpya unakwenda wapi.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Inatoka wapi Taarifa. Ndiyo, Mheshimiwa Kihenzile.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakubaliana na Mheshimiwa mchangiaji kwamba, Katiba Mpya ni mali ya Watanzania, lakini pia ninamkumbusha mali za Watanzania ni pamoja na ardhi, fedha na vinginevyo. Kwa sasa mwenye mkataba wa kuvisimamia ni Serikali na Serikali ya sasa ni ya CCM kwa hiyo, huwezi kuvitenganisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, siipokei taarifa hiyo. Kwa sababu ninaona nakwamishwa kwamishwa hapa, gari lina nasanasa niiache ajenda hiyo ujumbe umefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajenda ya pili ambayo ninaona ni ukimya kwenye hotuba ya Waziri Mkuu ni vita dhidi ya ufisadi, rushwa na ubadhirifu. Sijaona kama imepewa kishindo kinachostahili. Ninaamini Hayati Sokoine angefufuka leo wala nisingepata shida kujua ajenda yake namba moja ingekuwa ni ajenda gani. Ninafahamu... *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa, niko hapa taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumpa taarifa Mheshimiwa Ado kwamba, unapozungumzia mtu ambaye tangu ameapa, tangu tumemdhibitisha kwenye Bunge hili kwa kinywa chake, kwa vitendo kuzungumzia masuala ya ufisadi na kukemea ubadhirifu na kukemea uzembe ni Waziri Mkuu Dkt. Mwigulu Nchemba. Kwenye hotuba yake Waziri Mkuu amesema Serikali ya Awamu ya Sita chini yake yeye, kama Msimamizi Mkuu wa Serikali atahakikisha wazembe, wabadhirifu watachukuliwa hatua na wananchi wa Tanzania waweze kupata maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana mdogo wangu leo alikuwa hajajiandaa kuchangia. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ADO S. ADO:** Siipokei taarifa hiyo. Mimi ninafahamu rejea ya uchambuzi, ni hotuba ya Waziri Mkuu. Ninaweza kumweleza Waziri Mkuu wapi amezungumzia juu ya rushwa na ufisadi. Alizungumzia ripoti ya *CAG* na *commitment* ya Serikali, kwa maoni yangu mimi, Waziri Mkuu hajatoa uzito unaostahili kwenye hotuba yake kwa ajenda ya rushwa na ufisadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uniruhusu nitoe mfano tu nimepigwa breki sana hapa.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado kuna taarifa. Kanuni zetu zinaruhusu. Kuna taarifa ninaomba uipokee.

**TAARIFA**

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpe taarifa mzungumzaji rafiki yangu Mheshimiwa Ado, ninadhani atakuwa hajaisoma vizuri hotuba ya Waziri Mkuu. Ukisoma hotuba ya Waziri Mkuu kwenye eneo lote alilozungumzia utekelezaji wa shughuli za Serikali ameeleza kuhusu vita dhidi ya rushwa na ufisadi kwa ujumla, lakini ameeleza kwenye maeneo mahsusi.

Mheshimiwa Mwenyekiyi, Waziri Mkuu alipozungumza kuhusu ripoti ya *CAG* amesema, alipozungumza kuhusu kasi ya kuongeza ukusanyaji wa mapato amesema, kuhusu kuzuia kuvuja kwa mapato, hiyo ndiyo lugha ambayo Waziri Mkuu amesema *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri Mkuu ya masaa mawili lisaa limoja asingeweza kusema kila kitu, huwezi kumpangia aiseme kwa namna gani, lakini Waziri Mkuu ameisema na ujumbe umeenda nasi kama Wabunge tunatakiwa tuifanyie kazi hotuba ya Waziri Mkuu. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado ninakupa nafasi upokee taarifa hiyo na muda wako pia umekwisha.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawaacha kwa tafakuri ndogo tu na ninaomba unitendee haki kwa dakika moja tu halafu mtaona kama mimi nilikuwa naelekea wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazingira ya sasa ambayo tunapokea taarifa kwamba Serikali imeingia katika mtindo wa kuwa na makubaliano ya pembeni nje ya Mahakama za Kimataifa kuwalipa wanaotudai mabilioni ya fedha, mazingira ambayo yana harufu ya ufisadi, kwa mfano malipo ya bilioni zinazofikia 268 kwa Benki *ya Standard Charter* ambayo hiyo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ado muda wako ulishaisha.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuhusu taarifa na muda, mimi ninavyoyaona mazingira ya ufisadi nchini sijaridhika na uzito ambao Waziri Mkuu ameuweka kwenye hotuba

yake kwa ajenda ya ufisadi, mengine tutachangia kwa maandishi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo na Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta ajiandae.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia ya hotuba ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na dunia kwa kutujalia uhai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitumie nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri ambazo anazifanya kwenye Taifa letu la Tanzania pamoja na Makamu wake Balozi Dkt. Nchimbi. Ninapenda pia kuwashukuru wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa ushirikiano wanaonipa. Ninapenda nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu Dkt. Lameck Nchemba na Mawaziri wote ambao wameteuliwa kwenye nafasi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nichangie hoja na hotuba ya Waziri Mkuu ambayo imesheheni pia mambo mbalimbali ya TAMISEMI na mambo mbalimbali yanayohusu nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2023 niliwahi kusimama hapa Bungeni nikasema kwamba kwenye Mkoa wetu wa Katavi tuna upungufu wa madarasa, madawati pamoja na vyoo. Tatizo hilo kwenye Mkoa wa Katavi bado ni tatizo kubwa kwenye shule za msingi, tukiwa tunakwenda sasa kuwa na shule za ufundi ambazo ni shule za amali kwenye Taifa letu la Tanzania, lakini tukiwa tumebadilisha sera ya nchi yetu ya Tanzania kwamba elimu ya shule ya msingi ni kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la sita pia mpaka darasa la 12. Mkoa wetu wa Katavi bado unakabiliwa na upungufu wa madawati, madarasa pamoja na matundu ya vyoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nizitaje takwimu kwa sababu zinatisha. Kwenye Mkoa wetu wa Katavi tuna upungufu wa wa

madarasa, tunao uhitaji wa madarasa tunahitaji wa madarasa 6,671, lakini sasa hivi tuna madarasa 2,866, tunao upungufu wa madarasa 3,205. Pamoja na upungufu wa hayo madarasa tunao pia upungufu mkubwa wa madawati kwenye Mkoa wetu wa Katavi. Tuna uhitaji wa madawati 87,681 lakini kwa sasa hivi tuna madawati 61,332 na kuleta upungufu wa madawati 27,348.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mkoa wetu wa Katavi tunao uhitaji wa matundu ya vyoo 9,122. Kwa sasa hivi, tuna matundu ya vyoo 3,762 na tuna upungufu wa matundu ya vyoo 3,762. Ukiangalia hoja ya elimu kwenye Mkoa wetu wa Katavi ukichukua upungufu wa madarasa, upungufu wa madawati na upungufu wa matundu ya vyoo, unakuta kwamba Mkoa unahitaji kupata madawati, kupata hayo matundu ya vyoo na kupata madarasa ili Mkoa wetu wa Katavi uende sambamba na mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali iweze kuwahimiza Halmashauri zilizoko kwenye Mkoa wetu wa Katavi nikiwa na maana Halmashauri ya Mlele, Halmashauri ya Tanganyika, Halmashauri ya Mpimbwe pamoja na Manispaa ya Mpanda kutoa tarehe maalum, lakini kutoa ratiba maalum kwenye hizo halmashauri ili ziweze kutengeneza hayo madawati na kukamilisha matundu ya choo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaweza nikatolea mfano shule ambazo zipo pale Mpanda Mjini katikati ya kitovu cha Mkoa wa Katavi ambazo zina wanafunzi ambao wamezidi. Tunayo Shule ya Nsemulwa ambayo inao wanafunzi takribani 1,523, lakini ina walimu 16, ina madawati 102. Unaangalia jinsi watoto wanavyobanana darasani. Watoto wanakaa takriban 191 mpaka 200 kwenye darasa moja. Tunazo Shule za Msakila zina wanafunzi takribani zaidi ya 2,000 lakini watoto wanaokaa kwenye shule hiyo watoto 100 mpaka 200. Ninaomba mambo haya yachukuliwe kwa uzito ili Mkoa wetu wa Katavi uende sambamba na Mikoa mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumza hapa ni suala la halmashauri nchini kwetu Tanzania ambazo zimejitengenezea kitega uchumi cha kujenga Shule za *English medium*. Imezuka tabia kwenye halmashauri nyingi nchini kwetu

Tanzania kuweka kitega uchumi cha kujenga Shule ya *English medium* ilhali inatumia walimu wanaolipwa na Serikali, lakini pia inawachukua wale walimu wazuri na kuwapeleka kwenye shule hizo na kusema kwamba wametengeneza kitega uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo Halmashauri zaidi ya 40 nchini kwetu Tanzania zinafundisha elimu ya msingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Ahsante naomba dakika moja. Zinafundisha elimu ya msingi kuanzia darasa la kwanza mpaka la saba kwa lugha ya Kiingereza, lakini sera ya elimu nchini kwetu Tanzania inasema nini? Inasema kwamba elimu ya msingi kutoka darasa la kwanza mpaka la sita au la saba inatakiwa ifundishwe kwa lugha ya Kiswahili. Je wanafuata sera gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta na tutamalizia na Mheshimiwa Joseph Enock Tama.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili nichangie hoja iliyoko mezani. Kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai, lakini pia ninawashukuru sana wananchi wa Urambo na familia yangu kwa *support* wanayonipa ambayo imeniwezesha kufanya kazi mpaka wakati huo. Nichukue pia nafasi hii kuipongeza sana Serikali inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo wametupa miradi mikubwa Urambo ikiwemo Kituo cha Kupozea Umeme, Mradi wa Maji ambao unaendelea, Shule na kadhalika. Tunaishukuru sana Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mazuri yote yanayofanywa pamoja na TAMISEMI ambayo Waziri wake Mheshimiwa Shemdoe anafanya kazi nzuri akisaidiana na Naibu Mawaziri na Wakuu wa Idara

wote, kwa kweli pamoja na shukrani, lakini bado tunarudi kwao kwa ajili ya maombi maalum kwa niaba ya wananchi wa Urambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Urambo tunategemea sana kilimo hasa cha tumbaku, mahindi na kadhalika, kwa hiyo tunahitaji barabara imara vijijini. Kazi ya *TARURA* ni nzuri, lakini tunaomba iongezewe ipewe uwezo zaidi ili barabara za vijijini ziweze kubeba mazao yetu kuyapeleka kwenye soko. Pia nichukue nafasi hii kuishukuru *TANROADS* kwa kazi kubwa inayofanya, lakini na yenyewe tunaiomba pia iimarishe barabara zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Tabora katika Wilaya ya Urambo, Ulyankulu, Kaliua na Sikonge tuunganishwe na barabara ya lami ili tuweze kupeleka mazao yetu kwa utaratibu ambao utatusaidia kubadilishana mazao na kuinua uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Urambo tuna changamoto pia kwa upande wa shule. Serikali yetu imefanya kazi kubwa sana lakini kuna shule kwa mfano ya mjini inayoitwa Shule ya Ukombozi ambayo ina wanafunzi 1,600. Tunaomba Serikali yetu itupe shule nyingine Urambo Mjini kwenye Kata ya Urambo ili wanafunzi 1,600 wapungue wapate shule nyingine. Hali kadhalika, tunaomba shule ya msingi ijengwe sehemu ya Imara Makoe ambayo wanafunzi wanashindwa kwenda shule ambayo iko kilometa nne kutoka pale walipo, wakitaka mbadala inabidi wavuke barabara ya kwenda Kigoma ambayo ni hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningeomba sana pia kwa upande wa afya hospitali yetu ya Wilaya ya Urambo jengo la utawala ambalo liko karibu na jengo la dharura halijakamilika. Tunaomba tusaidiwe ni zaidi ya milioni 250 ambazo zinahitajika ili tuwe na jengo la utawala karibu na jengo la dharura. Wakati huo huo ninaomba, kuna Kata moja inaitwa Uyogo ambayo iko na kilometa 59 kutoka mjini tunaomba na yenyewe ipatiwe kituo cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudi kwa upande wa wafanyakazi hasa nikiwalenga walimu, ninaiomba Serikali kwa mara ya ngapi sijui, bado kuna haja ya kuangalia *TSC* inavyofanya kazi. *TSC* iliundwa kwa

Sheria Namba 25 mwaka 2015, bado haina hela za kutosha, bado wafanyakazi hawatoshi, lakini kazi yake iliyoundiwa ya kufanya kazi ya ajira, maadili na maendeleo ya wafanyakazi haifanyi kazi vizuri. Ninaomba kwa heshima na taadhima Serikali iangalie Tume ya Utumishi wa Walimu *TSC* ili ifanye kazi iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukulie pia kwa upande wa wafanyakazi wote kwa ujumla, ninaomba sana walimu na wafanyakazi wengine wa afya na kadhalika wanapomaliza muda wao wa kazi yaani wanapokaribia kustaafu, wanapata tabu sana kwa sababu mishahara yao inakuwa haijarekebishwa hasa wale waliopanda madaraja. Hivi ninavyoongea hapa nina Walimu 20 na wafanyakazi wengine ambao wamestaafu bila kurekebishiwa mishahara yao. Kwa hiyo inawapa shida sana wakati wa kupata *pension*. Kwa hiyo, tunaomba sana mfanyakazi yeyote yule kabla hajastaafu, mshahara wake uwe umerekebishwa ili kumsaidia aweze kupata *pension* kwa uzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo kuwaacha wafanyakazi wanahangaika baada ya kufanya kazi kubwa ya kutumikia ndani ya nchi yetu inakuwa siyo vizuri wasaidiwe waweze kupata haki zao kwa wakati mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninashukuru sana, lakini watusaidie sisi hasa tunaotoka vijijini tupatiwe kwa kweli barabara nzuri. Ninarudia tena barabara nzuri! *TARURA* wanafanya kazi nzuri sana, *TANROADS* wanafanya kazi nzuri sana, lakini waongeze fedha ili ziweze kuwasaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa suala la wajasiriamali. Tumeongelea hapa kuhusu akina mama kupewa mikopo, vijana kupewa mikopo, lakini kama hatutapata elimu ya ujasiriamali kwanza kabla hawajawapa hizi fedha, inakuwa shida sana. Kwa hiyo, ninafikiri Maafisa Maendeleo wawezeshwe kutembea kutoa elimu kwa hawa vijana wenye ulemavu pamoja na wanawake ili wanapopata fedha elimu ya uendeshaji wa shughuli zao za kiuchumi waweze kuzimudu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Joseph Enock Tama atakuwa mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

**MHE. JOSEPH E. TAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye amenipatia fursa ya kuiona siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa sababu ni mara yangu ya kwanza kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kaliua kwa kuniamini na kunichagua niwe mwakilishi wao humu Bungeni, hakika ninawaahidi kwamba, nitakuwa mwakilishi mwema kwa sababu ninazo sababu alizonipatia Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa miradi na fedha nyingi alizozileta kwenye Jimbo letu la Kaliua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi, kwa sababu ukienda kwenye sekta ya umeme nishati tumeletewa umeme vitongoji takribani 22 na ninaamini ndani ya mwaka huu kabla hujaisha tutaongezewa vingine na maisha yetu tutaendelea kutabasamu kama jinsi ambavyo Majimbo mengine wameendelea kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye upande wa maji, ninaamini kabla ya mwaka kwisha wananchi wangu wa Jimbo la Kaliua watakunywa maji kutoka Ziwa Victoria na tutaendelea kutabasamu, hakika tunaendelea kumwombea kwa Mwenyezi Mungu, Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu, niseme mambo machache kwenye sekta ya afya. Ninafahamu Serikali imefanya kazi kubwa kwenye Jimbo letu la Kaliua. Tumepata hospitali ya wilaya, hizi ni juhudi za Dkt. Samia Suluhu Hassan, tulikuwa hatuna hospitali ya wilaya, sasa tuna hospitali ya wilaya na vituo vya afya takriban vinne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwaomba TAMISEMI, ipo Kata ya Igwisi ina wakazi zaidi ya elfu sabini na mbili (72,000). Kata hii haina kituo cha afya, lakini Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, wote Wabunge wanafahamu, kwa miaka mitano ilikuwepo *program* ya kujenga vituo vya afya vya kimkakati katika kila jimbo, taarifa zilizopo ni kwamba yamebaki majimbo 93 ikiwemo Jimbo la Kaliua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri wa TAMISEMI, niombe tena kwa mara ya pili, niombe kwa mara ya tatu, wapeleke fedha hizi tuweze kupata kituo cha afya, wananchi waweze kutabasamu, mama zetu waweze kujifungua kwenye maeneo mazuri, safi, huku wakiwa wanapiga mluzi taratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujabaki nyuma kwa sababu kupitia jitihada za wananchi kwenye Kata ya Ugunga, Kata ya Ukumbi Siganga, tumeanzisha ujenzi wa vituo vya afya, ninaomba Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI iweze kupeleka fedha ili kukamilisha vituo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye eneo la barabara. Yamesemwa mengi, wananchi wanatambua ya kwamba kila msimu, kila mwaka mvua zinanyesha na mvua ni baraka, ni kweli, mvua zikinyesha tunalima, lakini ni kweli zina madhara yake barabara zimekatika. Niombe Wizara ya TAMISEMI basi iharakishe mpango wake wa kupata hizo fedha bilioni 98 kuweza kuwapelekea wananchi kwenye majimbo yote tuweze kutengenezewa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ujenzi wa barabara, lipo jambo ambalo nisipolisema wananchi wa Jimbo la Kaliua hawawezi wakanielewa, bahati nzuri na wewe umepita Jimboni kuninadi, tarehe 11 mwezi wa Septemba, 2025 alikuja Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama mwenye huruma, Mama mchapakazi, Mama anayeipenda Tanzania yake, aliwaahidi wananchi wa Kaliua kwamba anakwenda kufungua Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Tabora na Mkoa wa Shinyanga kwa kuijenga kiwango cha lami Barabara ya Mpanda – Ugala – Kaliua – Ulyankulu mpaka Kahama, barabara hii ina urefu wa kilometa 428.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa uchungu kwa sababu barabara hii ina muda wa takriban miaka 20 tunaiomba. Upembuzi yakinifu umekamilika, usanifu wa kina umekwishafanyika. Ukienda kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2015-2020, ukurasa wa 59 imeahidiwa, ujenzi bado haujaanza. Ukienda kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2020-2025, ukurasa wa 75, ahadi hii ilikuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya vizuri, imefanya na kukamilisha usanifu, ninaomba hata 2025 - 2030 kwenye Ilani hii imeahidiwa. Niwaombe sana Wizara ya Ujenzi na ninamwamini Waziri Mkuu na ninamwalika kwenye Mkoa wetu wa Tabora, akifika Tabora nitakuwa kiongozi wake wa msafara kumpeleka Kaliua aone jinsi ambavyo Serikali imefanya kazi kubwa ya kufungua uchumi. Dhamira ya Rais ni kufungua uchumi kwa kujenga barabara hii nina hakika pato la Serikali litaongezeka na kwa kujenga barabara hii mazao mbalimbali yatasafirishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu Kaliua ndiyo "Toronto" ya Tabora, ninaomba sana Wizara ya TAMISEMI, hatuna stendi ya kisasa, ninaomba kwa sababu tayari tumeshatenga eneo na halina mgogoro na halmashauri yetu tumeshatenga milioni 150. Sisi tuko tayari tumeshaanza kukimbia kuunga juhudi za Dkt. Samia Suluhu Hassan. Tunaomba wakamilishe kibali ujenzi uweze kuanza na ikiwezekana mtu-*support* kwa kianzio kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye sekta ya kilimo. Kaliua pamoja na Mkoa wa Tabora, tumbaku ndiyo dhahabu yetu. Zao la tumbaku ndiyo kimbilio letu, zao la tumbaku ndiyo jicho letu, Wanakaliua na wananchi kwa ujumla. Sote tunafahamu humu ndani sekta ya kilimo ina mchango mkubwa katika Serikali, sekta ya kilimo ina mchango mkubwa kufikia Dira ya Taifa 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana kwa takwimu Kaliua pekee tumezalisha kilo milioni 35, mauzo tumepata bilioni 212, lakini hizi zote tunampa maua Dkt. Samia Suluhu Hassan alipeleka ruzuku ya mbolea, alirahisisha mazingira safi na mbolea ilifika kwa wakati. Kwa msimu huu, zipo changamoto na ninaomba Wizara ya Kilimo isilale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kuna ucheleweshaji wa pembejeo za kilimo kwa msimu huu, ambapo msimu wanaanza kuandaa mwezi Agosti, mbolea inafika mwezi Novemba, hii siyo sawa kwa mkulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya pili ni ongezeko la gharama za uzalishaji, ongezeko limetokea kwenye upande wa mbolea. Ukienda kwenye mbolea ya *NPK* mwaka jana msimu uliopita ilikuwa ni dola 60.7 sasa hivi ni dola 63.8. Ukienda kwenye mbolea ya muhimu *CAN*, mwaka jana ilikuwa ni dola 30.34, mwaka huu msimu huu ni dola 34.08. Kama kweli tuna lengo la kumkomboa mkulima, tutazame gharama za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu kwa maana ya musimu huu bei ya tumbaku imeporomoka kwa kilo moja wastani ni dola 1.95. Msimu uliopita ilikuwa ni dola 2.15 kwa kilo moja. Naiomba Serikali yangu sikivu, Serikali ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali bingwa na hakuna asiyefahamu makubwa na uwezo ni kuamua sisi tufanye, ninaomba tumtazame mkulima wa tumbaku ili basi tuweze kulisafisha eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia changamoto ya mwisho ambayo Serikali niombe iweze kuifanyia kazi ni ucheleweshaji wa malipo ya fedha za wakulima. Mpaka leo tunavyozungumza wakulima wamelima msimu uliopita wakamaliza, wanadai kuna makampuni kama *MAGEFA, JFO,* na *OBAMACO* zinadaiwa fedha nyingi. Fedha hizi Halmashauri ndiyo tunazotegemea kama *cess.* Kwa mwaka jana mauzo yale ya bilioni 212, *cess* pekee yake iliyoenda Halmashauri ni bilioni 6.3. Tafsiri yake ni nini? Wakichelewa kulipa maana yake tunacheleweshwa na maendeleo. Niombe Serikali yangu sikivu ya Chama Cha Mapinduzi iweze kulifanyia kazi na haya makampuni yaweze kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, mnyonge mnyongeni haki yake mpeni. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambazo amezifanya, kwa fedha nyingi ambazo amepeleka kwenye Majimbo yetu, hakika leo hii ninashangaa hata Ndugu yangu Mheshimiwa Ado kuomba Katiba, omba maji! Leo hii watu wanatabasamu kwa

kuletewa maji ya Ziwa Victoria Tabora nzima na Majimbo mengine. Omba umeme! Tumepelekewa...

**MWENYEKITI:** Taarifa Mheshimiwa.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MSUKUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka kumweka sawa mchangiaji. Amesema "mnyonge mnyongeni haki yake mpeni'', Sasa mtu umeshamnyonga unampaje haki? Ninataka arekebishe aseme mtu anayefanya kazi vizuri tumpe hongera zake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JOSEPH E. TAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nimeipokea taarifa hiyo kwa mikono miwili, ninaongezea na miwili mingine kwa sababu hakuna kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hata vitabu vya Mungu vinasema, tumpate wapi mtu kama huyu? Hakika Mungu ametubariki Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa Kikao chetu cha Saba, Mkutano wa Tatu na shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamilika. Hivyo ninaomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho siku ya Jumanne, Tarehe 14 Aprili, 2026, saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.47 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumanne, Tarehe 14 Aprili, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*